
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII MKOA WA IRINGA




**Kimetayarishwa kwa Ushirikiano kati ya:**

TUME YA MIPANGO
DAR ES SALAAM
na
OFISI YA MKOA WA

**IRINGA**

# YALIYOMO

**Ukurasa**

DIBAJI .......... **IV**

## SEHEMU YA I

## 1.0 ARDHI, WATU NA HALI YA HEWA

1.1 Eneo la Mkoa Kijiografia .......... 1
1.2 Eneo la Ardhi: .......... 1
1.3 Maeneo ya Utawala: .......... 1
1.4 Makabila: .......... 3
1.5 Idadi ya Watu na Ongezeko lake: .......... 3
1.6 Wastani wa Watu kwa Kilometa ya Mraba: .......... 10
1.7 Uhamiaji: .......... 15
1.8 Ajira: .......... 17
1.9 Hali ya Hewa na Udongo: .......... 20
1.10 Mvua: .......... 23
1.11 Udongo: .......... 23
1.12 Kanda za Kilimo na Uchumi: .......... 25
1.13 Umbile la Ardhi, Mabonde na Mito: .......... 28

## SEHEMU YA II
## 2.0 UCHUMI WA MKOA

2.1 Utangulizi: .......... 30
2.2 Pato La Mwaka La Mkoa (GDP) Na Wastani Wa Pato La Mtu Binafsi Kwa Mwaka (Per Capita GDP) .......... 30
2.3 Sekta Za Uzalishaji: .......... 36
2.3.1 Kilimo: .......... 36
2.3.2 Mifugo: .......... 64
2.3.3 Maliasili: .......... 69
2.3.4 Viwanda: .......... 83
2.3.5 Madini: .......... 83

## SEHEMU YA III
## 3.0 MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

3.1 Mtandao wa Barabara: .......... 85
3.2 Usafiri wa Anga: .......... 89
3.3 Mtandao wa Mawasiliano: .......... 89
3.4 Nishati: .......... 90

# SEHEMU YA IV

## 4.0 HUDUMA ZA JAMII


**4.1 SEKTA YA ELIMU:** ........ 93
4.1.1 Shule za Awali: ........ 93
4.1.2 Elimu ya Msingi: ........ 95
4.1.3 Elimu ya Sekondari: ........ 118
4.1.4 Elimu ya Watu Wazima: ........ 122
4.1.5 Elimu ya Ufundi: ........ 125
**4.2 SEKTA YA AFYA:** ........ **125**
4.2.1 Zahanati: ........ 128
4.2.2 Vituo vya Afya: ........ 128
4.2.3 Huduma za Hospitali: ........ 129
4.2.4 Matarajio ya Umri wa Kuishi: ........ 132
4.2.5 Vifo vya Watoto wachanga na Watoto chini ya Umri wa miaka Mitano: ........ 133
4.2.6 Viwango vya Vifo vya Akina mama Wajawazito: ........ 136
4.2.7 Utapiamlo: ........ 139
4.2.8 Usafi wa Mazingira: ........ 142
**4.3 SEKTA YA MAJI:** ........ **144**
4.3.1 Huduma ya Maji Mjini: ........ 145
4.3.2 Usambazaji Maji Vijijini: ........ 149
4.3.3 Mifereji ya Maji Machafu: ........ 150


## SEHEMU YA V

## 5.0 MASUALA MENGINE KUHUSIANA NA MAENDELEO


5.1 Maendeleo ya Wanawake: ........ 151
5.2 Elimu ya Wanawake: ........ 154
5.3 Matatizo yanayojitokeza katika vikundi vya Wanawake: ........ 154
5.4 Ushirika: ........ 155
5.5 Shughuli za NGO's Mkoani Iringa: ........ 155


## SEHEMU YA VI


**6.0 MAENEO YENYE UTAJIRI KWA UWEKEZAJI** ........ **161**

**KIAMBATISHO "A"** ........ **169**

Mkoa wa Iringa kwa Kifupi ........ 169

**KIAMBATISHO "B"** ..... **171**
Wilaya ya Iringa Vijijini ..... 171
**KIAMBATISHO "C"** ..... **174**
Wilaya ya Njombe ..... 174
**KIAMBATISHO "D"** ..... **178**
Wilaya ya Makete ..... 178
**KIAMBATISHO "E"** ..... **181**
Wilaya ya Ludewa ..... 181
**KIAMBATISHO "F"** ..... **184**
Wilaya ya Mufindi ..... 184
**1.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU TANZANIA** ..... **187**
1.1 Mahali Ilipo: ..... 187
1.2 Mipaka Ya Nchi: ..... 187
1.3 Ukubwa/Eneo: ..... 187
1.4 Ukubwa Wa Eneo La Kila Mkoa Tanzania Bara ($Km^2$): ..... 187
1.5 Idadi Ya Watu: ..... 188
1.6 Matumizi Ya Ardhi (Ha): ..... 189
1.7 Ardhi Kwa Ajili Ya Kilimo Na Mifugo: ..... 189
1.8 Maziwa: ..... 189
1.9 Milima: (Mita Za Urefu Kutoka Usawa Wa Bahari) ..... 189
1.10 Hali Ya Hewa: ..... 190
**2.0 HUDUMA ZA JAMII** ..... **191**
2.1 Afya: ..... 191
2.2 Elimu: ..... 191
2.3 Maji: ..... 192
**3.0 HIFADHI ZA TAIFA:** ..... **192**

# *DIBAJI*

1. *Kadri tunavyoikaribia Karne ya 21, matatizo ya maendeleo vijijini katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, ndivyo yanavyozidi kuwa mengi na makubwa. Huduma za kijamii na kiuchumi zinadidimia na hivyo kusababisha nchi hizi kukabiliwa na tatizo la kushindwa kutoa huduma kwa msingi wa uendelevu. Kwa mfano, kwetu Tanzania viwango vya uandikishaji wa wanafunzi mashuleni vinazidi kushuka, hali ya upatikanaji wa chakula ni mbaya, vifo vya watoto wachanga na akina mama wajawazito vinaendelea kuongezeka, ukosefu wa ajira unaongezeka na kusababisha vijana wengi vijijini kuhamia mijini ambako tayari kuna msongamano mkubwa wa watu, n.k. Katika mkoa wa Iringa, msongamano kwenye ardhi unazidi kuongezeka, sambamba na kutoweka kwa misitu kwa kiwango cha kutisha.*

2. *Hali hii imejitokeza kutokana na sababu mbali mbali, kama vile kukosekana kwa mipango madhubuti ya maendeleo vijijini, pamoja na ufuatiliaji na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa programu za maendeleo na mikakati ya kisekta. Upungufu huu katika sera na utayarishaji na utekelezaji wa programu na mipango ya maendeleo vijijini katika nchi zinazoendelea, ni matokeo ya uhaba wa takwimu na habari za kutosha na za kuaminika kuhusu masuala ya maendeleo vijijini.*

3. *Utayarishaji na uchapishaji wa vitabu hivi vinavyoonesha hali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya kila Mkoa, ambao unafanyika na Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, ni hatua muhimu ya*

*kuelekea kwenye ufumbuzi wa tatizo la ukosefu au uhaba wa takwimu na taarifa muhimu.*

4. *Vitabu hivi vinatoa takwimu na taarifa za aina mbali mbali, zikiwemo za kijiografia, idadi ya watu, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, huduma za jamii, miundombinu ya kiuchumi pamoja na sekta za uzalishaji. Machapisho haya yametokea kuhitajika sana kama chanzo muhimu cha taarifa kwa viongozi na watu wote wenye dhamana ya kutunga sera, maafisa mipango, watafiti, wahisani na viongozi wa sekta mbalimbali za maendeleo nchini. Tume ya Mipango imeona umuhimu wa kuihusisha mikoa yote katika zoezi hili muhimu. Hivyo basi wasomaji wa machapisho haya wanakaribishwa kutoa maoni yao na kukosoa kwa lengo la kuboresha maudhui ya machapisho yatakayofuata, na hivyo kuyafanya kuwa yenye msaada zaidi kwa watumiaji.*

5. *Ningependa kutumia fursa hii, kwa mara nyingine, kutambua na kutoa kwa shukrani kubwa kwa msaada wa kifedha kutoka ubalozi wa Norway nchini, ambao umeiwezesha Tume ya Mipango na Mkoa wa Iringa, kutoa kitabu hiki kuelezea hali ya maendeleo ya mkoa huo. Mwisho napenda kuwashukuru sana watumishi wa Idara ya Mipango Mkoani Iringa, kwa juhudi zao kubwa walizofanya katika kufanikisha jukumu hili.*

***Nassoro W. Malocho (MB)***
***WAZIRI WA NCHI,***

***MIPANGO NA UREKEBISHAJI WA SEKTA YA MASHIRIKA YA UMMA.***

*Desemba, 1998*

## SEHEMU YA I

## 1.0 ARDHI, WATU NA HALI YA HEWA

### 1.1 Eneo la Mkoa Kijiografia

Mkoa wa Iringa uko katika Nyanda za juu za Kusini mwa Tanzania. Mkoa unapakana na ukanda mkavu wa kati wa Tanzania katika upande wa Kaskazini na kupakana Kusini na Ziwa Nyasa. Mkoa wa Iringa umetanda kati ya latitudo $7^0$ 05' na $12^0$ 32' kusini, na longitudo $33^0$ 47' hadi $36^0$ 32 Mashariki mwa Meridiani. Mkoa wa Iringa unapakana na Mikoa ya Dodoma na Singida upande wa Kaskazini, Mkoa wa Mbeya upande wa Magharibi, mkoa wa Morogoro upande wa Mashariki na Mkoa wa Ruvuma kwa upande wa Kusini. Ziwa Nyasa linatenganisha mkoa wa Iringa na nchi ya Malawi upande wa Kusini Magharibi mwa Tanzania.

### 1.2 Eneo la Ardhi:

Mkoa wa Iringa unaukubwa wa eneo lenye jumla ya kilomita za mraba 58,936 na ni wastani wa asilimia 74 tu ya eneo hili inafaa kwa shughuli za kilimo ambayo ni sawa na kilomita za mraba 43,935. Eneo linalosalia la kilomita za mraba zipatazo 15,001 ni eneo la maji, hifadhi ya mbuga za Taifa milima n.k.

Idadi ya watu waliopo Mkoani ni 1,208,914; idadi hii ya watu inaufanya Mkoa kuwa wa wastani kwa idadi ya watu nchini. Pamoja na kiwango hiki kikubwa cha watu kiwango cha msongamano wa watu 21.3 kwa kila kilomita za mraba (Sensa ya 1988) kinaufanya Mkoa wa Iringa kuwa moja wapo ya mikoa yenye msongamano mdogo wa watu nchini.

### 1.3 Maeneo ya Utawala:


Mkoa wa Iringa unazo wilaya sita, Mufindi, Iringa Vijijini, Iringa Manispaa, Njombe, Ludewa na Makete. Zipo Tarafa 31, kata 113 na vijiji 628, angalia Jedwali lifuatalo:-

**JEDWALI Na 1: ENEO LA ARDHI NA MAENEO YA UTAWALA, MKOA WA IRINGA**

| Wilaya | Ukubwa wa Eneo | Tarafa | Kata | Vijiji |
|---|---|---|---|---|
| Iringa (Vijijini na Manispaa) | 28,620 | 10 | 39 | 185 |
| Mufindi | 7,123 | 5 | 14 | 126 |
| Njombe | 10,668 | 7 | 25 | 172 |
| Ludewa | 8,397 | 4 | 20 | 50 |
| Makete | 4,128 | 5 | 15 | 95 |
| Jumla | 58,936 | 31 | 113 | 628 |

Chanzo: 1. Mkoa wa Iringa: Taarifa ya Maendeleo ya Kilimo 1994/95.
2. Sensa ya 1988 - Taarifa ya Kitaifa.

**Kielelezo 1: Eneo la Ardhi Kiwilaya, Mkoa wa Iringa**



## 1.4 Makabila:

Makabila makubwa mkoani Iringa ni Wahehe, Wabena, Wakinga na Wapangwa. Kabila la Kihehe ndilo kubwa kupita makabila mengine. Asilimia ipatayo 43 ya idadi ya watu wote Mkoani ni Wahehe. Watu wa kabila hili wanaishi wilaya za Iringa na Mfindi - kabila linalofuata kwa ukubwa ni Wabena ambao ni asilimia 37 ya wakazi wa Mkoa huu, Wakinga ni asilimia 11 na Wapangwa asilimia 3. Kabila la Kibena liko wilaya ya Njombe na eneo la Malangali likiwa linapakana na wilaya ya Ulanga na Kilombero (Mkoa wa Morogoro). Wakinga wako wilaya ya Makete na Wapangwa wako eneo la Malangali. Yapo pia makabila madogo kama vile Wakisi, Wamanda n.k ambao kwa ujumla wao wanachukua asilimia 6 iliyosalia ya watu Mkoani Iringa.

## 1.5 Idadi ya Watu na Ongezeko lake:

Idadi ya watu, mazingira na maendeleo yake ni mambo ya msingi yanayogusa maisha ya mwanadamu. Katika nchi yeyote, lengo la maendeleo huwa ni watu na ongezeko la kila mwaka la idadi ya watu kwa namna mbali mbali hugusa misingi ya rasilimali kwa namna nyingi. Kwa mfano kuongezeka kwa watu husababisha kuongezeka kwa mahitaji ya chakula, maji ardhi kwa ajili ya kilimo na mahitaji mengine mbali mbali. Hivyo ni muhimu kila mara kuainisha maswala katika uandaaji maendeleo na katika maswala yote ya mipango ya maendeleo kwa ngazi zote.

Mkoa wa Iringa ni mmoja wapo ya mikoa kumi nchini inayokuwa na idadi kubwa ya watu. Sensa ya 1988 ilionyesha Mkoa ulikuwa na idadi ya watu 1,208,914. Idadi hii ilikuwa sawa na asilimia 5.3 ya watu wote Tanzania Bara ukifuatia


mikoa ya Mbeya, Kagera, Morogoro, Tanga, Arusha na Dodoma, ambayo yote ina idadi ya watu ya wastani. Limekuwepo ongezeko la kila mwaka la wastani wa asilimia 2.7 Mkoani Iringa kati ya mwaka 1978 - 1988. Kutokana na ongezeko hili la kila mwaka inakisiwa kwamba Mkoa utakuwa umefikia idadi ya watu 1,678,302 ifikapo mwaka 2000 (Jedwali V). Jedwali II pia linalinganisha idadi ya watu kimkoa Tanzania Bara kulingana na Takiwmu za Sensa ya 1988.

**Jedwali Na. II Idadi ya Watu Tanzania Bara, Sensa ya 1988**

| | |
|---|---|
| Dodoma | 1,237,819 |
| Arusha | 1,351,675 |
| Kilimanjaro | 1,108,699 |
| Tanga | 1,283,636 |
| Morogoro | 1,222,737 |
| Pwani | 638,015 |
| Dar es Salaam | 1,360,850 |
| Lindi | 646,550 |
| Mtwara | 889,494 |
| Ruvuma | 783,327 |
| Iringa | 1,208,914 |
| Mbeya | 1,476,199 |
| Singida | 791,814 |
| Tabora | 1,036,293 |
| Rukwa | 694,974 |
| Kagera | 1,326,183 |
| Mwanza | 1,879,271 |
| Mara | 970,942 |
| Shinyanga | 1,763,960 |
| Kigoma | 853,263 |

| | |
|---|---|
| Jumla | 22,533,758 |

**Kielelezo Na. 2: Idadi ya Watu (Maelfu) na Viwango vya Ongezeko kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya Ruvuma na Rukwa (Mikoa Maarufu Kwa Uzalishaji wa ziada ya Mahindi).**




**JEDWALI NA. III: IDADI YA WATU NA VIWANGO VYA ONGEZEKO KWA MIKOA YA IRINGA, MBEYA RUVUMA NA RUKWA (MIKOA MAARUFU KWA UZALISHAJI WA ZIADA YA MAHINDI).**

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Viwango vya Ongezeko la Watu | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1967 | 1978 | 1988 | 1967 - 1978 | 1978 - 1988 |
| Iringa | 689,905 | 925,044 | 1,208,914 | 2.7 | 2.7 |
| Mbeya | 753,765 | 1,079,864 | 1,476,199 | 3.3 | 3.1 |
| Ruvuma | 395,47 | 561,575 | 783,327 | 3.2 | 3.4 |
| Rukwa | 276,091 | 451,897 | 694,974 | 4.5 | 4.3 |

Chanzo: Sensa ya Watu 1988

Ukilinganisha Mkoa wa Iringa na mikoa mingine mitatu (Jedwali III) Mkoa wa Iringa ulikuwa na kiwango kidogo zaidi cha ongezeko la watu la kila mwaka kulingana na matokeo ya Sensa ya idadi ya watu ya mwaka 1978 na 1988. Mkoa wa

Rukwa ulikuwa na ongezeko kubwa zaidi ya mikoa mingine mitatu kwa matokeo hayo hayo, lakini ni mkoa wenye idadi ndogo zaidi ya watu kulingana na Sensa zote tatu za watu (Jedwali Na. III).

**Jedwali IV: Idadi ya watu na Ongezeko la Kiwilaya, Mkoa wa Iringa 1978-1988**

| Wilaya | Sensa ya Watu | | | Viwango vya Ongezeko la kila mwaka 1978 - 1988 |
|---|---|---|---|---|
| | 1967 | 1978 | 1988 | |
| Iringa Vijijini | 252,627 | 290,101 | 363,605 | 2.7+ |
| Njombe | 318,811++ | 326,084* | 315,976 | 2.8 |
| Mufindi | 118,464 | 173,824 | 229,304 | 2.8 |
| Ludewa | - | 75,610 | 99,689 | 2.8 |
| Makete | - | - | 115,480 | 1.2 |
| Iringa Mjini | - | 57,182 | 84,860 | 4.5+ |
| **Jumla** | **689,905** | **922,801** | **1,208,914** | **2.7** |

Chanzo: Sensa ya Watu, 1,967, 1978 na 1988.

* Idadi ya watu kuwa kubwa Sensa ya 1978 inatokana na kwamba Njombe ilikuwa inajumuisha Wilaya ya Makete wakati huo.


\+ Ongezeko la idadi ya watu inatokana na takwimu zilizomo katika jalada la "SITUATION".

++ Idadi ya watu ilijumuisha idadi ya watu wa Wilaya ya Ludewa na Makete.

Ikichunguzwa kwa makini Jedwali Na. V linadhihirisha wazi kwamba kati ya Sensa za 1967 na 1988, mkoa wa Iringa ulipata ongezeko la asilimia 75 ya watu kutoka jumla ya watu 689,905 hadi 1,208,914. Vile vile inajionyesha kwamba ifikapo mwaka 2000 idadi ya watu mkoani Iringa itakuwa imeongezeka mara tatu ikilinganishwa na ile ya 1967. Ongezeko hili litakuwa kubwa kuliko lolote lililokwisha kupatikana, na kwa sababu hii kuna ulazima wa kudhibiti kiwango kikubwa kama hiki la sivyo kiwango cha uzalishaji chakula hakitatosheleza mahitaji ya chakula kwa idadi hiyo kubwa ya watu; vile vile huduma mbalimbali za kijamii hazitatosheleza mahitaji. Uzoefu umekwisha onyesha kuwa

ongezeko kubwa la haraka haraka la watu husababishwa hasa na viwango vya juu vya kuzaliana, mila na desturi za ndoa na kutotumia njia za uzazi wa mpango kama vile kutotumia njia za kuzuia mimba. Jedwali Na. V laendelea kuonyesha makisio ya idadi ya watu hadi mwaka 2000 kutokana na takwimu za Sensa za kiwilaya ya 1988 Mkoa wa Iringa.

**Kielelezo Na 3: Mwelekeo wa Ongezeko la Watu (maelfu) kutokana na wastani wa viwango vya ongezeko kiwilaya, Mkoa wa Iringa.**




**JEDWALI NA. V: MWELEKEO WA ONGEZEKO LA WATU KUTOKANA NA WASTANI WA VIWANGO VYA ONGEZEKO KIWILAYA, MKOA WA IRINGA.**

| Wilaya | Sensa ya 1967 | Sensa ya 1988 | Mwelekeo wa Ongezeko la Watu * | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1995 | 1998 | 2000 |
| Iringa Vijijini | 252,627 | 363,605 | 438,149 | 474,605 | 500,579 |
| Iringa Mjini | - | 84,860 | 115,482 | 131,784 | 143,911 |
| Mufindi | 118,467 | 229,304 | 278,202 | 302,232 | 319,481 |
| Njombe | *318,811 + | 315,976 | 383,359 | 416,472 | 440,121 |
| Ludewa | - | 99,689 | 120,946 | 131,392 | 138,853 |
| Makete | - | 115,480 | 127,520 | 132,166 | 135,357 |
| Jumla | 689,905 | 1,208,914 | 1,463,658 | 1,588,651 | 1,678,302 |

Chanzo: 1. Taarifa ya Sensa ya Watu ya 1967 na 1988
2. Takwimu: Tume ya Mipango, Dar es Salaam.
* Viwango vya ongezeko la watu vilivyotumika vimo katika Jedwali IV.

\+ Idadi ya Watu inajumuisha na ile ya watu wa wilaya mpya za Ludewa na Makete.

Jedwali Na. V laonyesha wazi kwamba wilaya zote isipokuwa wilaya ya Makete idadi ya watu katika wilaya hizo itaongezeka kwa kiwango cha asilimia 38 au zaidi katika kipindi cha miaka 12 kuanzia 1988 hadi 2000. Viwango hivi vya ongezeko la watu ni vikubwa sana ikilinganishwa na ongezeko la uzalishaji chakula mkoani. Upo ulazima wa kuchukua hatua madhubuti za kuongeza uzalishaji chakula kwa kiwango cha juu sana, lakini ukweli uliopo sasa ni kwamba uzalishaji chakula mkoani unaendelea kushuka. Mbinu ya pili ni kupunguza viwango vya ongezeko la watu kwa kutumia njia za uzazi wa mpango.

**Jedwali Na. VI: Mwelekeo wa Ongezeko la Watu Kijinsia kwa Takwimu za Sensa ya 1988**

| Wilaya | Sensa ya Watu 1988 | | | Makisio ya Idadi ya Watu 1988 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Iringa Vijijini | 174,624 | 188,981 | 363,605 | 227,919 | 246,658 | 474,577 |
| Iringa Mjini | 41,812 | 43,048 | 84,860 | 64,934 | 66,854 | 131,787 |
| Mufindi | 108,289 | 121,015 | 229,304 | 142,725 | 159,498 | 302,223 |
| Njombe | 145,465 | 170,511 | 315,976 | 191,723 | 224,733 | 416,456 |
| Ludewa | 46,609 | 53,080 | 99,689 | 61,431 | 69,959 | 131,390 |
| Makete | 48,442 | 67,038 | 115,480 | 54,580 | 75,532 | 130,112 |
| Jumla | 565,241 | 643,673 | 1,208,914 | 743,312 | 843,234 | 1,586,545 |

Chanzo: 1. Sensa ya Watu, 1988
2. Takwimu za viwango vya ongezeko la watu: Tume ya Mipango, Dar es Salaam.

Kama ilivyokwisha jieleza hapo awali katika Jedwali Na. IV viwango vya ongezeko la watu kwa mwaka ni vya juu sana. Hali hii inajidhihirisha pia katika Jedwali Na. V. Ongezeko la watu wanaume kwa wanawake katika wilaya zote isipokuwa Makete, itakuwa kwa kiasi kisichopungua asilimia 30 kati ya miaka 1988 hadi 1998. Wilayani Makete idadi hii itaongezeka kwa kiasi cha asilimia 13 tu kwa wanawake na wanaume.

## 1.6 Wastani wa Watu kwa Kilometa ya Mraba:

Wastani wa watu kwa kilomita ya mraba Mkoani Iringa ni wachache sana ikilinganishwa na ile ya Mikoa yenye watu wengi kwa kilomita ya mraba ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Tanga na Kagera. Kwa takwimu za Sensa ya 1988 mkoa wa Iringa ulikuwa na wastani wa watu 21.3 kwa kila kilomita ya mraba, kiwango hiki kiko chini ya kiwango cha kitaifa cha wastani wa watu 26 kwa kila kilomita ya mraba.

**Jedwali Na. VII: Wastani wa watu kwa kilomita ya mraba na asilimia ya ongezeko (1978/88) Kimkoa, 1978 na 1988 (Taarifa ya Sensa), Tanzania Bara.**

| Mkoa | Watu kwa Kilomita ya Mraba - Sensa ya: | | Ongezeko la Asilimia (1978/1988) |
|---|---|---|---|
| | 1978 | 1988 | |
| Dar es Salaam | 553.2 | 976.9 | 77 |
| Mwanza | 73.3 | 95.4 | 31 |
| Kilimanjaro | 68.1 | 83.7 | 22 |
| Mtwara | 46.2 | 53.2 | 15 |
| Tanga | 38.9 | 48.1 | 23 |
| Kagera | 35.5 | 46.6 | 32 |
| Mara | 33.2 | 43.7 | 49 |
| Shinyanga | 26.1 | 34.9 | 34 |
| Dodoma | 23.5 | 30.0 | 28 |
| Mbeya | 17.9 | 24.5 | 37 |
| Kigoma | 17.5 | 23.1 | 32 |
| **Iringa** | **16.2** | **21.3** | **31** |
| Pwani | 15.9 | 19.6 | 24 |
| Morogoro | 13.3 | 17.3 | 30 |
| Arusha | 12.4 | 16.5 | 29 |
| Singida | 11.3 | 16.0 | 45 |
| Tabora | 10.7 | 13.6 | 27 |
| Ruvuma | 8.9 | 12.3 | 38 |
| Rukwa | 8.0 | 10.1 | 23 |
| Lindi | 6.6 | 9.8 | 53 |
| Jumla | 19.8 | 26.2 | 32 |

Chanzo: 1988 National Profile: Analytiical Report (1988 Census).

Jedwali Na: VII linalinganisha wastani wa watu kwa kilomita ya mraba kimkoa kwa Sensa mbili za 1978 na 1988; linaonyesha vile vile ongezeko la watu kwa kilomita ya mraba kwa hicho kipindi. Mkoa umekuwa na ongezeko la watu kwa kilomita ya mraba kutoka watu 16.2 mwaka 1978 hadi 21.3 mwaka 1988. Hiki ni kiwango cha ongezeko cha asilimia 31 kati ya Sensa ya 1978 na ile ya 1988. Ongezeko hili la watu kwa kilomita ya mraba yawezekana kusababishwa na ongezeko la kawaida la watu na watu kuhama na kuingia kutoka mikoa mingine. Kiwango cha watu 21.3 kwa kilomita ya mraba ni cha chini sana ikilinganishwa na nchi za kimataifa (Mbaruku, 1983). Hata hivyo, Mbaruku anafafanua kuwa viwango vya watu kwa kilomita ya mraba huwa ni makisio tu na huwa haizingatii tofauti inayoweza kutokea katika sehemu husika.

**Jedwali Na. VIII: Wastani wa watu kwa kilomita ya Mraba na mgawanyiko Kiwilaya, Mkoa wa Iringa, 1988 na Matarajio ya 1995 na 2000**


| Wilaya | Eneo la Nchi Kavu (Km$^2$) | Idadi ya Watu Sensa ya 1988 | Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kilomita ya mraba (1988) | Makisio ya Idadi ya Watu 1995 | Makisio ya Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kilomita ya mraba (1995) | Makisio ya Idadi ya Watu 2000 | Makisio ya Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kilomita ya mraba (2000) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 28,620 | 363,605 | 12.7 | 438,149 | 15.3 | 500,579 | 17.5 |
| Mufindi | 7,123 | 229,304 | 32.2 | 278,202 | 39.0 | 319,481 | 44.8 |
| Iringa Mjini | 2,072 | 84,860 | 41.0 | 115,482 | 55.7 | 143,911 | 69.5 |
| Njombe | 10,668 | 315,976 | 29.6 | 383,359 | 36 | 440,121 | 41.2 |
| Ludewa | 6,325 | 99,689 | 15.8 | 120,946 | 19.1 | 138,853 | 22 |
| Makete | 4,128 | 115,480 | 28 | 127,520 | 30.9 | 135,357 | 32.8 |
| Jumla | 58,936 | 1,208,914 | 21.3 | 1,463,568 | 24 | 1,678,302 | 28.5 |

Chanzo: 1. Sensa ya Watu 1988
2. Takwimu: Tume ya Mipango, Dar es Salaam.

Jedwali VIII linaonyesha jinsi mgawanyiko wa Watu Mkoani Iringa unavyotofautiana. Inadhihirika kwamba wilaya ya Iringa

Vijijini pamoja na kuwa na idadi ya watu wapatao 365,605 tu linachukua karibu asilimia 50 ya eneo lote la nchi kavu Mkoani. Wilaya za Mufindi, Njombe na Makete zikiwa na idadi ya watu 660,760 kwa pamoja (1988) zimesalia na asilimia 38 tu ya nchi kavu ya mkoa wa Iringa. Hata hivyo kulingana Sensa ya Idadi ya Watu ya 1988na wilaya ya Iringa mjini ilikuwa na wastani wa watu wengi zaidi kwa kilomita ya mraba, ikifuatiwa na Mufindi, Njombe, Makete na Ludewa.

**Kielelezo Na. 4: Idadi ya Watu (Maelfu) Kijinsia, Kiwilaya Mkoani Iringa 1988**




**JEDWALI Na. IX: IDADI YA WATU KIJINSIA, IDADI YA KAYA NA WASTANI WA UKUBWA WA KAYA KIWILAYA MKOANI IRINGA 1988.**

| Wilaya | Jinsia | | | Idadi ya Kaya | Wastani wa Ukubwa wa Kaya |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | | |
| Iringa Vijijini | 174,624 | 188,981 | 363,605 | 72,665 | 5.0 |
| Iringa Mjini | 41,812 | 43,048 | 84,860 | 18,283 | 4.6 |
| Mufindi | 108,289 | 121,015 | 229,304 | 47,327 | 4.8 |
| Njombe | 145,465 | 170,511 | 315,976 | 65,075 | 4.8 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ludewa | 46,609 | 53,080 | 99,689 | 19,981 | 4.9 |
| Makete | 48,442 | 67,038 | 115,480 | 25,148 | 4.5 |
| Jumla | 565,241 | 643.673 | 1,208,914 | 248,479 | 4.8 |

Chanzo: Sensa ya Watu, 1988

Takwimu katika Jedwali Na. IX zinaonyesha kuwa wastani wa ukubwa wa Kaya ni juu zaidi kwa wilaya ya Iringa Vijijini, ukifuatiwa na wilaya za Ludewa, Mufindi na Njombe. Idadi kubwa ya watu kwa Kaya kwa kiwango fulani inachangiwa na idadi kubwa ya Watu Mkoani humo kuoa zaidi ya mwanamke mmoja; na uzazi mwingi kwa wanawake.

**JEDWALI Na. X: IDADI YA WATU KWA MAKUNDI KI UMRI NA JINSIA KIWILAYA, MKOA WA IRINGA, 1988**

| Kundi la Umri (Miaka) | Iringa Vijijini | | Iringa Mjini | | Mufindi | | Njombe | | Ludewa | | Makete | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ume | Wake | Ume | Wake | Ume | Wake | Ume | Wake | Ume | Wake | Ume | Wake |
| 0 - 4 | 30,372 | 30,576 | 5,245 | 6,838 | 19,304 | 20,070 | 26,377 | 26,295 | 8,492 | 8,734 | 7,875 | 8,100 |
| 5 - 14 | 56,636 | 56,535 | 11,816 | 13,600 | 34,816 | 35,795 | 47,209 | 48,769 | 15,189 | 16,042 | 15,628 | 16,189 |
| 15 - 44 | 64,124 | 79,234 | 17,142 | 20,176 | 40,263 | 51,623 | 52,855 | 70,903 | 16,328 | 21,822 | 14,550 | 21,906 |
| 45 - 64 | 13,933 | 17,561 | 4,047 | 2,736 | 8,239 | 11,146 | 11,333 | 17,078 | 4,153 | 5,574 | 4,799 | 8,089 |
| 65+ | 6,467 | 6,477 | 1,354 | 1,557 | 3,781 | 3,861 | 5,210 | 6,617 | 1,718 | 2,006 | 2,432 | 2,776 |

Chanzo: Sensa ya 1988: Mkoa wa Iringa.

Jedwali Na. X linaonyesha idadi ya watu kulingana na umri. Watoto walio na umri kati ya miaka 0 - 14 ni sawa na asilimia 47 ya idadi ya watu wote Mkoani Iringa, ambapo watu walio kati ya miaka 15 - 44 (Watu wazima) ni sawa na asilimia 39 ya idadi ya watu Mkoani. Kundi la umri wa kufanya kazi, kati ya miaka (15 - 64) linalotegemewa ni asilimia 48. Kundi tegemezi ni lile kati ya miaka 0-14 na lile la Wazee miaka 65 na zaidi linachukua asilimia 50 ya watu wote mkoani. Hali hii inamaanisha kwamba uwiano kati ya kundi tegemezi na wategemewa ni zaidi ya asilimia 100 yaani 104.2%. Hii ina

maana kwamba kila watu 100 wenye uwezo wa kufanya kazi Mkoani Iringa wanalisha watu 104.2, hali hii ni mbaya kiuchumi kwa nchi changa inayojenga uchumi na uchumi wake bado unakua. Hii ni kwa sababu idadi kubwa ya watu tegemezi inahitaji huduma mbali mbali za kijamii na chakula.

Jedwali Na. XI linaonyesha uwiano kati ya kundi tegemezi na wategemewa kiwilaya. Wilaya za Ludewa, Makete na Iringa Vijijini zinaonyesha viwango vya juu sana vya uwiano tegemezi.


**Jedwali Na. XI: IDADI YA WATU KULINGANA NA MAKUNDI KI UMRI NA UWIANO KATI YA KUNDI TEGEMEZI NA ATEGEMEWA KIWILAYA, MKOANI IRINGA, SENSA YA 1988**

| Wilaya | Idadi ya Watu Kulingana na Umri | | | | | Uwiano wa tegemezi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0 - 4 | 5 - 14 | 15 - 44 | 45 - 64 | 65+ | |
| Iringa Vijijini | 60,948 | 113,171 | 143,358 | 31,494 | 12,944 | 106.98 |
| Iringa Mjini | 12,083 | 25,416 | 37,318 | 6,783 | 2,911 | 91.63 |
| Mufindi | 39,374 | 70,611 | 91,886 | 19,385 | 7,642 | 105.71 |
| Ludewa | 17,226 | 31,231 | 38,150 | 9,727 | 3,724 | 108.99 |
| Makete | 15,975 | 31,817 | 36,456 | 12,888 | 5,208 | 107.41 |
| Njombe | 52,672 | 95,978 | 123,758 | 28,411 | 11,827 | 105.46 |
| Jumla | 198,278 | 368,224 | 470,926 | 108,688 | 44,256 | 104.4 |

Chanzo: Tume ya Mipango: Mkusanyo wa Takwimu kutokana na Sensa ya Idadi ya Watu, 1988 Mkoa wa Iringa.

**Kielelezo Na. 5: Idadi ya Watu Kufuatana na Makundi ki Umri na Uwiano kati ya Kundi Tegemezi na Wategemewa Kiwilaya, Mkoani Iringa, Sensa ya 1988**

**Maelfu**




## 1.7 Uhamiaji:

Uhamiaji maana yake kubadili makazi kutoka eneo moja kwenda eneo jingine (Shyrock, H.S. and Siegel, J.S.). Baadhi ya sababu au mambo muhimu yanayoweza kuleta mabadiliko katika idadi ya watu katika eneo fulani ni uzazi, vifo na uhamiaji. Uhamiaji kwa kiwango kikubwa waweza kubadili idadi ya watu, pia unaweza kubadili mwelekeo wa idadi ya watu kutokana na kuzaliana. Jedwali Na. XII linaonyesha uhamiaji wa maisha/kudumu kimkoa Tanzania Bara. Mkoa wa Dar es Salaam una kiwango cha juu sana ukifuatiwa na Mikoa ya Arusha, Tabora, Mbeya na Morogoro. Dar es Salaam ina idadi kubwa ya wahamiaji kuliko mikoa yote nchini; sababu kuu ni kutokana na umaarufu wa mkoa wenyewe ukiwa ndiyo mji mkuu wa nchi. Idadi kubwa ya watu huingia wakitafuta ajira. Mkoa wa Iringa ni wa pili kwa kuwa na idadi ndogo ya watu waingiao, ukifuatiwa na mikoa ya Kigoma na Mtwara.

Jedwali Na. XII linabainisha zaidi kwamba idadi ya watu waliouhama Mkoa wa Iringa ilikuwa watu 169,480, hali hii pia inaonyesha idadi kubwa zaidi ya watu waliotoka kuliko

walioingia mkoa huu. Kulikuwa na watu 120,198 zaidi waliouhama mkoa kuliko waliohamia (Sensa ya 1988). Mwelekeo wa watu wengi kuhama kuliko kuhamia unaufanya mkoa wa Iringa kuwa wa pili, ukitanguliwa na mkoa wa Kilimajaro ambao ulikuwa na watu 123,383 zaidi waliouhama kuliko waliohamia mkoani humo.

**JEDWALI Na. XII: UHAMIAJI WA MAISHA/KUDUMU, KIMKOA, TANZANIA BARA (SENSA YA WATU, 1988).**

| Mkoa | Uhamiaji wa Maisha /kudumu Mkoani | Uhamiaji wa Maisha Nje ya Mkoa | Tofauti halisi Kati ya Uhamaji na Uhamiaji | Uhamiaji kwa Jumla (Gross Migration) |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 89,900 | 190,985 | - 101,085 | 280,885 |
| Arusha | 218,427 | 76,703 | 141,724 | 295,130 |
| Kilimanjaro | 93,040 | 217,423 | - 124,383 | 310,463 |
| Tanga | 98,747 | 150,915 | - 52,168 | 249,662 |
| Morogoro | 172,393 | 141,956 | 30,437 | 314,349 |
| Pwani | 103,804 | 207,716 | - 103,912 | 311,520 |
| Dar es Salaam | 651,246 | 150,625 | 500,621 | 801,871 |
| Lindi | 95,200 | 145,031 | - 49,831 | 240,231 |
| Mtwara | 46,299 | 144,988 | - 98,689 | 191,287 |
| Ruvuma | 66,442 | 81,661 | - 15,219 | 148,103 |
| **Iringa** | **49,282** | **169,480** | **- 120,198** | **218,762** |
| Mbeya | 160,377 | 113,378 | 46,999 | 273,755 |
| Singida | 86,651 | 150,531 | - 63,880 | 237,182 |
| Tabora | 241,729 | 175,359 | 66,370 | 417,088 |
| Rukwa | 87,599 | 49,294 | 38,305 | 136,893 |
| Kigoma | 26,795 | 129,718 | - 102,923 | 156,513 |
| Shinyanga | 288,210 | 281,447 | 6,763 | 569,657 |
| Kagera | 103,713 | 109,693 | - 5,980 | 213,406 |
| Mwanza | 270,142 | 303,646 | - 33,504 | 573,788 |
| Mara | 75,987 | 115,865 | - 39,878 | 191,852 |
| Jumla | 3,025,983 | 3,106,414 | - 80,431 | 6,132,397 |

Chanzo: Sensa ya Idadi ya Watu 1988: Taarifa ya Kitaifa.

## 1.8 Ajira:

Taarifa ya kitaifa ya Sensa ya Idadi ya Watu ya 1988 inasema kwamba watu wote waliokuwa wa umri wa miaka 10 na zaidi na waliokuwa hawana kazi (yakuajiriwa au kujiajiri) waliwekwa katika kundi la watu wasiokuwa na ajira. Orodha

ya watu waliokuwa hawana ajira mkoani Iringa imeonyeshwa katika Jedwali Na. XIII.

**Jedwali Na. XIII: IDADI YA WATU WENYE MIAKA 10 NA ZAIDI KIJINSIA, KIWILAYA NA SHUGHULI ZAO KATIKA MKOA WA IRINGA, 1988**

| Wilaya | Kazi za Kiofisi na Uuzaji katika Maduka | Shughuli za Kilimo | Ajira za Kiwandani na nyinginezo | Idadi ya Wasiokuwa na ajira |
|---|---|---|---|---|
| | Jinsia : A. Wanaume | | | |
| Iringa Vijijini | 727 | 69,591 | 3.403 | 33,568 |
| Iringa Mjini | 1,226 | 7,358 | 7,713 | 8,071 |
| Mufindi | 1,104 | 38,463 | 4,397 | 21,270 |
| Njombe | 935 | 55,125 | 3,465 | 29,136 |
| Ludewa | 168 | 17,971 | 728 | 9,148 |
| Makete | 221 | 17,482 | 573 | 9,703 |
| Jumla | 4,381 | 205,990 | 20,279 | 110,896 |
| Wilaya | Jinsia : B. Wanawake | | | |
| Iringa Vijijini | 541 | 91,830 | 1,507 | 34,245 |
| Iringa Mjini | 1,983 | 14,567 | 1,745 | 11,793 |
| Mufindi | 758 | 56,611 | 966 | 23,608 |
| Njombe | 824 | 83,028 | 1,164 | 32,101 |
| Ludewa | 155 | 25,474 | 849 | 10,113 |
| Makete | 182 | 29,849 | 174 | 10,207 |
| Jumla | 4,443 | 301,359 | 6,405 | 122,067 |
| Wilaya | Jinsia : C. Zote Mbili | | | |
| Iringa Vijijini | 1,368 | 161,421 | 4,910 | 67,813 |
| Iringa Mjini | 3,209 | 21,925 | 9,458 | 19,864 |
| Mufindi | 1,862 | 95,074 | 5,363 | 44,878 |
| Njombe | 323 | 43,445 | 1,577 | 19,261 |
| Ludewa | 403 | 47,331 | 747 | 19.910 |
| Makete | 1,759 | 138,153 | 4,629 | 61,237 |
| Jumla | 8,924 | 507,349 | 26,684 | 232,963 |

Chanzo: 1. Sensa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1988 Mkoa wa Iringa.
2. Mkusanyo wa Takwimu: Tume ya Mipango.

Jedwali Na. XIII linaonyesha kwamba jum;la ya watu 232,963 Mkoani Iringa walikuwa hawana ajira kati ya hawa, 122,067 walikuwa wanawake sawa na asilimia 52 ya watu wote waliokuwa hawana ajira. Wanaume 110,896 sawa na asilimia 48 walikuwa hawana ajira. Wilaya ya Iringa Vijijini ilikuwa

ikiongoza kwa wanawake na wanaume wasiokuwa na ajira Mkoani Iringa. Wilaya ya Njombe ilifuatia ikiwa na Wanawake 32,101 na wanaume 29,136 waliokuwa hawana ajira. Wilaya za Iringa Mjini na Makete zilikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wasiokuwa na ajira wa jinsia zote mbili. Taarifa hii zaidi inadhihirisha kwamba idadi kubwa ya watu katika wilaya zote walikuwa wanaajira zinazohusiana na shughuli za kilimo. Idadi hii ingekuwa kubwa zaidi iwapo sekta hii ya kilimo ingeendelea kutoa tija ya kuvutia. Kushuka kwa uzalishaji wa sekta hii hasa katika wilaya ya Iringa Vijijini (Mfano Tarafa za Ismani na Pawaga) kumekatisha tamaa uwekezaji katika sekta hii. Taarifa zaidi zinaonyesha ongezeko la wadudu waharibifu wa mazao, mvua chache zinazoaminika katika maeneo mengi; huduma duni, kuongezeka kwa ardhi isiyokuwa na rutuba; ubovu wa miundombinu na upatikanaji hafifu na uhaba wa madawa ya mimea, mbolea na bei kubwa ya pembejeo zimeifanya sekta ya kilimo Mkoani kuwa siyakuvutia kiuchumi kushindwa kukidhi mahitaji ya ajira kwa pindi chote cha mwaka kwa watu wanaotegemea sekta hii kwa maisha yao.

## 1.9 Hali ya Hewa na Udongo:

Zipo kanda tatu zinazotofautisha sehemu mbalimbali za Mkoa kihali ya hewa. Nyanda hizi ni Nyanda za juu, Nyanda za kati na Nyanda za chini.

### a) **Nyanda za Juu**:

Nyanda hizi ni za mwinuko mkubwa wa kati ya mita 1,600 hadi mita 2,700 kutoka usawa wa bahari. Ukubwa wa Kanda hii unakaribia kilomita za mraba 22,570. Ukanda huu unachukua sehemu ya mashariki

ya wilaya za Iringa na Mufindi, sehemu ya kati na masahriki ya wilaya ya Njombe; vile vile wilaya za Ludewa na Makete. Hali ya joto katika ukanda huu kwa kawaida ni chini ya nyuzi 15 sentigredi. Ukanda huu unapata mvua nyingi kati ya milimeta 1,000 hadi 1,600 kwa mwaka. Mvua hunyesha kwa muda mrefu kati ya siku 200 hadi 280.

b) **Nyanda za Kati:**

Ukanda huu uko kati ya urefu wa mita 1,200 hadi 1,600 kutoka usawa wa bahari na unajumuisha eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 17,500. Maeneo ya Mkoa yaliyo katika ukanda huu ni sehemu ya kati ya eneo la Mkoa hasa wilaya ya Mfindi. Hali ya joto iko kati ya nyuzi 20 hadi 25 sentigradi na mvua za wastani kati ya milimeta 600 hadi 1000 kwa mwaka.

c) **Nyanda za Chini**:

Ukanda huu uko kati ya milimeta 900 hadi 1200 kutoka usawa wa bahari; ukubwa wa ukanda wafikia kilomita za mraba 5,940. Sehemu za mkoa zilizo katika ukanda huu ni sehemu za tambarare za Iringa Kaskazini sambamba na mto Ruaha. Hali ya joto ni kati ya nyuzi 20 hadi 25 na mvua chache kati ya milimeta 500 hadi 600 kwa mwaka. Udongo wa ukanda huu ni mwekundu na wa kahawia ukiwa aina ya tifutifu na wenye rutuba nyingi kuliko sehemu nyingine za mkoa.

## 1.10 Mvua:

Mkoa wa Iringa una msimu mmoja tu wa mvua inayonyesha kati ya Novemba hadi Mei. Ukame katika Nyanda zenye mvua nyingi huwa mfupi zaidi kuanzia mwezi Juni hadi Septemba pepo kavu na baridi za kusini mashariki (monsoon) huvuma na wakati huo huwa ni kiangazi.

## 1.11 Udongo:

Mkoa wa Iringa una aina ya pekee ya maumbo na umeainishwa kwa kuwa na hali ya hewa ya aina mbali mbali na aina nyingi za udongo. Kwa mfano mvua za masika hutofautiana kati ya sehemu na sehemu, huanzia milimeta 500 hadi zaidi ya milimeta 1600. Nyanda za mwinuko/milima ni zenye udongo mwekundu au aina ya njano mwepesi na rutuba ndogo kutokana na kuchujika na mvua nyingi. Udongo aina hii wahitaji kurutubishwa mara kwa mara ili kuzalisha mazao mengi na mazuri. Udongo una upungufu wa madini ya aina ya calcium, magnesium na mengine muhimu. Ramani ya Mkoa wa Iringa hapo chini inaonyesha mgawanyiko wa kanda kuu tatu za kilimo na uchumi.

**RAMANI MKOA WA IRINGA KUONYESHA KANDA ZA KILIMO NA UCHUMI**

### 1.12 Kanda za Kilimo na Uchumi:

Mkoa wa Iringa waweza pia kugawanywa katika kanda tatu tofauti kwa misingi ya matumizi ya kiuchumi ya maeneo, maeneo ya kilimo, mimea na ufugaji.

a) **Ukanda wa Juu**:

Ukanda wa juu ni pamoja na tarafa ya Kilolo na Kata ya Udekwa katika wilaya ya Iringa, tarafa za Kibengu, Kasanga na Ifwagi katika wilaya ya Mufindi; tarafa za Lupembe, Igominyi na Imalinyi katika wilaya ya Njombe; tarafa za Mlangali na Mwengi katika wilaya ya Ludewa na pia tarafa zote za wilaya ya Makete Kasoro kata za Mfumbi na Ikuwo. Ukanda huu kwa kawaida hali ya joto huwa chini ya nyuzi 15 sentigredi na hupata mvua nyingi sana kati ya milimeta 1000 hadi 1600 kwa mwaka. Ukanda una misitu mikubwa, maeneo makubwa ya nyasi na misitu ya miombo. Zao kuu linalolimwa ni mahindi ambalo ni zao kuu la chakula. Mazao mengine ya chakula yanayolimwa katika kanda hii ni pamoja na ndizi na njegere. Mazao makuu ya biashara ni chai, kahawa, ngano na pareto. Matunda yanayostahimili hali ya ubaridi hulimwa pia. Ng'ombe wa asili na ng'ombe wa maziwa wanafugwa na pia wanyama wengine kama vile nguruwe, sungura na kondoo.

b) **Ukanda wa Kati:**

Maeneo yaliyomo katika ukanda huu ni tarafa za Mazombe, Mlolo, Kiponzelo na Kalenga, vile vile na kata za Kihorogota na Nduli katika wilaya ya Iringa;

tarafa za Sadani na Malangali katika wilaya ya Mufindi; tarafa za Mdandu, Makambako ma Wanging'ombe katika wilaya ya Njombe; tarafa za Masasi na sehemu ya Mwambao katika wilaya ya Ludewa pia kata ya Iluwa katika wilaya ya Makete. Hali ya joto huwa kati ya nyuzi 15 - 20 sentigredi na wastani wa mvua kati ya milimeta 600 na 1000 kwa mwaka. Ukanda unajulikana kwa kuwa na maeneo makubwa ya nyasi, vichaka na miombo. Yapo maeneo ya misitu iliyopandwa kusini magharibi mwa Mafinga. Zao la mahindi ambalo ni zao la chakula hulimwa kwa wingi. Vile vile mazao kama maharage, viazi vitamu, mboga, njerege na matunda hulimwa. Kama ilivyo katika ukanda wa juu ng'ombe kwa ajili ya nyama na ng'ombe wa maziwa , kondoo, sungura, nguruwe na mbuzi hufugwa.

c) **Ukanda wa Chini:**

Maeneo ya Mkoa wa Iringa yaliyomo katika ukanda huu ni pamoja na tarafa za Pawaga, Idodi, Izazi, Mahenge na kata ya Malengamakali katika wilaya ya Iringa. Kawaida ukanda huu ni wa ukame, ukiwa na hali ya joto kwa wastani kati ya nyuzi 20 hadi 25 sentigredi. Vile vile ukanda hupata mvua kidogo tu wakati wa masika kati ya milimeta 500 hadi 600 kwa mwaka. Kutokana na hali ya hewa ya sehemu hii mazao ya chakula yalimwayo huwa yale yenye kustahimili ukame kama vile mtama na mihogo na ndiyo mazao makuu ya chakula eneo hilo. Vile vile mazao ya karanga, mpunga, ndizi, mboga, matunda na zabibu hulimwa. Mifugo muhimu ifugwayo ukanda huu ni ng'ombe wa asili, mbuzi, kondoo na punda.

## 1.13 Umbile la Ardhi, Mabonde na Mito:

### i) Umbile la Ardhi:

Sehemu kubwa ya mkoa wa Iringa ina umbile la mfululizo wa milima ya Kipengere na Livingstone kwa upande wa kusini; na milima ya Udizungwa ambayo hutenganisha mikoa ya Iringa na Morogoro. Sehemu ya kaskazini ya Mkoa wa Iringa ni tambarare, pia na sehemu za mwinuko zilizokatishwa na sehemu ya mashariki ya bonde la ufa ambao Mto Ruaha hupita. Mkoa wa Iringa una mwinuko wa nchi kutoka usawa wa bahari kati ya meta 500 hadi kuvuka meta 2000 katika milima ya Kipengere. Pamoja na kuwepo kwa bonde la ufa vile vile kuna uwanda wa juu wenye sehemu zilizopindika. Uwanda wa juu umechukua sehemu kubwa ya mkoa uwanda huu umekatishwa sehemu nyingi na mabonde ya miteremko mikali yatokanayo na mimomonyoko ya ardhi ya miaka mingi tangu nyakati za Jurassic.

### ii) Mabonde na Mito:

Mkoa wa Iringa ni moja wapo ya chanzo cha mito inayotiririka katika Bahari ya Hindi. Mto Ruaha Mkuu na mdogo huunganika na Mto Rufiji nje ya Mkoa wa Iringa na kufanya muungano huo kuwa Bonde la Mto Rufiji. Mtiririko wa maji ya mito hutegemea majira ya mwaka, huwa mengi wakati wa mvua. Ujenzi wa bwawa la Mtera katika wilaya ya Iringa Vijijini umefanya bwawa hili kuwa chanzo muhimu cha umeme kutokana na nguvu ya maji, na hii pia kwa kiwango kikubwa imebadilisha mtitiriko wa maji kuelekea mto

Ruaha Mkuu.  Mkoani Iringa uwanda wa kati umeigawa mito katika sehemu mbili:  Mito inayotiririka kuelekea kaskazini na ile inayoelekeza maji yake kusini.  Mito inayotiririka kuelekea kaskazini yote huunganika na kufanya mto mmoja Mto Ruaha Mkuu ambao nao huunganika na kufanya kile kinachojulika kama Bonde la Mto Rufiji.  Mito inayotiririka kusini huunganika na mito Rufiji na Kilombero ambayo nayo huingiza maji yake katika mto Rufiji.  Sehemu kubwa ya kusini ya Mkoa wa Iringa humwaga maji yake ndani ya ziwa Nyasa ambalo pia hupitia mito ya Shire na Zambezi huunganika na Bahari ya Hindi.

# SEHEMU YA II

## 2.0 UCHUMI WA MKOA

### 2.1 Utangulizi:


Shughuli muhimu za kiuchumi za wakazi wa Mkoa wa Iringa ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Zao la mahindi ni chakula kikuu mkoani. Vyakula vingenevyo vitumiwavyo na wakazi wa humo mkoani ni ngano (kwa wale waishio ukanda wa juu), mtama, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage, muhogo, mpunga, karanga, nyanya, matunda na mboga.

Mazao makuu ya biashara ni tumbaku, pareto, chai, alizeti, kahawa na vitunguu. Wakazi wa Mkoa kila mmoja ana pato la wastani la T.Shs. 64,502 kila mwaka. Mwaka 1994 kiwango hiki kilikuwa cha juu kupita kile cha wastani wa kitaifa ambacho ni Tshs. 62,138 kwa kipindi hicho hicho (National Accounts of Tanzania 1976 - 1994, 11th Edition August, 1995). Hata hivyo pato la kila mtu kwa mwaka kwa wakazi wa Mkoa wa Iringa bado liko chini zaidi ya asilimia 84.36 ya T.Shs. 412,500 pato la chini kabisa la kila mtu kwa mwaka katika nchi za Umoja wa Madola.

### 2.2 Pato la Mwaka la Mkoa (GDP) na wastani wa pato la mtu binafsi kwa mwaka (Per Capita GDP)

Pato la Taifa huelezwa kuwa ni thamani ya bidhaa na huduma zilizoko katika soko huria zilizozalishwa au kutolewa nchini kabla ya punguzo la thamani hizo kutokana na uchakavu wa nyenzo zilizotumika kuzalisha au katika utoaji wa huduma hizo.

**Kielelezo Na. 6: Mapato ya Mkoa, Mikoa Minne Mashuhuri kwa Uzalishaji wa Mahindi (Iringa, Mbeya, Ruvuma, na Rukwa) Katika Mamilioni ya Shilingi kwa Bei za Sasa.**




**JEDWALI XIV: MAPATO YA MKOA NA WASTANI WA MAPATO BINAFSI YA MIKOA MINNE MASHUHURI KWA UZALISHAJI WA ZIADA WA MAHINDI (IRINGA, MBEYA,RUVUMA, NA RUKWA) KATIKA MAMILIONI YA SHILINGI KWA BEI ZA SASA.**

| Mwaka | Iringa | | Mbeya | | Ruvuma | | Rukwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Pato la Mkoa (GDP) | Pato Binafsi* | Pato la Mkoa (GDP) | Pato Binafsi * | Pato la Mkoa (GDP) | Pato Binafsi* | Pato la Mkoa (GDP) | Pato Binafsi * |
| 1985 | 5,801 | 5,204 | 7,904 | 5,911 | 3,329 | 4,691 | 2,751 | 4,534 |
| 1986 | 7,773 | 6,789 | 10,362 | 7,517 | 3,886 | 5,296 | 3,886 | 6,141 |
| 1987 | 11,040 | 9,390 | 8,074 | 5,681 | 9,163 | 12,077 | 6,425 | 9,733 |
| 1988 | 20,515 | 17,010 | 14,542 | 9,874 | 17,210 | 22,023 | 12,103 | 17,457 |
| 1989 | 32,667 | 26,339 | 23,485 | 15,507 | 27,412 | 34,109 | 19,273 | 27,031 |
| 1990 | 35,897 | 28,144 | 32,978 | 21,174 | 18,063 | 21,856 | 24,346 | 33,203 |
| 1991 | 45,663 | 34,812 | 42,243 | 26,374 | 22,909 | 26,654 | 31,721 | 42,067 |
| 1992 | 56,694 | 42,028 | 52,191 | 31,685 | 29,567 | 33,828 | 39933 | 51,495 |
| 1993 | 71,664 | 51,659 | 65,901 | 38,904 | 38,638 | 42,985 | 51,631 | 64,742 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1994 | 92,021 | 64,502 | 84,903 | 48,737 | 48,565 | 52,537 | 66,160 | 80,669 |

Chanzo: Tume ya Mipango: Takwimu Muhimu za Uchumi wa Taifa 1976 - 1994 za Taifa, Toleo la II, Agosti 1995.

* Wastani wa Pato Binafsi sio katika mamilioni ya shilingi.

Pato la Mkoa wa Iringa ni kubwa ukilinganisha na pato la mikoa mingine mitatu katika (Jedwali Na. XIV). Pato la Mkoa wa Iringa lilikua katika kipindi cha miaka kumi kutoka kiwango cha chini cha T.Shs. 5,801 milioni mwaka 1985 hadi T.Shs. 92,021 milioni mwaka 1994. Mkoa wa Mbeya katika kipindi hicho uchumi wake kwa pato la Mkoa ulikuwa kutoka T.Shs. 7,904 milioni mwaka 1985 hadi T.Shs. 84,903 milioni mwaka 1994. Wakati huo huo Mkoa wa Ruvuma uchumi wake kwa pato la Mkoa ulikuwa wa chini sana kupita mikoa mingine maarufu kwa uzalishaji wa ziada kwa zao la mahindi, ukifuatiwa na Mkoa wa Rukwa. Lakini katika mtazamo wa Pato la binafsi mkoa wa Rukwa unaongoza tangu 1990 hadi 1994 kwa kuwa na kiwango cha juu kwa pato la binafsi.


Mkoa wa Rukwa ulikuwa na Pato la binafsi la T.Shs. 33,203 mwaka 1990 ambapo mikoa mingine mitatu ilikuwa kama ifuatavyo:- Iringa Shs. 28,144, Mbeya Shs. 21,174, na Shs. 21,856 Mkoa wa Ruvuma. Sababu kubwa inayosababisha Mkoa wa Rukwa kuwa na pato kubwa la binafsi, ni idadi ndogo ya watu waishio katika mkoa huo. (Sensa ya Idadi ya Watu 1988).

Mkoa wa Ruvuma ulifanikiwa kukuza uchumi wake kwa mfululizo miaka 1987, 1988 na 1989. Hata hivyo kwa ujumla pato la Mkoa wa Ruvuma liko chini sana ikilinganishwa na pato la mikoa mingine mitatu mashuhuri kwa uzalishaji zao la mahindi. Jedwali Na. XIV latoa kielelezo hiki ambapo hapo mwishoni mwa mwaka 1994 pato la Mkoa (GDP) wa Ruvuma lilikuwa T.Shs. 48,565 milioni tu ambapo lile la mkoa wa Iringa

lilikuwa T.Shs. 92,021 milioni, T.Shs. 84,903milioni kwa Mkoa wa Mbeya na T.Shs. 66,160 milioni kwa Mkoa wa Rukwa. Vile vile pato la binafsi (per capita GDP) mkoani Ruvuma lilikuwa chini kulikoa yale ya mikoa ya Rukwa na Iringa. Hakuna sababu dhahiri kabisa iliyoweza kusababisha hali hii duni kwa Mkoa wa Ruvuma. Hata hivyo upo umuhimu wa kufanyika utafiti ili kufahamu juu ya sababu zilizochangia hali hii ukiwemo utumiaji holela wa mbolea za viwandani na kusababisha uharibifu wa virutubisho vya udongo (nutrients), au kupanda sana kwa bei ya mbolea hivyo kuwanyima wakulima wengi uwezo wa kununua mbolea hiyo.

**Kielelezo Na 7: Wastani wa Mapato ya Mkoa, Mikoa Minne Mashuhuri kwa Uzalishaji wa Mahindi (Iringa, Mbeya, Ruvuma, na Rukwa) Katika Mamilioni ya Shilingi kwa Bei Za Sasa.**

**Maelfu**



**Jedwali Na. XV: PATO LA MKOA NA WASTANI WA PATO BINAFSI, MKOA WA IRINGA KWA BEI ZA SASA NA ASILIMIA YA BADILIKO, 1980 -1994**

| Mwaka | Pato la Mkoa kwa Bei za sasa (Mamilioni ya T.Shs.) | Badiliko kwa Asilimia | Wastani wa Pato la Binafsi kwa Bei za sasa shilingi na Dola ya Kimarekani. | | | Badiliko Asilimia | Wastani wa % ya Mchango katika pato la Taifa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Shilingi ya Tanzania | Bei ya Dola kwa Shilingi | Dola za Kimarekani | | |
| 1980 | 1,757 | - | 1,801 | 8.22 | 219 | - | 4 |
| 1981 | 2,300 | 33 | 2,325 | 8.35 | 278 | 27 | 4 |
| 1982 | 2,952 | 27 | 2,868 | 9.52 | 301 | 8 | 5 |
| 1983 | 3,309 | 12 | 3,131 | 12.44 | 252 | - 16 | 5 |
| 1984 | 4,315 | 30 | 3,975 | 18.16 | 219 | - 13 | 5 |
| 1985 | 5,801 | 34 | 5,204 | 16.50 | 315 | 44 | 5 |
| 1986 | 7,773 | 34 | 6,789 | 51.70 | 131 | - 58 | 5 |
| 1987 | 11,040 | 42 | 9,390 | 83.70 | 112 | - 14 | 5 |
| 1988 | 20,515 | 86 | 17,010 | 125.00 | 136 | 21 | 6 |
| 1989 | 32,667 | 59 | 26,339 | 192.00 | 137 | 0.7 | 6 |
| 1900 | 35,897 | 10 | 28,144 | 197.00 | 143 | 4 | 5 |
| 1991 | 45,663 | 27 | 34,812 | 234.00 | 149 | 4 | 5 |
| 1992 | 56,694 | 24 | 42,028 | 335.00 | 125 | - 16 | 5 |
| 1993 | 71,664 | 26 | 52,659 | 480.00 | 108 | - 14 | 5 |
| 1994 | 92,021 | 28 | 64,502 | 553,00 | 117 | 8 | 5 |

Chanzo: 1. Tume ya Mipango, Takwimu za Uchumi za Kitaifa, Tanzania 1976 - 1994, Toleo la 11, Agosti 1995.
2. Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania, 1981 - 1994.

Jedwali Na. XV linaonyesha kwamba kitakwimu kweli kulikuwa na ongezeko la pato binafsi la wakazi wa Mkoa Iringa kutoka T.Shs. 1,801/= mwaka 1980 hadi kufikia T.Shs. 64,502 mwaka 1994; lakini wakati huo huo thamani ya shilingi ilishuka ghafla kwa asilimia 46, yaani kutoka pato la Dola za Kimarekani 219 mwaka 1980 hadi kufikia kiwango cha chini cha Dola 117 mwaka 1994. Hii inamaanisha kwamba wananchi Mkoani Iringa walijikuta wako maskini zaidi 1994 kuliko walivyokuwa 1980. Umaskini wa watu hawa Mkoani Iringa unadhihirishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi kwa dola ya Kimarekani kutoka kwenye badiliko la T.Shs. 8.22 kwa Dola ya Kimarekani mwaka 1980 hadi kiwango cha

badilisho la T.Shs. 553 kwa Dola ya Kimarekani mwaka 1994. Jedwali Na. XV pia linaonyesha kukua kwa kiwango kidogo tu cha Pato la Mkoa kwa bei za sasa katika kipindi cha miaka minane, kati ya 1980 na 1988. Ilipofika mwaka 1988 kiwango cha kutosha cha ongezeko la pato na ulifikia pato la T.Shs. 20,151 milioni kwa mkoa na likaendelea kukua hadi 1994. Mkoa ulichangia kwa asilimia 5.53 kati ya mwaka 1980 hadi 1994, kwenye pato la Taifa kama mchango wa uchumi ikilinganishwa na asilimia 6 kwa mkoa wa Mbeya, asilimia 7.80 mkoa wa Arusha na asilimia 7.67 mkoa wa Mwanza (Jedwali Na. XVI). Hata hivyo mkoa wa Iringa ni wa sita katika umuhimu wa kuchangia katika Pato la Taifa.

**Jedwali Na. XVI: WASTANI WA MWAKA WA UCHANGIAJI WA PATO LA MKOA KATIKA PATO LA TAIFA (1980 - 1994)**

| Mkoa | Wastani wa Asilimia wa mchango wa Pato la Mkoa (GDP) katika Pato la Taifa. | Nafsi ya uchangiaji kwa Pato la Taifa |
|---|---|---|
| Dar es Salaam | 20.33 | 1 |
| Arusha | 7.80 | 2 |
| Mwanza | 7.67 | 3 |
| Mbeya | 6.00 | 4 |
| Shinyanga | 5.80 | 5 |
| **Iringa** | **5.53** | **6** |
| Tanga | 5.52 | 7 |
| Morogoro | 4.67 | 8 |
| Kagera | 4.60 | 9 |
| Kilimanjaro | 3.67 | 10 |
| Mara | 3.47 | 11 |
| Tabora | 3.40 | 12 |
| Ruvuma | 3.33 | 13 |
| Mtwara | 3.27 | 14 |
| Rukwa | 3.13 | 15 |
| Dodoma | 3.07 | 16 |
| Singida | 2.87 | 17 |
| Kigoma | 2.53 | 18 |
| Lindi | 2.00 | 19 |

| | | |
|---|---|---|
| Pwani | 1.00 | 20 |
| Jumla | 100.00 | |

Chanzo: Tume ya Mipango, Takwimu za uchumi za Taifa, Tanzania 1976 - 1994. Toleo la II, Agosti 1995.

## 2.3 Sekta za Uzalishaji:

Sekta hizi ni: Kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, ufugaji nyuki, uchimbaji madini na viwanda.

### 2.3.1 Kilimo:


Ardhi ndiyo rasilimali kuu ya Mkoa wa Iringa ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 58,936. Kilometa za mraba 41,945 zinafaa kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Kwa sasa ni kilometa za mraba 4,644 tu ndizo zinatumika kwa kilimo, hii ni sawa na asilimia 11.1 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo Mkoani. Kwa mfano wilaya ya Mfindi inatumia asilimia 19.68 tu ya ardhi yake inayofaa kwa kilimo, na wilaya za Njombe na Iringa zinatumia asilimia 14.82 na 7.26 kwa kufuatana. Hii ina maana kwamba sehemu kubwa sana ya eneo la mkoa linalofaa kwa kilimo halijaendelezwa bado. Shughuli nyingi za kilimo zingweza kuendeshwa mkoani iwapo kilimo cha umwagiliaji kingeendelezwa. Jedwali Na. XVII lifuatalo linaonyesha maeneo yanayofaa kwa kilimo kiwilaya:

Maji ya mito na ziwa yangeweza kutumika kwa kilimo hiki cha umwagiliaji kuliko kutegemea kilimo cha mvua peke yake.

Kilimo ndiyo shughuli kuu ya uchumi kwa wananchi wengi mkoani Iringa. Sekta hii pekee inachangia asilimia 85 ya pato la mkoa kwa mwaka na kutoa ajira kwa asilimia 90 ya wakazi mkoani humo. Ingawaje kilimo kinatoa ajira kubwa namna hiyo hata hivyo uzalishaji wa mazao bado ni duni. Mambo yanayochangia kwa uzalishaji huu mdogo ni utumiaji wa zana

duni za kilimo, utumiaji wa njia za kilimo zilizokwisha pitwa na wakati, wadudu na magonjwa ya mimea, uchakavu wa ardhi na kupungua kwa rutuba ya udongo (k.m. Tarafa za Isimani na Pawaga); kukosekana kwa pembejeo za kilimo (mbolea, madawa ya mimea n.k), aidha uwezo mdogo wa wakulima kifedha una sababisha wakulima kutumia zana duni za kilimo.

**Kielelezo Na. 8: Eneo linalofaa kwa kilimo kiwilaya, Mkoa wa ringa**




**JEDWALI XVII: MAENEO YANAYOFAA KWA KILIMO, KIWILAYA, MKOA WA IRINGA.**

| Wilaya | Ukubwa wa Eneo (Ardhi) (km$^2$) | Eneo linalofaa kwa kilimo (km$^2$) | Eneo linalotumika kwa Kilimo (km$^2$) | Asilimia ya Eneo litumikalo kwa Kilimo (km$^2$) |
|---|---|---|---|---|
| Iringa | 28,620 | 16,607.85 | 1,206.12 | 7.26 |
| Mufindi | 7,123 | 6,765.9 | 1,331.45 | 19,68 |
| Njombe | 10,668 | 9,728.75 | 1,441.79 | 14.82 |
| Ludewa | 8,397 | 4,650.30 | 344.44 | 9.46 |
| Makete | 4,128 | 4,195.00 | 320.37 | 7.64 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jumla | 58,936 | 41.948 | 4,644.17 | 11.10 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa: Mikakati ya Kuongeza kipato wananchi wa Mkoa wa Iringa, 1996.

Jedwali Na. XVII linadhihirisha kwamba asilimia 11.10 tu ya ardhi inayofaa kwa kilimo inatumika. Wilaya ya Iringa ambayo inaeneo linalofaa kwa kilimo kubwa zaidi kuliko wilaya nyingine mkoani Iringa, inatumia asilimia 7.2 tu. Je?, inamaanisha kwamba wananchi Mkoani Iringa hawajaitikia vyema sera ya Mikoa Minne Maarufu kwa kilimo cha mahindi? Wangekuwa wameitikia vyema hali ingedhihirisha kwa uzalishaji mkubwa kwa kila hekta na pia maeneo makubwa zaidi yangekuwa yanalimwa.

a) **Mazao ya chakula na Biashara:**

Kiwango cha uzalishaji kwa kila eneo ni kidogo sana. Jedwali Na. XVII linafafanua zaidi juu ya hali hii. Uzalishaji wa mahindi kwa hekta ni mdogo sana, kwa mfano mwaka 1996 wastani wa tani 2 tu zilizalishwa kwa kila hekta ikilinganishwa na uwezo wa kuzalisha tani 6.5/ha. Baada ya Mkoa huu kutangazwa kuwa ni mmoja wa mikoa minne maarufu inayozalisha mahindi, na kupatiwa misaada muhimu mbalimbali na Serikali ya Mkoa na Serikali Kuu ilitarajiwa uzalishajii ungekuwa umepanda kwa kiwango kikubwa.

Ni vyema sababu zikajulikana zinazokwamisha uzalishaji bora wa mazao na hasa mahindi, kwani hata nusu ya tani 6.5/ha haijafikiwa, kiwango ambacho kinaweza kabisa kupatikana mkoani humo.

**Jedwali Na. XVIII: UZALISHAJI WA MAZAO TANI/HEKTA, MKOANI IRINGA, 1996.**


| Aina ya Zao | Uzalishaji (Tani/Ha) | Kiwango cha Uzalishaji kinachoweza kupatikana (Tani/Ha) | Kiwango ambacho hakijafikiwa (Tani/Ha) |
|---|---|---|---|
| Mahindi | 2.0 | 6.5 | 4.5 |
| Maharage | 0.6 | 1.3 | 0.9 |
| Mtama | 1.5 | | |
| Mpunga | 2.0 | 4.5 | 2.5 |
| Ngano | 1.2 | 3.0 | 1.8 |
| Vitunguu | 7.0 | 15.0 | 8.0 |
| Nyanya | 30.0 | 80.0 | 50.0 |
| Cabbage | 40.0 | 60.0 | 20.0 |
| Viazi Mviringo | 8.0 | 15.0 | 7.0 |
| Tumbaku | 0.7 | 1.5 | 0.8 |
| Kahawa | 0.35 | 1.5 | 1.25 |
| Pareto | 1.2 | 2.5 | 1.3 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa:
Mikakati ya kuwaongezea kipato wananchi wa Mkoa wa iringa - Rasimu, 1996.

i) **Mazao ya Chakula**:

Mahindi ni zao muhimu kwa chakula na biashara mkoani Iringa. Zao hili linaweza kuzalishwa sehemu zote za mkoa ingawaje yapo maeneo mengine yanayozalisha zaidi kuliko mengine kutokana na hali nzuri ya hewa kwa uzalishaji wa zao hili. Yapo vile vile mazao mengine yanayolimwa mkoani ingawaje ni kwa kiwango kidogo. Mazao haya ni pamoja na: mpunga na mtama. Eneo maarufu kwa kilimo cha mpunga ni bonde la mto Ruaha, wilaya ya Iringa; Sadani katika wilaya ya Mufindi na Upangwa sehemu ya kusini ya wilaya ya Njombe. Maeneo yanayolima mpunga kwa kiwango kidogo ni eneo la chini Mufindi, eneo la chini Ubena na eneo la Wanging'ombe. Maeneo yanayolima mtama yametawanyika mkoani na hustawi vizuri katika maeneo yote yenyemvua chache mkoani.

**Kielelezo Na. 9: Uzalishaji wa Mazao Muhimu ya Chakula Muhimu, Mkoani Iringa (Tani), 1987/88 - 1994/95**




**Jedwali Na.XIX: UZALISHAJI WA MAZAO MUHIMU YA CHAKULA, MKOANI IRINGA (TANI), 1987/88 - 1994/95**

| **Zao** | **Msimu wa Kilimo** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **1987/8** | **1988/8** | **1989/9** | **1990/9** | **1991/9** | **1992/9** | **1993/9** | **1994/95** |
| Mahindi | - | 515,50 | 482,13 | 404,79 | 438,69 | 453,44 | 247,61 | 461,394 |
| Mtama | 16,970 | 5,428 | 24,612 | 6,657 | 6,800 | 23,720 | 17,541 | 38,086 |
| Mpunga | 1,905 | 3,393 | 2,426 | 3,241 | 2,827 | 5,710 | 3,057 | 9,797 |
| Ngano | 23,414 | 15,193 | 13,062 | 15,349 | 28,735 | 20,911 | 11,962 | 14,223 |
| Maharage | 21,121 | 24,681 | 44,805 | 35,964 | 35,659 | 49,401 | 20,792 | 41,018 |
| Muhogo | 4,260 | 860 | 3,932 | 5,403 | 23,455 | 29,836 | 9,897 | 19,249 |
| Viazi Mviringo | 26,183 | 116,14 | 178,55 | 161,59 | 227,53 | 134,09 | 122,36 | 170,903 |
| Viazi Vitamu | 26,183 | 25,810 | 13,075 | 2,640 | - | 20,870 | 69,085 | 43,959 |
| Karanga | 2,211 | - | 480 | 818 | 2,212 | 2,845 | 1,139 | 1,139 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Njungu | - | - | - | 1,211 | 2,272 | 2,175 | 1,779 | 3,218 |
| Matunda | - | - | 3,360 | - | 3,056 | 3,056 | 1,171 | 1,172 |
| Kabegi | - | - | 3,875 | - | 2,016 | 7,425 | 6,593 | 852 |
| Nyanya | - | - | 3,875 | - | 5,592 | - | - | - |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Afisa Kilimo na Mifugo, 1996.

Mazao ya nafaka huzalishwa zaidi na wakulima wadogo. Zao la mpunga hulimwa peke yake bila kuchanganywa na mazao mengine. Kilimo cha mpunga ni cha namna mbili Mkoani, cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji, na hulimwa Sadani, eneo la chini la Mufindi na katika bonde la mto Ruaha. Ina ya pili ni kilimo cha mpunga cha kutegemea mafuriko ya mvua kwenye mabonde. Shughuli zote za kilimo cha mpunga hufanywa kwa mkono.

Mtama hulimwa kwa mchanganyiko na mazao mengine ya nafaka na maharage. Hakuna takwimu zakuaminika juu ya ukubwa wa maeneo na kiwango cha uzalishaji wa matunda na mboga Mkoani Iringa. Kilimo cha mboga hufanyika wakati wa masika na wakulima wadogo wadogo, zao muhimu likiwa ni kabeji, ambalo limechukua nafasi ya mboga ya kienyeji ijulikanayo kama "delega". Kitaifa Mkoa wa Iringa huzalisha kwa kiwango kidogo sana cha zao la ngano. Wilaya ya Njombe huzalisha kwa wingi ngano mkoani. Kilimo cha ngano kimeathirika vibaya na ongezeko kubwa la bei ya pembejeo za kilimo kama ilivyo kwa uzalishaji wa zao la mahindi.


**JEDWALI Na. XX: UKUAJI WA UZALISHAJI KWA MAZAO MUHIMU YA CHAKULA.**

| Zao | 1988/89 hadi 1990/91 | 1993/94 hadi 1994/95 |
|---|---:|---:|
| Mahindi | - 0.11 | 0.86 |
| Mtama | 1.40 | 1.17 |
| Mpunga | - 0.10 | 2.20 |
| Ngano | 0.03 | 0.19 |
| Maharage | 0.61 | 0.97 |
| Muhogo | 3.20 | 0.94 |


Chanzo: Tume ya Mipango: Mkusanyo wa Takwimu kutoka Afisa kilimo na Mifugo wa Mkoa wa iringa, 1996.

Jedwali Na. XX linaonyesha kukua na kushuka kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao ya chakula kati ya misimu ya kilimo ya 1988/89 hadi 1994/95. Uzalishaji wa Mazao ya chakula mahindi na mpunga ulishuka kati ya misimu ya 1988/89 na 1990/91, lakini ukaongezeka kwa kiwango cha 0.86 na 2.20 kati ya misimu ya 1993/94 hadi 1994/95. Ni mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama na muhogo yaliyonyesha takwimu za kukua katika kipindi hivyo. Vile vile maharage na ngano yalionyesha dalili ya kuongezeka ingawaje kwa kiwango kidogo.

**Kielelezo Na. 10a: Uzalishaji wa mahindi (tani), Kiwilaya, Mkoa wa Iringa**




**Kielelezo Na. 10b: Uzalishaji wa ngano (tani), Kiwilaya, Mkoa wa Iringa**




**JEDWALI Na. XXI: MAZAO MUHIMU YALIYOZALISHWA (TANI) KIWILAYA, MKOA WA IRINGA, 1994/95**

| Zao | Wilaya | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Iringa (tani)** | **Mufindi (tani)** | **Njombe (tani)** | **Ludewa (tani)** | **Makete (tani)** | **Jumla (tani)** |
| Mahindi | 159,823 | 74,482 | 159,352 | 43,320 | 24,516 | 461,394 |
| Mtama | 35,323 | 74 | 1,899 | 219 | 571 | 38,086 |
| Ngano | 5,898 | 1,101 | 3,494 | 254 | 3,476 | 14,223 |
| Mpunga | 9,147 | - | - | 144 | 506 | 9,797 |
| Maharage | 9,121 | 12,543 | 15,910 | 1,630 | 1,814 | 41,018 |
| Muhogo | 1,521 | 5.214 | - | 12,514 | - | 19,249 |
| Viazi Mviringo | 37,674 | 18,702 | 89,402 | 640 | 23,985 | 170,903 |
| Viazi Vitamu | 11,050 | 13,041 | 19,045 | 120 | 697 | 43,959 |
| Njugu/karanga | 440 | 309 | 390 | - | - | 1,139 |
| Jumla | 269,997 | 125,466 | 289,492 | 58,741 | 55,565 | 799,768 |


Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa: Afisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo Mkoa, Iringa, 1996.

Jedwali XXI linaonyesha kwamba katika msimu wa kilimo wa 1994/95 wilaya ya Iringa iliongoza katika uzalishaji wa mahindi na kufuatiwa na wilaya ya Njombe kwa upungufu wa asilimia 0.3 tu ya kiwango kilichozalishwa na wilaya ya Iringa. Wilaya


ya Makete ilizalisha tani 24,516 tu za mahindi ikilinganishwa na tani 159,823 zilizozalishwa na wilaya ya Iringa na tani 159,352 wilaya ya Njombe.  Taarifa zaidi toka jedwali hilo ni kwamba wilaya ya Iringa ni maarufu pia kwa uzalishaji wa mazao ya mahindi, mtama, ngano na muhogo, aidha wilaya za Mufindi na Njombe ni maarufu kwa kilimo cha maharage.  Wilaya ya Njombe inaongoza katika kilimo cha viazi mviringo.  Kwa msimu wa kilimo wa 1994/95 tani 89,402 za viazi mviringo zilizalishwa ikilinganishwa na tani 18,702; 37,674; 649 zilizozalishwa na wilaya ya Mufindi, 37,674 na Iringa (Vijijini), tani 649 Ludewa na tani 23,985 wilaya ya Makete.  Uzalishaji mkubwa wa zao la zaidi katika wilaya ya Ludewa inatokana na hali ya kijiografia na hewa ambayo ni ya joto kubwa na mvua kidogo.

Juhudi zilizokwisha fanywa na uongozi wa Mkoa wa kuweka malengo ya uzalishaji wa zao la mahindi zinadhihirisha umuhimu wa zao hili mkoani humo likiwa zao la chakula na biashara.  Jedwali Na. XXII linaonyesha malengo ya uzalishaji kati ya msimu wa kilimo kwa mwaka 1988/89 na 1994/95.


**Kielelezo Na. 10c: Uzalishaji wa Maharage (tani), Kiwilaya, Mkoa wa Iringa**



**Kielelezo Na. 10d: Uzalishaji wa viazi mviringo (tani), Kiwilaya, Mkoa wa Iringa**




**Kielelezo Na. 11: Maelengo ya uzalishaji wa mahindi, Mkoa wa Iringa 1988/89 - 1994/95**




**JEDWWALI Na. XXII: MALENGO YA UZALISHAJI WA MAHINDI MKOA WA IRINGA 1988/89 - 1994/95**

| Msimu | Malengo ya Uzalishaji | Kilichozalishwa |
|---|---|---|

| Muda | Hekta | Tani | Hekta | Tani |
|---|---|---|---|---|
| 1988/89 | 519,139 | 580,799 | 281,555 | 515,508 |
| 1989/90 | 316,736 | 593,620 | 257,986 | 482,131 |
| 1990/91 | 310,113 | 543,857 | 273,482 | 404,799 |
| 1991/92 | 321,543 | 574,026 | 261,354 | 438,693 |
| 1992/93 | 325,328 | 835,190 | 277,968 | 453,448 |
| 1993/94 | 326,155 | 560,817 | 221,039 | 247,613 |
| 1994/95 | 304,975 | 509,500 | 275,917 | 461,394 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Afisa Kilimo na Mifugo, Mkoa wa Iringa, 1996.

Jedwali XXII linadhihirisha kwamba katika kipindi chote cha miaka saba (1988/89 - 1994/95) viwango vilivyofikiwa vya uzalishaji viliendelea kuwa chini ya malengo yaliyowekwa. Kwa mfano msimu wa 1988/89 uzalishaji ulikuwa chini kwa silimia 46 ya malengo ya hekta zilizopashwa kulimwa na asilimia 11 ya malengo ya mavuno. Katika msimu wa 1992/93 uzalishaji ulishuka kwa asilimia 14 ya lengo la hekta ambazo zingelimwa na kwa asilimia 46 ya lengo la uzalishaji. Msimu wa 1994/95 uzalishaji ulishuka kwa asilimia 10 ya lengo la hekta za kulimwa na asilimia 9 ya lengo la tani ambazo zingezalishwa. Mwelekeo huu wa maendeleo ya kilimo unaleta wasiwasi juu ya usahihi wa sera ya Mikoa minne Maarufu kwa kilimo cha mahindi na ufanisi wa mradi wa Sasakawa Global 2000 katika mkoa Iringa. Ilitarajiwa kungekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa mahindi kutokana na sera ya kilimo cha mahindi Mkoani na mradi wa Sasakawa Global 2000.

ii) **Mazao ya Biashara**:

Mazao makuu ya biashara kwa Mkoa wa iringa ni: Chai, tumbaku, pareto, alizeti na kahawa.


Jedwali XXIV linaonyesha viwango vya uzalishaji wa kila zao hilo la biashara kiwilaya kwa msimu wa kilimo wa 1994/95.

**Jedwali Na XXIII: MALENGO YA UZALISHAJI WA MAHINDI KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1998/89 - 1994/95**


| Wilaya | 1991/92 | | 1992/93 | | 1993/94 | | 1994/95 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Malengo (ton) | Kilichozalishwa (ton) | Malengo (ton) | Kilichozalishwa (ton) | Malengo (ton) | Kilichozalishwa (ton) | Malengo (ton) | Kilichozalishwa (ton) |
| Iringa | 154,490 | 85,000 | 186,220 | 144,607 | 201,756 | 80,702 | 180,190 | 159,823 |
| Mufindi | 141,325 | 132,307 | 96,352 | 75,202 | 97,508 | 28,451 | 84,450 | 74,482 |
| Njombe | 191,447 | 139,394 | 171,880 | 166,185 | 172,000 | 94,600 | 174,490 | 159,352 |
| Ludewa | 58,190 | 58,000 | 50800 | 44,882 | 59,000 | 30,119 | 59,000 | 43,220 |
| Makete | 28,574 | 23,992 | 29,938 | 22,572 | 30,535 | 13,741 | 28,510 | 24,516 |
| **Jumla** | **574,026** | **438,693** | **835,190** | **453,448** | **560,817** | **247,613** | **509,500** | **461,394** |

Chanzo: Ofisi ya Kilimo Mkoa wa Iringa, 1996

**Kielelezo Na. 12a: Uzalishaji wa zao la Kahawa Kiwilaya Mkoa wa Iringa, 1994/95**




**Kielelezo Na. 12b: Uzalishaji wa zao la Pareto Kiwilaya Mkoa wa Iringa, 1994/95**




**Jedwali Na. XXIV: MAZAO MAKUU YA BIASHARA YANAYOZALISHWA KIWILAYA MKOA WA IRINGA, 1994/95**

| Wilaya | Chai (Tani) | Kahawa (Tani) | Pareto (Tani) | Alizeti (Tani) | Tumbaku (Tani) | Pamba (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Iringa | - | 11 | 9 | 12,286 | 768 | 242 |
| Mufindi | 9,520 | 3 | 17 | 2,147 | 4 | - |
| Njombe | 1,522 | 36 | 60 | 6,400 | 2 | - |
| Ludewa | - | 95 | 8 | 34 | 15 | - |
| Makete | - | 3 | 340 | - | - | - |
| Jumla | 11,042 | 148 | 434 | 20,867 | 789 | 242 |

Chanzo: Afisa kilimo na Mifugo, Mkoa wa Iringa 1996.

Kulingana na Jedwali Na. XXIV msimu wa kilimo katika mwaka 1994/95, wilaya ya Iringa Vijijini ilizalisha zaidi ya tani 12,286 za alizeti na tumbaku tani 768. Wilaya iliongoza kwa uzalishaji wa mazao haya mawili. Wilaya ya Mufindi nayo iliongoza katika uzalishaji wa chai kwa tani 9,520. Wilaya ya Makete iliongoza katika kuzalisha pareto kwa kiwango cha tani 340, wilaya ya Ludewa iliongoza kwa kuvuna tani 95 za kahawa. Wilaya ya Njombe haikuongoza katika uzalishaji wa zao lolote kati ya mazao sita yaliyoorodheshwa kwenye jedwali pamoja na kwamba inayo hali nzuri ya hewa. Wilaya ya Njombe iliweza kuzalisha tani 1,522 za chai, tani 36 za kahawa, tani 60 za pareto na tani 6,400 za alizeti.

**JEDWALI Na. XXV: IDADI YA HEKTA ZILIZOLIMWA NA KIWANGO CHA MAZAO YA BIASHARA YALIYOVUNWA MISIMU YA KILIMO 1990/91 - 1994/95:**

| Zao | 1990/91 | | 1991/92 | | 1992/93 | | 1993/94 | | 1994/95 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Eneo (Ha) | Mavuno (Tani) | Eneo (Ha) | Mavuno (Ha) | Eneo (Ha) | Mavuno (Tani) | Eneo (Ha) | Mavuno (Tani) | Eneo (Ha) | Mavuno (Tani) |
| Chai | 6,425 | 9,119 | 6,311 | 10,459 | 6,295 | 10,440 | 5,865 | 11,042 | 5,951 | 11,020 |
| Kahawa | 3,998 | 325 | 6,304 | 243 | 6,300 | 136 | 4,817 | 146 | 4,817 | 148.5 |
| Tumbaku | 1,410 | 1,038 | 1,699 | 1,462 | 1,566 | 1,156 | 1,356 | 1,277 | 1,356 | 789.7 |
| Alizeti | 4,480 | 6,385 | 16,520 | 13,418 | 22,309 | 19,597 | 18,872 | 9,792 | 23,924 | 20,867 |
| Pareto | 4,554 | 802 | 3,451 | 1,291 | 2,897 | 406 | 2,439 | 471 | 818 | 434.9 |
| Pamba | - | - | 620 | 280 | 93 | 7 | 22 | 10 | 322 | 241.8 |
| Jumla | 20,867 | 18,119 | 34,905 | 27,153 | 39,460 | 31,742 | 33,371 | 22,592 | 37,188 | 33,501 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, Idara ya Kilimo na Mifugo.

Jambo muhimu linalojitokeza katika jedwali XXV ni kuendelea kupunguka kwa hekta za mazao ya chai na pareto misimu ya 1990/91 - 1994/95. Kwa zao la alizeti hekta zimekuwa zikiongezeka isipokuwa msimu wa 1993/94. Kwa mfano jumla ya hekta 4,480 za alizeti zilipandwa 1990/91 na hekta 23,924 za zao hilo msimu 1994/95.

Maeneo yaliyokuwa chini ya zao la kahawa yalibadilika badilika kutoka hekta 3,998 msimu 1990/91 hadi hekta 6,300 msimu 1992/93 na hekta 4,817 msimu 1994/95, sawa kwa zao la tumbaku. Jedwali Na. XXVI linaelezea vizuri zaidi mwelekeo huu wa uzalishaji.

**Jedwali Na. XXVI: UKUAJI WA UZALISHAJI KWA MAZAO MACHACHE YA BIASHARA MKOANI IRINGA MISIMU 1990/91 - 1994/95.**

| Zao | 1990/91 - 1992/93 | 1993/94 - 1994/95 |
|---|---|---|
| Chai | - 0.016 | - 0.002 |
| Kahawa | - 0.095 | 0.01 |
| Tumbaku | 0.1 | - 0.38 |
| Alizeti | 0.71 | 1.13 |

| | | |
|---|---|---|
| Pareto | - 0.035 | - 0.08 |

Chanzo: Takwimu, Tume ya Mipango.

Inadhihirika kutoka Jedwali Na. XXVI kwamba kati ya msimu 1990/91 na 1992/93 mazao ya tumbaku na alizeti pekee yalipata ongezeko katika uzalishaji ingawaje kwa viwango vidogo tu. Uzalishaji wa zao la kahawa ulipungua sana kati ya misimu ya 1990/91 hadi 1992/93. Mwelekeo ulikuwa kama huo wa kushuka kwa mazao ya pareto na chai kwa misimu hiyo. Kulikuwepo na ukuaji mdogo wa zao la kahawa kati ya misimu 1993/94 na 1994/95 kutoka - 0.095 hadi 0.01. Uzalishaji wa tumbaku nao ulishuka kati ya mismu 1993/94 na 1994/95 kutoka 0.1 hadi - 0.38. Hata hivyo kulikuwa na ukuaji wa uzalishaji wa zao la alizeti kati ya 1993/94 - 1994/95 kutoka 0.71 (1990/91) hadi 1.13 (1993/94 - 1994/95).

b) **Pembejeo za Kilimo**:

Utumiaji wa pembejeo hasa mbolea umekuwa ukiendelea kushuka kutokana na upandaji wa haraka wa bei za pembejeo. Jedwali Na. XXVII linaonyesha aina ya mbolea, kiwango kilichotumika, upatikanaji wake na uwezo wa kuwafikia wakulima. Jedwali linaonyesha wazi kwamba mahitaji ya mbolea ya kupandia aina ya TSP yalikuwa tani 21,300 Mkoani Iringa katika msimu wa 1993/94, hata hivyo kiasi kilichoweza kupatikana ni tani 1,759.5 tu, na kiasi cha tani 1,530.8 ndicho kilichowafikia wakulima. Kwa maneno mengine, mahitaji yalikuwa makubwa kuliko upatikanaji wake kwa kiwango cha tani 19,769.2. Aidha mahitaji ya mbolea ya kukuzia aina ya CAN msimu wa kilimo 1993/94 yalikuwa tani 28,835 kwa mkoa mzima hata hivyo ni kiasi cha tani 7,941.1 tu ndizo zilizopatikana na kati ya hizi ni tani 6,752.7 tu ndizo ziliweza kuwafikia wakulima. Kama ilivyokuwa kwa TSP na CAN

mahitaji ya mbolea ya UREA yalikuwa tani 6,680 lakini ni tani 4,480.95 tu zilipatikana, na tani 4,161 zilisambazwa kwa wakulima. Hali hii iliendelea katika msimu wa 1994/95 kwa mahitaji, upatikanaji na usambazaji wa mbolea. Kwa ujumla tani 20,180.25 za mbolea ya aina zote ilisambazwa kwa wakulima kwa msimu wa 1993/94 dhidi ya mahitaji ya tani 63,206. Tani 29,235 zilisambazwa 1994/95 ukilinganisha na mahitaji ya tani 63,206. Iwapo hali halisi ya upatikanaji na usambazaji wa mbolea kwa wakulima ni huu basi ni dhahiri umaarufu wa mikoa minne ya uzalishaji wa mahindi hautakuwepo. Pia wakulima watakatishwa tamaa pia mategemo yao kwa ufanisi wa Sasakawa Global 2000. Kumekuwepo pia na upungufu wa mbegu bora zilizoweza kuwafikia wakulima ikilinganishwa na mahitaji halisi ya pembejeo hiyo. Hali kadhalika kwa mahitaji ya madawa ya mimea. Angalia Jedwali Na. XXIX.

**JEDWALI Na. XXVII: AINA YA MBOLEA ILIYOHITAJIKA, ILIYOPATIKANA NA KUZAMBAZWA MKOA WA IRINGA MISIMU YA KILIMO 1993/94 NA 1994/95.**

| Mwaka | Aina ya Mbolea | Mahitaji (Tani) | Iliyopatikana (Tani) | Iliyosambwazwa (Tani) |
|---|---|---|---|---|
| 1993/94 | TSP | 21,300 | 1,759.5 | 1,530.8 |
| | DAP | - | 1,418 | 1,354.25 |
| | SSP | - | 1,103.7 | 83.15 |
| | SOP/MOP | 23 | 21 | - |
| | CAN | 28,835 | 7,954.1 | 6,752.7 |
| | SA | 853 | 5,164.2 | 5,153.1 |
| | UREA | 6,680 | 4,480.95 | 4,146.1 |
| | AN | - | - | - |
| | NPK | 5,485 | 1,350.1 | 1,160.15 |
| | MRP | - | - | - |
| Jumla | | 63,206 | 23,351.55 | 20,180.25 |
| 1994/95 | TSP | 21,300 | 2,179.4 | 1,878.4 |
| | DAP | - | 1,257.0 | 1,196.3 |
| | SOP/MOP | - | 110.1 | 110 |
| | CAN | 23 | 17 | - |
| | SA | 28,835 | 21,765.2 | 14,661.2 |
| | UREA | 853 | 2,064.05 | 930.6 |
| | AN | 6,680 | 10,525.35 | 6,775 |
| | NPK | - | 645.05 | 184.63 |
| | MRP | 5,485 | 5,145.4 | 3.133.8 |
| Jumla | | 63,206 | 43,948.65 | 29,235.1 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, Idara ya Mipango, 1995.

**JEDWALI Na. XXVIII: MAHITAJI, UPATIKANAJI NA USAMBAZAJI WA MBEGU BORA MKOANI IRINGA KWA MISIMU YA KILIMO 1993/94 NA 1994/95.**

| Mwaka | Aina ya Mbegu Bora | Mahitaji (Tani) | Upatikanaji (Tani) | Usambazaji (Tani) |
|---|---|---|---|---|
| 1993/94 | UCA | 142 | 15.1 | 9.1 |
| | H.632 | 74 | 47.2 | 22.3 |
| | H.614 | 307 | 65.8 | 24.7 |
| | H.6302 | 583 | 168.1 | 31.1 |
| | CG | 40 | 2.17 | 0.19 |
| | TMV II | 40 | 43 | 15 |
| | KITO/KILIMA | 96 | - | - |
| | MTAMA | 105 | 50.53 | 20.53 |
| | ALIZETI | 86 | 3.09 | 3.06 |
| | MAHARAGE | 124 | 1.8 | 1.2 |
| | KAHAWA | 2.5 | 2.5 | 2.5 |
| | PAMBA | 5 | 5 | 5 |
| Jumla | | 1604.5 | 404.3 | 138.4 |
| | UCA | 142 | 22.87 | 22.18 |
| | H 632 | 74 | 13.21 | 6.66 |
| | H 614 | 307 | 272.22 | 49.12 |
| | H 6302 | 585 | 152 | 73.52 |
| | CG | 40 | 18.3 | 3.3 |
| | TMV II | 75 | - | - |
| | KITO/KILIMA | 40 | 2.1 | 2.1 |
| | MTAMA | 105 | 42.2 | 42.2 |
| | ALIZETI | 86 | 2.84 | 0.87 |
| | MAHARAGE | 124 | 1.34 | 1.2 |
| | KAHAWA | 2.5 | 2.5 | 2.5 |
| | PAMBA | 5.5 | 5.5 | 5.5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jumla | | 1,604.5 | 535.1 | 208.96 |

Chanzo: Afisa Kilimo na Mifugo, Mkoa wa Iringa 1994/95.

**JEDWWALI Na. XXIX: AINA YA MADAWA YA MIMEA YALIYOHITAJIKA, YALIYOPATIKANA NA KUSAMBAZWA MKOANI IRINGA MISIMU YA KILIMO 1993/94 NA 1994/95.**

| Mwaka | Aina ya Madawa | Mahitaji (Kg/Lit.) | Iliyopatikana (Kg/Lit.) | Iliyosambazwa (Kg/Lit.) |
|---|---|---|---|---|
| 1993/94 | Sumithion 50 EC (Lts) | 362 | 126 | 62 |
| | Actellic Super dust (Tons) | 7.02 | 6.12 | 4.47 |
| | Actellic 50 EC (Lts) | 670 | 506 | 404 |
| | Thiodan 35 EC (Lts) | 1200 | 752 | 596 |
| 1994/95 | Sumithion 50 EC (Lts) | 160 | 725 | 525 |
| | Actellic Super dust (tons) | 10.6 | 6 | 3.29 |
| | Actellic 50 EC (Lts) | 1500 | 375 | 285 |
| | Thiodan 35 EC (Lts) | 807 | 425 | 304 |

Chanzo: Afisa Kilimo na Mifugo Mkoa, Iringa, 1994/95.

Ni dhahiri kwamba bila matumizi ya pembejeo za kilimo hakuna njia yeyote ile ya kumwezesha mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake. Kwa kuwa wakulima wa Mkoa huu wamekuwa wakitumia pembejeo za kilimo (mbolea za viwanda) ni kwa miaka mingi hawana budi kuendelea kufanya hivyo tena kwa kiwango kikubwa zaidi kupata mavuno yakuridhisha. Hii inatokana na ufahamu kwamba jinsi mbolea nyingi inavyoendelea kutumika katika kilimo na ndivyo virutubisho vingi ndani ya udongo vinavyochujuka na mvua kutoka kwenye udongo, na hivyo hulazimisha matumizi ya mbolea zaidi na zaidi ili kupata mavuno mazuri; hatimaye mzunguko huu unakuwa wa kudumu.

(c). **Zana za Kilimo:**

Jembe la mkono limeendelea kuwa zana kuu kwa wakulima wengi mkoani, kwani ni wachache tu walionauwezo wa kuwa na jembe la kukokotwa na ng'ombe au trekta. Kwa hivyo matumizi ya zana hizi za kisasa za kilimo si ya kawaida kwa wengi mkoani. Jedwali Na. XXX linaonyesha aina ya zana za kisasa za kilimo zitumikazo Mkoani Iringa na wilaya zake.

**JEDWALI XXX: ZANA ZA KILIMO ZA KISASA ZILIZOPO MKOANI IRINGA, KIWILAYA MSIMU WA KILIMO 1994/95.**

| Wilaya | Idadi ya Trakta | Idadi ya Plau | Idadi ya Haro | Idadi ya Planta | Idadi ya Cultivator | Idadi ya Harvester |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Iringa | 580 | 9,050 | 100 | 231 | 165 | 1 |
| Mufindi | 81 | 6,570 | 65 | 14 | 136 | 5 |
| Njombe | 80 | 10,042 | 75 | 6 | 164 | 2 |
| Ludewa | 36 | 6,365 | 36 | 3 | 109 | - |
| Makete | 20 | 114 | 9 | - | 6 | - |
| Jumla | 727 | 32,141 | 285 | 259 | 580 | 8 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Kilimo na Mifugo, Iringa.

Kwa kuchunguza Jedwali Na. XXX inadhihirika kwamba wilaya ya Njombe ina idadi ya plau nyingi zaidi ikifuatiwa na wilaya ya Iringa. Wilaya ya Makete ina idadi ndogo sana ya plau, hali hii inaweza kusababishwa na hali ya milima mingi na aina ya udongo kutofaa kwa matumizi ya zana hiyo. Kuna idadi ndogo tu ya trakta Mkoani karibu asilimia 73 ya trakta zote Mkoani zipo wilayani Iringa. Wilaya ya Makete ikiwa na idadi ndogo zaidi kati ya wilaya zote, inazo trekta 20 tu. Vile vile Jedwali Na. XXXI linaonyesha wilaya ya Makete kuwa na idadi ndogo sana ya majembe ya kukokotwa na ng'ombe ikilinganishwa na wilaya zingine. Iringa 12,455, Njombe 14,507, Ludewa 1,475, Mufindi 5,460 na Makete 369 tu.

Kutokana na Sensa ya Watu ya 1988 Mkoa wa Iringa ulikuwa na Kaya 248,479. Ikichukuliwa kwamba kila kaya ingekuwa na trekta moja au plau moja au yote mawili ingemaanisha kwamba familia 32,141 tu zingekuwa na plau na familia 757 zingekuwa na trekta, hivyo kuacha kaya 215,541 bila kuwa na trekta au plau. Hali hii ingetufanya kufikia uamuzi kwamba Mkoa wa Iringa bado unatumia zana duni katika shughuli za kilimo. Hii inatusaidia pia kueleza kwa nini uzalishaji katika kilimo unaendelea kushuka.

**JEDWALI XXXI: ZANA ZA KILIMO ZINAZOKOKOTWA NA WANYAMA MSIMU 1994/95, KIWILAYA MKOANI IRINGA.**

| Zana za Kilimo na Wanyama wanaotumika | Wilaya | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Iringa | Mufind | Njomb | Ludewa | Make | Jumla |
| Maksai | 12,455 | 5,460 | 14,507 | 1,475 | 369 | 37,266 |
| Punda | 2,203 | 278 | 519 | 28 | 121 | 3,147 |
| Plau | 9,050 | 6,570 | 10,042 | 6,365 | 114 | 32,141 |
| Haro | 100 | 65 | 75 | 36 | 9 | 265 |
| Rija Ridgers) | 122 | 59 | 64 | 18 | 2 | 278 |
| Cultivator | 165 | 136 | 164 | 109 | 6 | 580 |
| Mikokoteni | 512 | 166 | 118 | 76 | 3 | 875 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Iidara ya Kilimo na Mifugo, Iringa.

**JEDWALI Na. XXXII: IDADI YA KAYA NA ZANA ZA KILIMO WALIZOKUWANAZO MSIMU WA KILIMO 1994/95.**

| Wilaya | Idadi ya Trekta | Idadi ya Plau | Idadi ya Harvesters | Idadi ya Kaya (Sensa ya 1988) |
|---|---|---|---|---|
| Iringa | 580 | 9,050 | 1 | 90,948 |
| Mufindi | 81 | 6,570 | 5 | 47,327 |
| Njombe | 80 | 10,042 | 2 | 65,075 |
| Ludewa | 36 | 6,365 | - | 19,981 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Makete | 20 | 114 | - | 25,148 |
| Jumla | 797 | 32,141 | 8 | 248,479 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Kilimo na Mifugo, Iringa.

d) **Hifadhi ya Mazao**:

Tatizo la hifadhi ya chakula linatokana na upungufu na uduni wa huduma ya hifadhi; hali ambayo husababisha mazao kuwa katika hali ya kuweza kushambuliwa na wadudu, panya na uharibifu wa aina nyingine ye yote wa mavuno. Bahati nzuri tatizo la uharibifu utokanao na hifadhi haupo Mkoani Iringa kutokana na kuwepo kwa hifadhi kwa njia za jadi katika kila kaya Mkoani. Yapo pia maghala ya hifadhi yaliyojengwa na Serikali.

Jedwali Na. XXXIII linaonyesha idadi ya maghala hayo, ujazo wake na mgawanyo kiwilaya.

**JEDWALI Na. XXXIII: IDADI YA MAGHALA UJAZO NA MGAWANYO KIWILAYA, MKOANI IRINGA 1996.**

| Wilaya | Idadi ya Maghala | Ujazo (Tani) |
|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 69 | 57 |
| Mufindi | 43 | 19,160 |
| Njombe | 84 | 53,8795 |
| Ludewa | 19 | 15,595 |
| Makete | - | - |
| Jumla | 215 | 146,000 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Kilimo na Mifugo, Iringa, 1996.

e) **Kilimo cha Umwagiliaji**:

Kilimo cha umwagiliaji hakitumiki sana mkoani Iringa japokuwa ipo mito, mabwawa na maziwa (ziwa Nyasa). Bahati nzuri Serikali ya Mkoa na Serikali Kuu zimetambua kuwepo kwa uwezekano wa kuendeleza kilimo hiki Mkoani. Imekwisha fahamika kwamba kuna watu/wakulima waliokwisha hamasishwa na kushauriwa kujishughulisha na kilimo cha umwagiliaji na kuunda vikundi kwa shughuli hiyo, vikundi vijulikanavyo kama "Vikundi vya matumizi bora ya maji katika kilimo". Vikundi hivi vinashauriwa kushirikiana na vikundi vinavyoshughulika na miradi ya kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya jadi. Taarifa iliyopo inaeleza kwamba vipo vijiji visivyopungua vitano vinavyoshiriki katika mradi huu wa umwagiliaji kwa njia ya jadi: Msosa Mbuyuni, Mfowelo, Ikula Mtandika na Msombwe. Jedwali Na. XXXIV linaonyesha maeneo muhimu yenye uwezekano wa kuendelezwa kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji wilayani Iringa na Makete.

**JEDWALI Na. XXXIV: MAENEO YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI MKOANI IRINGA 1996.**

| Wilaya | Kijiji | Eneo (Ha) Linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji | Eneo (Ha) Linalolimwa kwa kuwagiliwa |
|---|---|---|---|
| Iringa | Mahingu | 450 | |
| | Tungamalenga | 240 | 150 |
| | Idodi | 1680 | 80 |
| | Mapogoro | 807.2 | 375 |
| | Makifu | 1600 | 139 |
| | Nyamahana | 88 | 400 |
| | Mlowa | 368 | 61.2 |
| | Pawaga | 2000 | 600 |
| | Ruaha | 800 | 650 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mbuyuni | | |
| Makete | Mfumbi | 400 | 150 |
| | Kimani | 400 | 150 |
| | Lifua | 400 | 50 |

Chanzo: Ofisi ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Mkoa wa Iringa, 1996

Mazao yanayozalishwa katika kilimo cha umwagiliaji Mkoani Iringa ni: Mpunga, Vitunguu na Nyaya.

**Sasakawa Global 2000 (SG 2000):**

Madhumuni ya Mradi wa Sasakawa Global 2000

- Kuwapa utaalamu wakulima wa mahindi juu ya njia bora za matumizi ya mbolea na matumizi ya mbinu bora za kilimo.
- Kuwapatia wakulima pembejeo kwa njia ya mkopo.
- Kuwapa msaada wa kitaalam au ushauri wakulima wenye kuhitaji.
- Kuwapa msaada wafanyabiashara wanaoshughulika na biashara ya uuzaji wa pembejeo ili waweze kutoa huduma hiyo kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya wakulima.
- Kumjenga mkulima kuwa na uwezo wa kujitegemea na kuendelea kuwa hivyo katika kujipatia pemebejeo za kilimo pasipo kutegemea kukopeshwa.

Imekwisha elezwa katika taarifa kwamba SG 2000 imefanikiwa kuuwezesha Mkoa wa Iringa kutekeleza yafuatayo:-

- Ujenzi wa maghala 147 kati ya maghala 150 yaliyokuwa yamepangwa.

- Wakulima 9,715 wamepatiwa utaalam wa kilimo cha kisasa.

- Tani 1452.45 za mbolea na pemebejeo nyingine za kilimo ziliwafikia wakulima kwa njia ya mikopo.

**JEDWALI Na. XXXV: IDADI YA VIJIJI, WAKULIMA NA EKARI ZILIZO CHINI YA MRADI WA SG 2000.**

| Wilaya ya Iringa | 1989/90 | 1990/91 | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Vijiji | 20 | 34 | 30 | 31 | 20 |
| 2. Wakulima | 220 | 2247 | 1500 | 1230 | 300 |
| 3. Ekari | 220 | 2227 | 1500 | 1230 | 300 |
| **Wilaya ya Mufindi** | | | | | |
| 1. Vijiji | - | 13 | 13 | 17 | 10 |
| 2. Wakulima | - | 130 | 372 | 293 | 100 |
| 3. Ekari | - | 130 | 372 | 293 | 100 |
| **Wilaya Njombe** | | | | | |
| 1. Vijiji | 10 | 30 | 38 | 30 | 16 |
| 2. Wakulima | 100 | 2000 | 1626 | 1245 | 320 |
| 3. Ekari | 100 | 2000 | 1626 | 1245 | 320 |

Chanzo: Idara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Mkoa wa Iringa, 1996.

Jambo lisilokawaida katika Jedwali Na. XXXV ni kushuka kwa idadi ya wakulima washiriki katika mradi wa SG 2000. Kushuka si kwa wakulima tu bali pia kwa vijiji shiriki na idadi ya ekari zilizokuwa katika mradi. Kwa mfano kulikuwa na vijiji 20 vilivyokuwa katika mradi SG 2000 msimu 1989/90. Idadi hii iliongezeka hadi kufikia vijiji 34 msimu 1990/91 na baadaye


ikashuka kufikia vijiji 30 msimu 1991/92 na ikaendelea kushuka tena na kufikia vijiji 20 tu msimu wa 1993/94. Kwa upande wa wakulima taarifa inazidi kutisha zaidi. Wilaya ya Iringa ilianza na wakulima washiriki 220 msimu wa 1989/90, idadi hiyo ikaongezeka hadi wakulima 2,247msimu wa 1990/91. Ghafla idadi ikashuka hadi kufikia wakulima 300 tu msimu wa 1993/94, Wilaya ya Njombe nayo ilianza na wakulima 100 msimu wa kilimo wa 1989/90, ghafla idadi hiyo ikapanda juu sana hadi kufikia wakulima 2000 msimu wa 1990/91. Katika msimu wa 1993/94 idadi ya wakulima ilistaajabisha kwa kushuka ghafla kwa kiwango kikubwa kutoka wakulima 2000 hadi kufikia wakulima 320 tu. Mwelekeo huo wa kuzorota kwa mradi ulijitokeza pia katika idadi ya ekari zilizokuwa zimelimwa katika mradi. Inashangaza kusikia kutoka kwa uongozi wa Mkoa ukisema kwamba mradi wa SG 2000 umesaidia sana kuongeza uzalishaji wa mahindi mkoani kutoka magunia 12 kwa helta hadi magunia 25/Ha.

Kwa mujibu wa madhumuni na maelezo ya mradi was SG 2000 ilitarajiwa kwamba wahusika wote wangeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi huu; lakini yanayojitokeza katika Jedwali Na. XXXV inaonyesha hali tofauti na ilivyokuwa imetarajiwa. Kushuka kwa vigezo vyote vya mradi huu kunathibitisha ukweli kwamba mradi wa SG 2000 haukuwa na mafanikio katika Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo ni vyema kwa uongozi wa Mkoa kuchambua sababu zilizofanya mradi usifanikiwe na hivyo kurekebisha kasoro hizo ili zisije zikajirudia katika miradi mingine au ya namna hiyo ya uzalishaji mahindi.

Kilimo cha Mahindi katika Mikoa maarufu kwa kilimo cha zao hilo msimu 1994/95:

Jedwali Na. XXXVI linaonyesha idadi ya hekta zinazolimwa mahindi ikilinganishwa na hektari zinazofaa kwa kilimo cha zao hilo katika mikoa hiyo minne maarufu kwa kilimo cha mahindi.

**Kielelezo Na. 13: Mahindi yaliyozalishwa na mikoa inayozalisha kwa wingi Mbeya, Rukwa, Iringa na Ruvuma, 1994/95**




**JEDWALI Na. XXXVI: IDADI/(JUMLA YA HEKTA) YA MAENEO YANAYOFAA KWA KILIMO CHA MAHINDI MAENEO YALIYOPANDWA NA UZALISHAJI KATIKA MIKOA MINNE MASHUHURI KWA KILIMO CHA MAHINDI 1994/95.**

| Mikoa | Maeneo (Ha) | Maeneo yaliyopandwa (Ha) | Uzalishaji (Tani) | Wastani (Tani/Ha) |
|---|---|---|---|---|
| Ruvuma | 137,570 | 108,961 | 202,557 | 1.859 |
| Iringa | 243,306 | 149,013 | 266,027 | 1.785 |
| Mbeya | 193,555 | 93,533 | 286,276 | 3.061 |
| Rukwa | 100,057 | 71,113 | 136,348 | 1.917 |
| Jumla | 674,488 | 422,620 | 891,208 | 2.155 |

Chanzo: National Sample Census of Agriculture 1994/95 Report, Volume III.

Jedwali Na. XXXVI linaonyesha kwamba Mkoa wa Iringa inayo maeneo makubwa yanayofaa kwa kilimo cha mahindi kuliko mikoa mingine mitatu maarufu kwa mahindi. Vile vile mkoa ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya hekta zilizolimwa mahindi msimu wa kilimo 1994/95. Pamoja na umaarufu huu, mkoa wa Iringa ulikuwa na kiwango cha chini zaidi cha uzalishaji kwa kila hekta msimu 1994/95. Mkoa wa Mbeya ulikuwa unaongoza kwa kiwango cha juu cha uzalishaji kwa kila hekta ukifuatiwa na Mikoa ya Rukwa na Ruvuma. Pamoja na Kuwepo kwa mradi wa SG 2000 na Sera ya Mikoa Minne maarufu kwa kilimo cha mahindi kiwango cha uzalishaji Mkoani Iringa kilibakia chini, jambo ambalo mkoa sharti ulifuatilie na kuirekebisha.

f) **Hali ya Chakula**:

Kawaida mkoa wa Iringa unajitosheleza kwa chakula kutokana na hali nzuri ya hewa kwa shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali. Hakuna ushahidi uliokwisha kupatikana ukionyesha uhaba wa chakula mkoani humo; isipokuwa msimu wa 1994/95 ilitolewa taarifa kwamba kulikuwa na kaya 49,846 zilizokuwa zimekumbwa na upungufu wa chakula (nafaka) kwa kiwango cha tani 30,044. Maeneo yaliyopatikana na jenga hili ni: Tarafa za Pawaga, Idodi, Mahenge na Kalenga - Wilaya ya Iringa. Tarafa ya Malangali katika wilaya ya Mufindi na tarafa Wanging'ombe, baadhi ya maeneo (Usuka na Mdandu) katika tarafa ya Mdandu. Katika tarafa ya Makambako vijiji vya Mawande, Welela na Idofi. Wilayani Ludewa kata za Luilo na Iwela pia zilipata upungufu huo wa chakula msimu wa 1994/95. Jedwali Na. XXXVII linaonyesha ukubwa wa tatizo hili Mkoani Iringa msimu wa 1994/95.

**JEDWALI Na. XXXVII: UKUBWA WA TATIZO LA UHABA WA CHAKULA MKOANI IRINGA - MSIMU WA 1994/95**

| Wilaya | Idadi ya Kaya | Mahitaji ya nafaka (Tanii) | |
|---|---|---|---|
| | | Mahindi | Maharage |
| Iringa | 32,170 | 21,173 | 918 |
| Mufindi | 6,758 | 3,566 | - |
| Njombe | 9,688 | 4,271 | - |
| Ludewa | 1,230 | 116 | - |
| Jumla | 49,846 | 29,126 | 918 |


Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,Taarifa ya Maendeleo ya Kilimo, mwaka 1994/95, Mkoa wa Iringa.

Tatizo la upungufu wa chakula laweza kuepukwa kwa kulima mazao yanayostahimili ukame na yale yanayokomaa kwa kipindi kifupi. Mazao haya ni kama: mtama, muhogo, viazi vitamu, mbegu maalum ya mahindi (composite) n.k. na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mabonde.


## 2.3.2 Mifugo:

Ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo Mkoani Iringa ni moja wapo ya shughuli muhimu ya kiuchumi kwa jamii. Mkoa ulikuwa na ng'ombe 534,792, mbuzi 178,874, kondoo 79,136, punda 3,772 na farasi 297 (Sensa ya Mifugo 1984) inakisiwa kuwepo kwa ng'ombe wa maziwa 13,000 mkoani na asilimia 75 wanafugwa kwenye nyanda za juu ambako hali ya hewa ni nzuri kwa ufugaji. Jedwali Na. XXXVIII linaonyesha mgawanyo wa mifugo kiwilaya kulingana na Sensa ya mifugo ya 1984.

**Kielelezo Na. 14a: Mgawanyiko wa Mifugo (Ng'ombe) Kiwilaya Mkoani Iringa (Sensa ya Mifugo 1984)**


Makete
6%
Ludewa
6%
Njombe
25%
Iringa
47%
Mufindi
16%

**Kielelezo Na. 14b: Mgawanyiko wa Mifugo (Mbuzi) Kiwilaya Mkoani Iringa (Sensa ya Mifugo 1984)**





**JEDWALI Na. XXXVIII: MGAWANYIKO WA MIFUGO KIWILAYA MKOANI IRINGA (SENSA YA MIFUGO 1984)**


| Aina ya Mifugo | Wilaya | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Iringa | Mufindi | Njombe | Ludewa | Makete | Jumla |
| Ng'ombe | 253,264 | 81,873 | 135,275 | 30,650 | 23,730 | 534,792 |
| Mbuzi | 94,221 | 12,413 | 36,596 | 16,035 | 19,609 | 178,874 |
| Kondoo | 31,462 | 7,616 | 25,870 | 4,493 | 6,695 | 79,136 |
| Punda | 3,448 | 180 | 412 | 180 | 144 | 3,772 |

Chanzo: Idara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Mkoa wa Iringa.

**Kielelezo Na. 14c: Mgawanyiko wa Mifugo (Punda) Kiwilaya Mkoani Iringa (Sensa Ya 1984)**




**Kielelezo Na. 15: Mgawanyiko wa Mifugo (Ng'ombe) Kiwilaya Mkoani Iringa (Sensa ya Mifugo 1984)**




**JEDWALI Na. XXXIX: MGWANYIKA WA NG'OMBE WA MAZIWA NA MASHAMBA YA MIFUGO MKOA, IRINGA.**

| Wilaya | Idadi ya Ng'ombe wa Maziwa | Mashamba Makubwa ya Ng'ombe wa Maziwa | |
|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Mashamba | Idadi ya Ng'ombe wa Maziwa |
| Iringa Vijijini | 828 | 11 | 2,573 |
| Iringa Mjini | 296 | 2 | 687 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mufindi | 979 | 5 | 556 |
| Njombe | 2,133 | 4 | 415 |
| Ludewa | 207 | - | - |
| Makete | 1,314 | 1 | 2,821 |
| Jumla | 5,757 | 23 | 7,052 |

Chanzo: Idara ya Kilimo na Mifugo Mkoa, Iringa, 1996

Ng'ombe wana umuhimu wake wa pekee kwa maisha ya wananchi kwa kuwapatia nyama ya maziwa na hivyo kuinua hali yao ya lishe. Idadi ya ng'ombe wa maziwa ni 12,809 wakimilikiwa na wafugaji wadogo wadogo na wakubwa na Mashirika ya Umma (kama vile DAFCO). Katika shamba la ng'ombe wa maziwa Kituko wapo ng'ombe wa maziwa wapatao 360 na hutoa lita za maziwa zipatazo 906,372 kwa mwaka. Uzalishaji wa maziwa mkoani huathiriwa na uhaba wa soko la maziwa na tatizo la usafirishaji na hifadhi. Jedwali Na. XL linaonyesha uzalishaji wa maziwa mkoani Iringa msimu wa 1992/93 hadi 1995/96.

**JEDWALI Na. XL: UZALISHAJI WA MAZIWA MKOA WA IRINGA, 1992/93 - 1995/96**

| Mwaka | Uzalishaji (Lita) |
|---|---|
| 1992/93 | 3,443,713 |
| 1993/94 | 3,722,720 |
| 1994/995 | 4,018,713 |
| 1995/96 | 4,179,457 |
| Jumla | 15,364,603 |

Chanzo: Idara ya Kilimo na maendeleo ya Mifugo Mkoa, Iringa.

**JEDWALI Na. XLI: HALI YA HUDUMA ZA MIFUGO ILIYOPO KIWILAYA, MKOA WA IRINGA 1996**

| Wilaya | Majosho | Machinjio | Vibanio | Vituo vya Afya | Mabanda ya Ngozi |
|---|---|---|---|---|---|

| | yaliyopo | Mahitaji | yaliyopo | mahitaji | vilivyopo | Mahitaji | Vilivyopo | Mahitaji | Yaliyopo | Mahitaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 64 | 90 | 6 | 12 | 2 | 15 | 5 | 9 | 6 | 12 |
| Iringa Mjini | 2 | 2 | 2 | 3 | - | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 |
| Mufindi | 40 | 63 | 7 | 10 | 8 | 8 | 3 | 5 | 7 | 10 |
| Njombe | 34 | 86 | 7 | 12 | 2 | 4 | 5 | 7 | 7 | 12 |
| Ludewa | 9 | 25 | 3 | 7 | 1 | 1 | 2 | 4 | 3 | 7 |
| Makete | 17 | 47 | 1 | 6 | - | 1 | 1 | 5 | 1 | 6 |
| Jumla | 272 | 313 | 26 | 50 | 13 | 30 | 16 | 31 | 25 | 50 |

Chanzo: Idara ya kilimo na Maendeleo ya Mifugo Mkoa, Iringa, 1996.

Majosho na vituo vya afya ni muhimu sana kwa huduma ya mifugo, kiwango kilichopo hakitoshekezi mahitaji. Kwa mfano mahitaji ya majosho ni 313 Mkoani lakini yaliyopo ni 272 tu. Wilaya zote Mkoani zina tatizo hili la upungufu wa majosho. Vile vile kuna upungufu wa vituo vya afya. Iringa Vijijini imeathirika sana na tatizo hili. Iringa Vijijini inatakiwa iwe na vituo 9 lakini kulikuwepo na vituo 5 tu. Pamoja na tatizo la uhaba wa huduma muhimu za mifugo tatizo la vifo vya mifugo nalo ni kubwa. Matatizo yasababishayo vifo vingi ni ugonjwa wa ndigana na homa za mapafu. Kuharibika kwa majosho, gharama kubwa ya madawa ya kupe huwafanya wafugaji wengi washindwe kuogesha mifugo yao.

### 2.3.3 Maliasili:

i) Mkoa wa Iringa unayo rasilimali kubwa itokanayo na misitu. Yapo mapori ya hifadhi 67 ikiwa ni pamoja na hifadhi ya msitu wa Sao Hill na mapori mengine. Msitu wa Sao Hill ni maarufu siyo tu kutokana na hadhi yake ya hifadhi bali kwa sababu ni moja wapo ya chanzo cha mto Ruaha. Kutokana na umaarufu wa msitu wa Sao Hill Serikali ilitambua uwezekano wa kujenga na kuendesha mtambo wa Karatasi wa Mgololo ambao ni mkubwa kuliko yote iliyopo kusini mwa jangwa la Sahara. Pamoja na ukubwa uliopo wa msitu wa Sao

Hill bado upo umuhimu wa kuutumia kwa uangalifu ili usije ukatumika ovyo bali kwa lengo la kuhifadhi. Inafahamika wazi kwamba iwapo misitu itakatwa bila utaratibu mzuri au kukatwa ovyo misitu hiyo hupotea baada ya muda mfupi tu na hivyo uwezo wake wa kutosheleza mahitaji ya binadamu nayo pia hupunguka. Juhudi za uongozi mkoani za kuhifadhi misitu zinatia moyo na pale pale kuotesha miche kwa wingi kwa lengo la kuendeleza maeneo ya misitu hasa kwenye maeneo yenye miti michache au hakuna kabisa. Jedwali Na. XLII linaonyesha idadi ya misitu ya hifadhi na misitu kwenye maeneo ya chanzo cha maji/mito kiwilaya Mkoani Iringa.

**JEDWALI Na. XLII: IDADI YA MISITU YA HIFADHI NA MAPORI KWENYE VYANZO VYA MAJI/MITO, KIWILAYA MKOANI IRINGA.**

| Wilaya | Idadi ya Misitu ya Hifadhi | Misitu ya Vyanzo vya Maji/Mito | Maeneo ya Hifadhi | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Misitu ya Hifadhi (Ha) | Misitu ya Vyanzo vya Maji/Mito (Ha) |
| Iringa | 13 | 11 | 159,100 | 155,302 |
| Mufindi | 23 | 18 | 47,338 | 16,690 |
| Njombe | 20 | 6 | 17,146 | 23,026 |
| Ludewa | 4 | 4 | 7,504 | 7,504 |
| Makete | 6 | 6 | 23,026 | 44,495 |
| Jumla | 66 | 45 | 253,976 | 247,017 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa.

Jedwali Na. XLII linaonyesha umaarufu wa Wilaya ya Iringa katika suala zima la hifadhi ya misitu, ipo misitu ya hifadhi yenye ukubwa wa Hekta 159,100 na misitu ya vyanzo vya maji/mito

hekta 155,302. Wilaya ya Mufindi ina misitu ya hifadhi 23 ambayo ni idadi kubwa zaidi ya wilaya zote ikifuatiwa na wilaya ya Njombe yenye misitu ya hifadhi 20. Mkoa umekuwa ukifanya juhudi ya kuotesha miche kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yaliyo wazi; juhudi hii imeanza tangu 1975. Angalia Jedwali Na. XLIII.

**JEDWALI Na. XLIII: IDADI YA MICHE ILIYOOTESHWA NA IDADI YA HEKTA ILIYOPANDWA MKOANIIRINGA, MWAKA 1975 - 1995.**

| Mwaka | Idadi ya Miche | Hekta Zilizopandwa |
|---|---|---|
| 1975 | 349,114 | 440 |
| 1976 | 182,644 | 458 |
| 1977 | 611,514 | 339 |
| 1978 | 1,008,034 | 536 |
| 1979 | 2,365,166 | 569 |
| 1980 | 2,922,276 | 1,732 |
| 1981 | 4,232,975 | 1,724 |
| 1982 | 2,044,227 | 1,582 |
| 1983 | 3,007 | 1,735 |
| 1984 | 4,577,979 | 2,797 |
| 1985 | 4,508,820 | 2,703 |
| 1986 | 3,744,793 | 1,866 |
| 1987 | 4,708,808 | 2,185.4 |
| 1988 | 3,490,603 | 1,745.3 |
| 1989 | 4,958,221 | 2,529.1 |
| 1990 | 14,066,495 | 2,945 |
| 1991 | 7,078,095 | 3,945 |
| 1992 | 5,574,563 | 3,395.6 |
| 1993 | 5,874,073 | 2,937 |
| 1994 | 6,332,969 | 3,166.5 |
| 1995 | 5,748,720 | 2,874.4 |
| Jumla | 84,383,096 | 42,203.8 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa.

Jedwali Na. XLIII lionaonyesha kwamba kuanzia mwaka 1975 hadi 1995 Mkoa umekuwa ukijishughulisha na uoteshaji na upandaji miti. Kiwango cha zoezi hili unatofautiana mwaka hadi mwaka. Jedwali na. XLIV linaonyesha makundi mbalimbali yaliyojihusisha na uoteshaji na upandaji miti Mkoani Iringa, 1986 - 1994.

**JEDWALI Na. XLIV: IDADI YA MICHE ILIYOOTESHWA NA KUPANDWA NA VIKUNDI MBALIMBALI MKOANI IRINGA, 1986 - 1994.**

| Mwaka | Idadi ya Miche iliyooteshwa na Vikundi | | | | | Maeneo yaliyopandwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idaa za Serikali | Vijiji | Taasisi za Kidini | Taasisi za Elimu | Wafadhili wa Jamii | |
| 1986 | 1,872,000 | 418,000 | 13,866 | 63,255 | 1,377,672 | 1,866 |
| 1987 | 2,596,169 | 677,231 | 177,500 | 82,000 | 837,908 | 2,185.4 |
| 1988 | 958,985 | 549,962 | 150,204 | 192,540 | 1,630,912 | 1,745.3 |
| 1989 | 1,848,912 | 531,607 | 18,287 | 302,433 | 2,356,982 | 2,529.1 |
| 1990 | 908,400 | 2,768,20 | 1,565,645 | - | 647,750 | 2,945 |
| 1991 | 2,500,000 | 637,790 | 1,678,000 | 878,917 | 2,195,000 | 3,945 |
| 1992 | 2,614,895 | 298,114 | 1,255,000 | 173,138 | 2,450,000 | 3,395.6 |
| 1993 | 2,448,193 | 211,000 | 1,200,000 | 155,192 | 1,859,688 | 2,937 |
| 1994 | 2,400,228 | 287,248 | 1,639,813 | 25,485 | 1,980,195 | 3,166.5 |
| Jumla | 18,147,782 | 6,379,152 | 7,698,315 | 1,872,960 | 15,336,107 | 24.715 |

Chanzo: Idara ya Maliasili Mkoa, Iringa, 1996

Vikundi mbalimbali vilijihusisha na uoteshaji/upandaji miti yaani, shule, idara za Serikali, Taasisi za Dini, Vijiji na Wafadhili mbalimbali. Kati ya mwaka 1986 hadi 1994 Idara za Serikali ziliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya miche iliyootesha (miche 18,147,782) zikifuatiwa na vikundi vya wafadhili ambavyo viliotesha miche 15,336,107 katika kipindi hicho. Taasisi za elimu zilikuwa za mwisho katika kufanikisha zoezi hili. Jedwali XLV linaonyesha idadi ya miche iliyooteshwa na kupandwa kiwilaya Mkoani Iringa mwaka 1995.

**JEDWALI Na. XLV: MICHE ILIYOOTESHWA NA KUPANDWA KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Miche iliyooteshwa | Maeneo Yaliyopandwa |
|---|---|---|
| Iringa | 1,361,471 | 680.7 |
| Mufundi | 1,256,041 | 628 |
| Njombe | 2,881,514 | 1,440.8 |
| Ludewa | 83,035 | 41.5 |
| Makete | 166,659 | 83.32 |
| Jumla | 5,748,720 | 2,873.52 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili Iringa, 1996.

Kulingana na Jedwali Na. XLV, wilaya ya Njombe iliongoza kwa idadi ya miche iliyooteshwa, ikifuatiwa na wilaya za Iringa na Mufindi. Aidha wilaya ya Njombe iliongoza kwa idadi kubwa ya hekta zilizopandwa miti mwaka 1995, ambapo wilaya hiyo ilipanda hekta 1,440.8 ikilinganishwa na hekta 41.5 za wilaya ya Ludewa, Makete hekta 83.32 na Mufindi hekta 628.

ii) **Wanyamapori**:

Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa michache yenye utajiri wa wanyamapori. Ukweli huu unadhihirika na kuwepo kwa mbuga za wanyama mbili. Ruaha na Udzungwa. Vile vile Mkoa una maeneo mawili mapori tengefu ya wanyama (Game Controlled areas): Luanda/Mkwambi na Kihongosa. Mbuga ya wanyama ya Ruaha ina ukubwa wa kilometa za mraba 10,300; Luanda/Mkwambi ina eneo la kilometa za mraba 6,817 na Kihongosa 30 $km^2$. Jedwali Na. XLVI linaonyesha ukubwa wa maeneo ya mbuga za wanyama na hifadhi ya mbuga za wanyama.

**JEDWALI Na. XLVI: AINA NA ENEO LILILO HIFADHIWA KWA AJILI YA WANYAMAPORI.**

| Aina | Ukubwa wa Eneo |
|---|---|
| A. Hifadhi ya Wanyamapori | |
| 1. Ruaha | 10,300 $km^2$ |
| 2. Udzungwa | 1,990 $km^2$ |
| B. Maeneo yaliyopendekezwa kuwa Hifadhi ya Wanyamapori:(Mapori tengfu) | |
| 1. Luanda/Mkwambi | 6,817 $km^2$ |
| 2. Kihongosa | 30 $km^2$ |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa, 1996.


Mbuga za wanyamapori za Ruaha na Udzungwa tofauti na mbuga nyingine zimeendelea kuhifadhi hali zake za kiasili kwa maisha ya viumbe vyote waishio katika mbuga hizo. Hii imetokana na kutoingiliwa na shughuli za binadamu. Mbuga za Ruaha ni ya pili kwa ukubwa baada ya mbuga ya Serengeti jina la mbuga hii limetokana na jina la Mto Ruaha ambao unapita eneo la mashariki la mbuga. Vipo vivutio vingi katika mto huu yakiwemo maporomoko ya maji na uzuri wa eneo. Wanyama kama viboko, mamba na pia samaki, hupatikana kwa wingi ndani ya mto huu. Mbuga ya Ruaha ina idadi ya wanyama mbalimbali isipokuwa suara aina ya Thomsongazelle, nyumbu na topi. Zipo aina mbalimbali ya ndege zaidi ya 370ndani ya mbuga na baadhi yake hawajawahi kuonekana katika mbuga za ukanda wa kaskazini mwa Tanzania. Kama ilivyo katika mbuga nyingine za wanyama nchini uwindaji haramu umeshamiri ndani ya mbuga hii. Jedwali Na. XLVII na Na. XLVIII yanatoa mwanga juu ya ukubwa wa tatizo hili katika mbuga za hifadhi za wanyamapori mkoani Iringa.

**JEDWALI Na. XLVII: IDADI YA WAWINDAJI HARAMU NA MATUKIO YALIYOTOLEWA TAARIFA 1980 - 1992**

| Mwaka | Idadi ya Wawindaji haramu walioshikwa | Idadi ya Matukio |
|---|---|---|
| 1980 | 624 | 19 |
| 1981 | 9 | 13 |
| 1982 | 132 | 13 |
| 1983 | 6 | 18 |
| 1984 | - | 68 |
| 1985 | 21 | 57 |
| 1986 | 18 | 26 |
| 1987 | 27 | 20 |
| 1988 | 36 | 11 |
| 1989 | 456 | 22 |
| 1990 | 24 | 10 |
| 1991 | 427 | 55 |
| 1992 | - | 15 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa, 1996

**Kielelezo Na. 16: Mapato Yaliyopatikana Kutokana na Shughuli za Wanyamapori 1990/91 - 1995/96 (T.Shs.)**



**JEDWALI Na. XLVIII: MAPATO YALIYOPATIKANA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA WANYAMAPORI 1990/91 - 1995/96 (T.SHS.)**

| Mwaka | Leseni Uwindaji | Leseni za kutengeneza Bidhaa za wanyamapori | Uuzaji wa Bidhaa za wanyamapori | Uuzaji wa kadi za wanyamapori | Adhabu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1990/91 | 1,473,237 | 8,000 | 2,400 | - | 83,800 | 1,567,437 |
| 1991/92 | 679,971 | 1,800 | 46,00 | 5,800 | 92,000 | 826,571 |
| 1992/93 | 796.650 | 4,200 | 12,000 | 17,200 | 50,000 | 880,050 |
| 1993/94 | 2,131,353 | 1,400 | 21,500 | 13,200 | 49,000 | 2,216,453 |
| 1994/95 | 1,777,829 | 600 | 1,600 | 15,400 | 217,600 | 2,011,829 |
| 1995/96 | 1,945,155 | 800 | - | 15,000 | 137,000 | 2,097,955 |

Chanzo: Idara ya Maliasili, Mkoa, Iringa 1996.

**JEDWALI Na. XLIX: IDADI YA MASALIA YA WANYAMAPORI NA SILAHA ZILIZOSHIKWA KUTOKA KWA MAJANGIRI 1985 - 1993**

| Mwaka | Idadi ya Pembe za Ndovu | Meno Viboko | Ngozi za Chui | Ngozi za mamba | Silaha (Bunduki) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1985 | 692 | - | 3 | - | 24 |
| 1986 | 146 | - | 1 | - | 12 |
| 1987 | 11 | - | - | - | 6 |
| 1988 | 14 | - | 1 | - | - |
| 1989 | 24 | - | - | - | 5 |
| 1990 | - | - | - | - | 1 |
| 1991 | 34 | 12 | 1 | 3 | - |
| 1992 | 367 | - | - | - | 7 |
| 1993 | - | - | - | - | 1994 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa.

## iii) Uvuvi:

Moja ya shughuli muhimu kwa wakazi wa Mkoa wa Iringa wanaoishi kando kando ya ziwa na mabwawa ni uvuvi. Maeneo maarufu kwa uvuvi mkoani ni Ziwa Nyasa. Bwawa la Mtera Ziwa Ngwazi wilayani Mufindi na bwawa la Itombololo.

Shughuli za uvuvi hufanyika katika mito ya Ruaha Mkuu na Ruaha. Uvuvi unafanyika zaidi katika Ziwa Nyasa ambalo kwa upande wa Tanzania lina ufuko wa urefu wa km. 260. Kilometa zipatazo 20 za ufuko zimo Mkoani Mbeya na zilizobaki zimegawanyika karibu nusu kwa nusu kati ya mikoa ya Iringa na Ruvuma. Ufuko katika Mkoa wa Iringa wote uko wilayani Ludewa na karibu ufuko huu wote haupitiki isipokuwa katika eneo la Manda kutokana na milima ya Livingstone inayopakana na Ziwa hili.

Uvuvi katika Mkoa wa Iringa unafanyika zaidi katika Ziwa Nyasa na Bwawa la Mtera. Shughuli hii huzalisha samaki wa kutosheleza mahitaji ya mkoa na ziada hupata masoko katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Ruvuma, Morogoro na hata Dar es Salaam. Bwawa la Mtera ni la kujengwa. Uvuaji katika bwawa hili uko chini ya uwezo wake, hali hii imetokana na uongozi mkoani kushindwa kusimamia na kuendeleza shughuli za uvuvi. Pia zana duni za uvuvi kama vile nyavu na vyombo vya kuvulia zimechangia kuleta ufanisi mdogo wa uvuvi mkoani. Jedwali Na. I hapo chini linaonyesha viwango vya samaki vilivyopatikana katika ziwa Nyasa na katika mabwawa, pia na vyombo vya kuvulia na idadi ya wavuvi mkoani.

**MUHTASARI WA TAKWIMU ZA UVUVI MKOANI IRINGA.**

**1. BWAWA LA MTERA, WILAYANI IRINGA.**

| Mwaka | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya vyombo vya uvuvi | Uzito wa samaki (Tani) | Thamani ya samaki waliovuliwa (T.Shs. '000) |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | 970 | 713 | 2,779.5 | 186,737.5 |
| 1991 | 822 | 665 | 315.2 | 210,352.21 |
| 1992 | 722 | 681 | 5037.05 | 511,642.11 |
| 1993 | 789 | 316 | 2346.34 | 489,124.75 |
| 1994 | 660 | 602 | 128.21 | 34,611.10 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1995 | 563 | 503 | 98.35 | 39,056.083 |

## 2. BWAWA LA ITOMBOLOLO, WILAYANI NJOMBE

| Mwaka | Idadi ya wavuvi | Idadi ya Vyombo vya Uvuvi | Uzito wa samaki (Tani) | Thamani ya Samaki (T.Shs. '000) |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | 26 | 24 | 59.8 | 4771.2 |
| 1991 | 28 | 21 | 63.10 | 5030.81 |
| 1992 | 18 | 18 | 43.12 | 3253.83 |
| 1993 | 38 | 10 | 9.84 | 2235.88 |
| 1994 | 132 | 25 | 6.005 | 1804.2 |
| 1995 | - | - | - | - |


## 3. ZIWA NYASA WILAYA YA LUDEWA:

| Mwaka | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya vyombo vya Uvuvi | Uzito wa Samaki (Tani) | Thamani ya Samaki waliovuliwa (T.Shs. '000) |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | 486 | 494 | 4,084.48 | 129,540.75 |
| 1991 | 568 | 717 | 2,925.9 | 125,587.89 |
| 1992 | 471 | 587 | 3,113.7 | 149,410.5 |
| 1993 | 320 | 322 | 2,623.71 | 289,648.47 |
| 1994 | 271 | 265 | 20.058 | 4,011.6 |
| 1995 | 334 | 240 | 56.518 | 5,986.5 |

## 4. BWAWA LA NGAZI WILAYA YA MFUNDI.

| Mwaka | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya vyombo vya Uvuvi | Uzito wa Samaki (Tani) | Thamani ya Samaki (T.Shs. '000) |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | 23 | 26 | 30.2 | 2,327.9 |
| 1991 | 87 | 41 | 61.81 | 2,061.8 |
| 1992 | 10 | 10 | 14.36 | 2,106.06 |
| 1993 | 38 | 10 | 9.84 | 2,235.88 |
| 1994 | 25 | 12 | 4.5 | 1,480.75 |
| 1995 | 32 | 9 | 3.5 | 1,635.7 |

**Kielelezo Na. 17: Jumla ya samaki waliovuliwa (maelfu ya tani), Mkoa wa Iringa**




## Soko la Samaki:

Kwa kawaida idadi kubwa ya samaki wanaovuliwa mkoani huuzwa wakiwa wabichi kwa matumizi ya mara moja au hukaushwa kwa moshi, jua, kukaangwa au kukaushwa kwa chumvi. Upo uharibifu wa samaki kwa kiwango fulani kutokana na hifadhi duni. Licha ya kiwango cha chini cha uvuaji samaki mkoani, bado mkoa unafanikisha kuuza nje katika mikoa ya Dar es salaam, Songea, Morogoro, Mbeya na Dodoma.


## iv) Ufugaji Nyuki:


Inafahamika kwamba zaidi ya asilimia 60 ya mkoa wa Iringa unafaa kwa ufugaji wa nyuki. Maeneo yote ya misitu ya Miombo na eneo lote sambamba na mto Ruaha. Maeneo yanayofaa zaidi kwa ufugaji wa nyuki ni kama yafuatayo:

| Wilaya | Eneo (Kijiji) |
|---|---|
| Iringa | Kiwere, Idodi, Pawaga, Image, Ibumu, Kilolo, Ipalamwa, Makungu, Ukwega, Mahenge, Mtandika na Udekwa. |
| Mufindi | Ipilima, Kiponda, Kwatwanga, Magunguli, Makungu, Sadani, Chogo, Malangali, Uhafiwa, Mapanda, King'eng'e, Ukosani, Mgololo na maeneo yanayopakana na Mashamba ya Chai ya Brooke Bond. |
| Njombe | Igula, Iyai, Mayale, Ikabula, Igekedza, Igominyi, Mpululu, Udonja, Banawanu, Ujindile, na Maeneo ya Lupembe. |
| Ludewa | Mbwila, Ludende, Lugarawa, Mkongobaki, Shauri Moyo, Milo, Mapogoro, Mavala, Mawengi na Luana. |
| Makete | Mfumbi, Ikuwo, Lupila, Matamba, Iwawa, Tandala, Idende na Kising'a. |

Kutokana na takwimu zilizopo wapo wafugaji wa nyuki 1210 mkoani Iringa. Hata hivyo wafugaji wengi hutumia mizinga ya asili. Jedwali L linaonyesha aina ya ufugaji wa nyuki na pato lipatikanalo.

**Kielelezo Na. 18: Muhtasari wa Uwiano wa ufugaji wa nyuki na uvunaji wa nta (kilo) kiwilaya, Mkoa wa Iringa**



**JEDWALI L: UFUGAJI WA NYUKI NA MAPATO YALIYOPATIKANA 1992/93 - 1994/95 MKOANI IRINGA.**

| Mwaka | Wilaya | Aina ya Mizinga | | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Asili idadi | Yakisasa idadi | Uzito (Kg) | Thamani (Shs. '000) | Uzito (Kg | Thamani (T.Shs'000) |
| 1992/93 | Iringa | 6110 | 524 | 45,400 | 22,700 | 2,580 | 1,290 |
| | Mufindi | 7,320 | 1,632 | 47,230 | 23,615 | 2610 | 1,305 |
| | Njombe | 9,517 | 249 | 33,640 | 16,820 | 1978 | 989 |
| | Ludewa | 3,812 | 64 | 32,310 | 16,155 | 1621 | 8,105 |
| 1993/94 | Iringa | 8,406 | 530 | 34,300 | 20,500 | 2287 | 1,372.2 |
| | Mufindi | 12,482 | 101 | 38,890 | 23,334 | 2593 | 1,555.8 |
| | Njombe | 10,720 | 270 | 30,870 | 18,522 | 2058 | 1,234.8 |
| | Ludewa | 1,314 | 108 | 2,475 | 17,325 | 695 | 417 |
| 1994/95 | Iringa | 10,120 | 537 | 12,000 | 7,200 | 613 | 919.5 |
| | Mufindi | 12,490 | 182 | 48,340 | 29,004 | 2417 | 1,450.2 |
| | Njombe | 11,200 | 300 | 51,770 | 51,770 | 2875 | 2,875 |
| | Ludewa | 3,827 | 114 | 3,396 | 23,772 | 675 | 405 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maliasili, Iringa.

Inaonekana katika Jedwali Na. L kwamba kuna mizinga michache tu ya kisasa inayotumika ikilinganishwa na idadi ya mazinga ya asili. Msimu wa 1992/93 wilaya ya Mufindi ilikuwa na mizinga mingi zaidi ya kisasa kuliko wilaya nyingine zote ikifuatiwa na wilaya ya Iringa. Hata hivyo idadi ya mizinga ya kisasa wilayani humo ilishuka ghafla kutoka idadi ya mizinga ya kisasa 1632 mwaka 1992/93 hadi kufikia mizinga 182 msimu wa 1994/95. Hali ilikuwa tofauti kwa wilaya ya Iringa ambapo idadi ya mizinga ya kisasa iliongezeka kutoka 524 msimu 1992/93 hadi kufikia 537 msimu wa 1994/95. Wilaya ya Njombe nayo ikaongeza kutoka 249 msimu wa 1992/93 hadi 300 msimu wa 1994/95. Wilaya ya Ludewa mizinga ya kisasa 64 msimu wa 1992/93 hadi 114 msimu wa 1994/95. Ufugaji wa nyuki ni njia moja wapo inayomwongezea pato mwananchi anayejishughulisha na ufugaji nyuki. Hivyo basi ni budi juhudi madhubuti zitumike ili kuhakikisha kwamba utumiaji wa mizinga ya asili unapunguka na kuongeza idadi ya matumizi ya mizinga ya kisasa. Kwa kufanya hivyo mfugaji atajipatia asali na nta nyingi zaidi kutokana na mauzo ya asali na nta. Msimu wa 1992/93 wafugaji nyuki wilayani Mufindi waliongeza mapato

kutokana na shughuli hiyo, walipata Shs. milioni 23.615 kutokana na asali na Shs. milioni 1.305 kutokana na mauzo ya nta. Hivyo hivyo kwa msimu wa 1993/94 (Jedwali L). Wilaya ya Njombe iliongoza katika msimu wa 1994/95 wafugaji nyuki walijipatia pato la Shs. milioni 51.77 kutokana na mauzo ya asali na Shs. milioni 2.875 kutokana na mauzo ya nta.

### 2.3.4 Viwanda:

Mkoa wa Iringa ulikuwa na viwanda vidogo vidogo vipatavyo zaidi ya 250 vikijihusisha na Useremala, ufugaji, ufinyanzi, utengenezaji sabuni, gereji, usagaji nafaka, utengenezaji matofali, utengenezaji ngozi n.k. Viwanda vya kati ni pamoja na viwanda vya: Cotex, Ufumaji nguo, Vacu-lug, Ukataji almasi, kiwanda cha Ruaha Bottling, kiwanda cha misumari, kiwanda cha kusindika matunda cha Dabaga, kiwanda cha mbao cha Sao Hill, kiwanda cha Chai cha Stone Valley, (chai) kiwanda cha kusindika Pareto, viwanda vya chai vya Lupembe na Luponde na kampuni ya Miwati.

Kipo kiwanda kikubwa kimoja tu mkoani Iringa nacho ni kiwanda cha Karatasi cha Mgololo. Mkoa wa Iringa bado unanafasi ya kupanua shughuli zake za viwanda ili hatimaye uweze kuongeza biashara yake na nchi ya jirani ya Malawi.

### 2.3.5 Madini:

Mkoa wa Iringa siyo maarufu kwa uchimbaji wa madini, kutokana na hali hii sekta ya madini ina mchango mdogo sana katika pato la Mkoa. Hata hivyo yapo maeneo kadhaa yameonyesha uwezekanowa kuwa na madini katika Mkoa wa Iringa. Kiwilaya maeneo yenye kuonyesha dalili ya kuwa na madini ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| Wilaya | Madini yanayowezekana Kupatikana |
|---|---|
| Njombe | Manganese oxide, Titano magnetite, Shaba, Carbonitites, makaa ya mawe, Kaolin, Soap Stone, dhahabu, Kimberlite, Platinum |
| Makete | Shaba, Chuma. Soap Stone, Kaolin Manganese, Chrome, Dhahabu, Talc, Ochre. |
| Iringa | Kaolin, Chokaa, Magnitite na Chuma. |
| Ludewa | Makaa ya mawe, chuma, dhahabu, Kimberlite, Almasi, Yelloescope, Rubby, green Tomalite. |
| Mufindi | Magnitite na dhahabu. |


## SEHEMU YA III

### 3.0 MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

### 3.1 Mtandao wa Barabara:

Zipo jumla ya kilometa 4,867 za mtandao wa barabara mkoani Iringa. Hii inajumuisha barabara Kuu za Kitaifa, barabara zilizopo chini ya Mkoa, wilaya na za vijijini. Sehemu kubwa ya barabara ya Tanzania - Zambia (TAZAM Road) iko mkoani Iringa ikianzia Mbuyuni katika wilaya ya Iringa hadi Iyayi wilayani Njombe. Iko barabara nyingine Kuu ya lami inayoanzia Makambako na kupitia mjini Njombe hadi milima ya Lukumbulu (Mkoani Iringa) na kuendelea hadi mjini Songea Mkoani Ruvuma. Ipo barabara nyingine Kuu (Changarawe) inayotoka Iringa mjini kwenda Mkoa wa Dodoma kupitia Bwawa la Mtera. Pamoja na kuwepo kwa mtandao huu wa barabara, ipo reli maarufu ya TAZARA (Tanzania/Zambia) inayoanzia Dar es Salaam hadi Iringa na Mbeya. Kwa ujumla huduma ya uchukuzi katika mkoa wa Iringa ni nzuri ikilinganishwa na mikoa mingine Tanzania Bara. Kasoro inayojitokeza ni kwenye barabara za vijijini kutokana na kutopitika wakati wa masika. Jedwali na. LI linaonyesha aina za barabara na urefu wake.

**Kielelezo na. 18: Uwiano wa Aina ya Barabara, Mkoa wa Iringa**




**JEDWALI Na. LI: AINA ZA BARABARA - MKOANI IRINGA.**

| Aina ya Barabara | Urefu (km) |
|---|---|
| Barabara Kuu | 788.09 |
| Barabara za Mkoa | 1212.88 |
| Barabara za Wilaya | 2075.0 |
| Barabara za Vijijini | 2599.0 |
| Jumla | 6,674.97 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa: Mikakati ya kuwaongezea kipato wananchi wa Mkoa wa Iringa, 1996.

Tofauti na hali ilivyo ya mikoa mingine, urefu wa barabara za wilaya na za vijijini karibu unalingana katika mkoa wa Iringa. Asilimia 31 ya urefu wa barabara zote Mkoani ni barabara za kiwilaya na asilimia 39 ni barabara za vijijini. Ni jambo la kawaida kwa barabara za vijijini kuwa na urefu mkubwa zaidi kutokana na umuhimu kiuchumi wa barabara hizi kwa wananchi vijijini. Kwa hiyo Mkoa unahitaji barabara nyingi zaidi za vijijini ili kuleta msukumo wa maendeleo na vile vile kurahisisha uchukuzi wa mizigo na huduma vijijini.

**JEDWALI LII - AINA ZA BARABARA NA SURA ZAKE MKOANI IRINGA.**

| Aina ya Barabara | Sura ya Barabara | |
|---|---|---|
| | Lami (Km) | Changarawe/Udongo (Km) |
| Barabara Kuu | 477.3 | 310.79 |
| Barabara za Mkoa | - | 1212.88 |
| Barabara za Wilaya | - | 2075.00 |
| Barabara za Vijijini | | 2599.00 |
| Jumla | 477.3 | 6197.67 |

Kuimarika kwa mtandao wa barabara na kuongezeka kwa idadi na urefu wa barabara ni muhimu sana katika kuendeleza kilimo katika maeneo mapya, kuimarisha biashara na vile vile kurahisisha usafiri wa watu. Zipo barabara kadhaa mkoani Iringa ambazo ni vikwazo kwa maendeleo ya wananchi kutokana na uchakavu.

Jedwali LIII linaonyesha urefu wa barabara kiwilaya Mkoani Iringa. Wilaya ya Makete ina kilometa chache zaidi za barabara ukilinganishwa na wilaya nyingine mkoani. Hata hivyo mkoa unahitaji barabara zaidi ili kuimarisha sekta ya kiuchumi.

**Jedwali Na. LIII - Mtandao wa Barabara Kiwilaya, Mkoa wa Iringa.**

| Wilaya | Aina ya Barabara | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Barabara Kuu (km) | Barabara za Mkoa (km) | Barabara za Wilaya (km) | Barabara za Vijijini (km) | Jumla (km) |
| Iringa | 278.0 | 415.92 | 532.0 | 834.0 | 2059.92 |
| Mufind | 178.5 | 210.03 | 360 | 475.0 | 1223.53 |
| Njomb | 140.0 | 276.21 | 430 | 656.0 | 1502.2 |
| Ludew | 179.59 | 80.34 | 565 | 320.0 | 1144.95 |
| Makete | 12.0 | 230.38 | 2,075.0 | 314.0 | 744.38 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | 788.09 | 1212.88 | 2,075.0 | 2,599.0 | 6,674.97 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuuwa Mkoa, Idara ya Ujenzi Mkoa, Iringa, 1996.

Barabara zifuatazo zimepangwa katika umuhimu wa kwanza katika kuziendeleza:

- Malangali - Manda
- Kitulo - Matamba - Mfumbi.
- Ipogoro - Kilolo - Kidabaga - Bombang'ombe - Idete.
- Ipogoro - Kilolo - Kidabaga - Bombang'ombe - Mwatasi
- Ipogoro - Kilolo - Kidabaga - Bombang'ombe - Kibengu
- Ilula - Mkaranga - Kilolo
- Mkaranga - Udekwa - Mahenge
- Lupembe - Ikondo - Idete - Kiyowela
- Ikondo - Lima - Upami - Ibiki Igongolo - Kifumbe - Mahongole - Nyigo.
- Nyigo - Ikuna - Mtwango.
- Mfuliza - Taveta - Ulanga
- Nkenja - Ikuwo - Uselimwani.
- Lusala - Lupila - Mlangali.
- Njombe - Iyayi.
- Wanging'ombe - Wang'ulwa - Banawanu - Mwango.
- Nyigo - Saja - Uhenga - Ufwala.
- Kinyanambo - Sadani - Ikweba - Kwatanga.
- Mafinga - Ihalimba - Usokami - Kidengu.
- Mawambala - Kidengu
- Mapanda - Kihansi
- Ifwagi - Mdabulo - Ihanu - Lulanda - Mapanga - Mlimba.

- Kalenga - Kiponzelo - Wassa - Ikugwe - Lugoba.
- Wasa - Ufyambe - Mahuninga - Tungamalenga.
- Pawaga - Mawande - Nyamahana.
- Isimani - Kihorogota - Igula - Nyakavangala
- Ilula - Vitono - Ihambingeto - Ilambilole - Mahongwi - Ndolela.
- Muholo - Lugarawa - Madilu - Madope
- Idofi - Igomba - Saja - Ufwale.
- Darajani - Ilembula - Mawande - Welela.
- Nyigo - Mgololo.
- Lumbila - Lupila - Kipengere.
- Makete - Isapulano - Ikuwo - Mfumbi.
- Mlowa - Lunda - Pawaga - Izazi.
- Kihologota - Nyakarangala.
- Idete - Kimala - Ukwega - Ipalamwa - Wotalisoli - Ilula - Ibumu.
- Mawambala - Usokami - Ihalimba - Mafinga.
- Lusia - Mivi - Mudindi.
- Lupembe - Mfiriga - Mdeke
- Banawanu - Igelango - Wangutwa - Wanging'ombe.
- Wanging'ombe - Kanamalenga - Usuka - Mdandu.

## 3.2 Usafiri wa Anga:

Mkoa wa Iringa umahudumiwa na viwanja vidogo vitatu: Nduli, Njombe na Mafinga. Kiwanja kidogo cha Nduli pekee kimewekewa lami na hivyo kuwezesha ndege za aina ya Fokker kutua na kuruka. Vile vile kiwanja cha Njombe kinacho uwezo huu kama kiwanja cha Nduli. Kiwanja cha Mafinga kinaruhusu ndege ndogo ndogo tu.

## 3.3 Mtandao wa Mawasiliano:

Wilaya zote tano Mkoani zinahuduma ya Posta na Simu. Makao Makuu ya wilaya za Iringa, Njombe na Mafinga yanahuduma ya "Telex" pia na "Fax". Mkoa wa Iringa una njia za simu 1215, njia za "telefax" 19, njia 51 za telex na radio call 9.

## 3.4 Nishati:

### i) Umeme

Umeme ni nishati muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na pale ambapo haupo si rahisi kuendesha shughuli za viwanda. Mkoa wa Iringa haujapata huduma ya umeme wakutosha. Takwimu za Sensa ya Watu ya 1988 zaonyesha asilimia 98 za kaya Mkoani hazikuwa na huduma ya Umeme. Jedwali LIV linaonyesha wazi wazi idadi ya kaya kiwilaya mkoani ambazo zilikuwa na umeme na zile bila umeme mwaka 1988

**JEDWALI Na. LIV: IDADI YA KAYA KIWILAYA ZILIZOKUWA NA UMEME MKOANI IRINGA, 1988**

| Wilaya | Jumla ya Kaya | Kaya zenye Umeme | Kaya bila Umeme | Asilimia ya Kaya enye Umeme |
|---|---|---|---|---|
| Iringa Mjini | 20361 | 3266 | 17060 | 16 |
| Iringa Vijijini | 71969 | 357 | 71612 | 0.5 |
| Mufindi | 48454 | 523 | 47931 | 1.1 |
| Njombe | 67658 | 1,461 | 66186 | 2.2 |
| Ludewa | 29706 | 394 | 19308 | 2.0 |
| Makete | 24790 | 31 | 2475 | 0.1 |
| Kimkoa | 252938 | 6032 | 246906 | 2.4 |

Chanzo: Iringa Regional Statistical Abstract, 1991.

Jedwali LIV laweka wazi hali ya upatikanaji wa huduma ya umeme mkoani. Kwa ujumla mkoa wa Iringa haukuwa umehudumiwa vyema. Ukiondoa wilaya ya Iringa mjini, wilaya

zilizobaki zilikuwa zimehudumiwa kwa viwango vya chini sana. Wilaya ya Njombe asilimia 2.2 tu ya kaya zilikuwa na huduma ya umeme mwaka 1988, ukifuatiwa na wilaya ya Kudewa kwa asilimia 2 tu. Ni jambo la kushangaza kwa mkoa mzima kuwa na asilimia 2.4 tu ya kaya zenye umeme. Hata Makao Makuu ya Mkoa yenyewe yalikuwa na asilimia 16 tu ya Kaya zenye huduma ya umeme. Wilaya iliyokuwa imehudumiwa kwa kiwango cha chini zaidi ni wilaya ya Makete ikifutatiwa na wilaya ya Iringa Vijijini. Mkoa wa Iringa ukilinganishwa na Mkoa wa Kilimanjaro wenye umeme aslimia 30.3 ya vijiji, tofauti inaonyesha ni kwa kiwango gani mkoa unatakuwa kufanya kazi ya kuleta maendeleo katika maisha ya wananchi wake vijijini ili wafikie mahali oa kuweza kuelewa umuhimu wa nishati hii kwa maendeleo yao.

ii) **Aina nyingine za Nishati:**

Mahitaji ya nishati ya aina nyingine kwa matumizi ya nyumbani yanazidi kuongezeka mkoani Iringa, hii inatokana na kuongezeka kwa idadi ya watu. Mahitaji ya kuni mkoani ni mita za ujazo 2,101,000 kwa mwaka. Utafiti umekwishaonyesha kwamba mkoa unao uwezo wa kutoa kuni kwa kiwango cha mita za ujazo 1,593,000 kwa mwaka. Hii ina maana kwamba kuna upungufu wa kuni za mita za ujazo 508,000. Kuongezeka kwa mahitaji ya nishati hii mijini na vijijini kunasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa ukataji misitu. Mfano hai ni ule wa Tarafa ya Ismani, tarafa ambayo miaka michache tu ilikuwa maarufu kwa kilimo cha mahindi lakini sasa haina uwezo wa kuzalisha mahindi tena. Katika kuandaa mikakati ya jinsi ya kuzuia kuenea kwa uharibifu wa maeneo, uongozi wa Mkoa hauna budi kutafuta mbinu za matumizi bora zaidi ya kuni na mkaa, kama vile matumizi ya majiko bora ya mkaa/kuni, ukaushaji bora wa

tumbaku na chai, matumizi ya biogas na nguvu ya mionzi ya jua kwa matumizi ya nyumbani.

# SEHEMU YA IV

## 4.0 HUDUMA ZA JAMII

### 4.1 Elimu:

#### 4.1.1 Shule za Awali:

Shule za awali zimetayarishwa ili kukidhi mahitaji ya elimu kwa watoto kati ya miaka 3 - 6. Idadi ya shule za awali kutoka mkoani ni kipimo kimojawapo cha maendeleo ya elimu katika mkoa husika. Mwaka 1995 Mkoa wa Iringa ulikuwa na shule za awali 92 tu ambapo Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa nazo 325. Jedwali na. LVI linaonyesha mgawanyo wa shule za awali kiwilaya mkoani Iringa, 1995.

**JEDWALI na. LVI: MGAWANYO WA SHULE ZA AWALI KIWILAYA, MKOA WA IRINGA MWAKA 1995.**

| Wilaya | Idadi ya Shule za Awali | |
|---|---|---|
| | 1994 | 1994 |
| Iringa Vijijini | 11 | 12 |
| Iringa Mjini | 18 | 22 |
| Mufindi | 10 | 11 |
| Njombe | 13 | 18 |
| Makete | 11 | 15 |
| Ludewa | 12 | 14 |
| Jumla | 75 | 92 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa: Mikakati ya kuwaongezea kipato wananchi wa Mkoa wa Iringa, 1996.

Takwimu za Jedwali Na. LVI zinaonyesha idadi ndogo ya shule za awali mkoani Iringa. Ni ukweli kabisa kwamba elimu ya shule za awali zinamtayarisha mtoto kwa masomo ya shule za msingi na baadaye. Kwa sababu hiyo, uongozi wa mkoa budi utilie maanani uanzishaji wa shule hizi katika maeneo mengi ili kukidhi mahitaji ya mkoa. Kwa wastani wilaya zote mkoani zina idadi ndogo ya shule hizi ikilinganishwa na mahitaji.

**JEDWALI LVII: IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA AWALI KIJINSIA NA KIWILAYA MWAKA 1994 NA 1995, MKOA WA IRINGA.**

| Wilaya | Idadi ya Wanafunzi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1994 | | | 1995 | | |
| | Wavulana | Wasichana | Jumla | Wavulana | Wasichana | Jumla |
| Iringa Vijijini | 391 | 427 | 818 | 360 | 250 | 710 |
| Iringa Mjini | 643 | 621 | 1264 | 807 | 774 | 1581 |
| Mufindi | 273 | 307 | 580 | 253 | 259 | 512 |
| Njombe | 353 | 375 | 728 | 503 | 533 | 1036 |
| Makete | 310 | 360 | 670 | 382 | 461 | 843 |
| Ludewa | 329 | 369 | 698 | 379 | 379 | 758 |
| Jumla | 2,299 | 2,459 | 4,758 | 2,684 | 2,756 | 5,440 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa: Mikakati ya kuwaongezea kipato wananchi wa Mkoa wa Iringa, 1996.

Majedwali Na. LVI na Na. LVII yote mawili yanadhihirisha ukweli wa uchache wa shule za awali Mkoani Iringa ikilinganishwa na idadi ya shule za msingi 723 na idadi ya wanafunzi darasa la I wanafunzi 43,125 mwaka 1995. Matatizo ya maendeleo ya shule za awali ni kama yafuatayo:

- Uchache wa madarasa na vifaa
- Mwamko mdogo wa wazazi juu ya umuhimu wa kuwapeleka shule za awali watoto wao.

- Michango midogo ya wazazi kwa shule hizo.
- Uhaba wa chakula cha watoto wa shule hizo za awali.
- Ushirikiano mdogo wa viongozi wa wilaya katika uanzishaji/ujenzi wa shule za awali.

### 4.1.2 Elimu ya Msingi:

Mwaka 1995 Mkoa wa Iringa ulikuwa na jumla ya shule za msingi za Serikali 723 zenye wanafunzi 236,542, ukilinganisha na wanafunzi 40,448 mwaka 1970. Idadi ya wanfunzi darasa la I iliongezeka kutoka 5,066 mwaka 1970 hadi 21,437 mwaka 1995, aidha idadi ya wasichana iliongezeka kutoka 3,410 mwaka 1970 hadi 21,658 mwaka 1995. Ongezeko la wanafunzi ni sawa na asilimia 323 kwa wavulana na asilimia 536 kwa wasichana.

Jedwali Na. LVIII linaonyesha kupanuka kwa elimu mkoani katika kipindi cha 25(19970 - 1995)

**JEDWALI Na. LVIII(a): KUKUA KWA SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI 1970 - 1995.**

| Wilaya | Idadi ya Shule za Msingi 1970 | Idadi ya Shule za Msingi 1985 | Idadi ya Shule za Msingi 1995 |
|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 55 | 184 | 187 |
| Iringa Mjini | - | 26 | 29 |
| Mufindi | 28 | 134 | 138 |
| Njombe | 109 | 175 | 205 |
| Ludewa | - | 65 | 77 |
| Makete | - | 83 | 87 |
| Jumla | 192 | 667 | 723 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu (Takwimu za Kielimu) 1970 - 1995.

Takwimu katika Jedwali Na. LVIII zinaonyesha kwamba idadi ya shule za msingi za Serikali ziliongezeka kwa asilimia kutoka mwaka 1970 hadi 1995, ukifuatiwa na wilaya za Iringa Vijijini asilimia 240 na wilaya ya Njombe kwa asilimia 88. Wilaya ya Ludewa na Makete zimeanzishwa baada ya mwaka 1970.

**JEDWALI Na. LVIII(b): IDADI YA MIKONDO YA SHULE ZA MSINGI KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | D A R A S A | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | I | II | III | IV | V | VI | VII | Jumla |
| Iringa Vijijini | 80 | 72 | 69 | 67 | 63 | 58 | 56 | 465 |
| Iringa Mjini | 331 | 310 | 298 | 299 | 277 | 259 | 259 | 2023 |
| Mufindi | 263 | 228 | 224 | 213 | 188 | 165 | 165 | 1446 |
| Njombe | 349 | 316 | 295 | 291 | 286 | 243 | 259 | 2039 |
| Ludewa | 118 | 115 | 108 | 91 | 87 | 79 | 81 | 679 |
| Makete | 95 | 96 | 98 | 92 | 93 | 83 | 89 | 464 |
| Jumla | 123 | 113 | 1,09 | 104 | 994 | 887 | 909 | 7,298 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa, Takwimu za Elimu, 1970 - 1995.

Jedwali LVIII(b) linaonyesha idadi ya mikondo iliyo kwa kila darasa kiwilaya. Wilaya ya Njombe ilikuwa na mikondo mingi zaidi kwa darasa la I; hii ina maana kwamba wilaya ilikuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kupokea wanafunzi darasa la Kwanza kuliko wilaya nyingine zote mkoani. Wilaya ya Iringa Vijijini ilikuwa na idadi ndogo zaidi yaani mikondo 80.

**JEDWALI Na. LVIII(c): IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI MWAKA 1970 - 1995 KIJINSIA NA KIWILAYA MKOA WA IRINGA.**

| Wilaya | Wanafunzi 1970 | | Wanafunzi 1985 | | Wanafunzi 1995 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Wavulama | Wasichana | Wavulana | Wasichana |
| Iringa Vijijijini | 7,615 | 4,603 | 31,085 | 32,333 | 34,008 | 34,854 |
| Iringa Mjini | - | - | 5,693 | 6,554 | 8,307 | 8,821 |
| Mufindi | 3,955 | 2,223 | 20,594 | 20,712 | 22,742 | 23,595 |
| Njombe | 13,217 | 8,825 | 26.864 | 28,138 | 31,303 | 32,797 |
| Ludewa | - | - | 9,166 | 9,741 | 9,528 | 9,918 |
| Makete | - | - | 10,756 | 10,889 | 10,126 | 10,541 |
| Jumla | 24,787 | 15,661 | 104,158 | 108,367 | 116,01 | 120,526 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa: Takwimu za Elimu, 1970 - 1995.

Kati ya mwaka 1985 na 1995 wilaya ya Iringa vijijini ilikuwa na ongezeko la asilimia 9 ya wanafunzi wavulana kutoka wanafunzi 31,085 hadi 34,008 na wasichana waliongezeka kwa asilimia 8 kutoka 32,333 hadi 34,854. Wilayani Njombe kulikuwepo ongezeko la asilimia 16 kwa wasichana na kwa wavulana. Tofauti na wilaya nyingine, wilaya ya Makete ilikuwa na upungufu wa wanafunzi katika ya kipindi hicho. Idadi ya wavulana ilishuka kutoka 10,756 hadi 10,126 na wasichana kutoka 10,889 hadi 10,541. Matarajio yalikuwa idadi ya wanafunzi ingeongezeka. Kwa sababu hiyo upo umuhimu wa kutafuta na kuchunguza sababu ya kupunguka kwa idadi ya wanafunzi wilayani humo. Inawezekana kwamba kiwango cha kuzaliana wilayani Makete kimepungua au watoto wengi wanakufa kabla hawajafikia umri wa kwenda shule au wazazi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao shuleni.

**JEDWALI Na. LVIII (d): WATOTO WALIOINGIA DARASA LA I KIWILYA NA KIJINSIA MWAKA 1985 NA 1995 MKOA WA IRINGA.**

| Wilaya | Wavulana | | Wasichana | |
|---|---|---|---|---|
| | **1985** | **1995** | **1985** | **1995** |
| Iringa Vijijini | 5,059 | 6,154 | 5,030 | 6,218 |
| Iringa Mjini | 1,070 | 1,475 | 1,185 | 1,457 |
| Mufindi | 3,320 | 4,475 | 2,365 | 4,523 |
| Njombe | 4,613 | 5,824 | 4,722 | 5,841 |
| Ludewa | 1,470 | 1,963 | 1,487 | 2,031 |
| Makete | 1,631 | 1,546 | 1,653 | 1,618 |
| Jumla | 17,151 | 21,437 | 17,462 | 21,688 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa, Takwimu za Elimu 1970 -1995.


Aidha watoto wavulana kwa wasichana walioingia darasa la I wilayani Makete mwaka 1995 walikuwa pungufu ikilinganishwa na idadi ya walioingia darasa hilo mwaka 1985 (Jedwali LVIII(d), sababu hazijulikani.

**JDWALI Na. LVIII(e): IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI KIJINSIA NA KIDARASA 1988-01995 MKOANI IRINGA.**

| Jinsia | Mwaka | DARAJA | | | | | | | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | V | VI | VII | |
| | 1988 | 17,948 | 15,454 | 15,054 | 20,610 | 9,985 | 8,840 | 11,676 | 99,567 |
| | 1989 | 17,985 | 16,361 | 14,866 | 17,442 | 15,345 | 9,602 | 9,178 | 100.997 |
| Wavulana | 1990 | 18,193 | 15,583 | 14,924 | 16,277 | 12,618 | 14,749 | 9,260 | 101.604 |
| | 1991 | 17,359 | 17,538 | 16,545 | 16,098 | 14,375 | 12,923 | 15,056 | 109,894 |
| | 1995 | 21,437 | 19,049 | 17,551 | 16,483 | 15,135 | 12,950 | 13,213 | 115,818 |
| | 1988 | 17,754 | 15,129 | 15,037 | 22,820 | 10,513 | 9,531 | 12,765 | 103,549 |
| | 1989 | 17,953 | 15,930 | 14,866 | 18,937 | 16,759 | 10,135 | 9,052 | 103,632 |
| Wasichana | 1990 | 17,656 | 16,292 | 15,429 | 16,277 | 13,029 | 16,113 | 9,647 | 104,443 |
| | 1991 | 17,217 | 17,161 | 16,532 | 16,558 | 14,777 | 13,135 | 16,541 | 111,920 |
| | 1995 | 21,688 | 19,469 | 18,125 | 17,047 | 15,880 | 13,861 | 14,654 | 120,724 |
| Jumla | 1988 | 35,702 | 30,583 | 30,091 | 43,430 | 20,498 | 18,371 | 24,441 | 203,116 |
| | 1989 | 35,938 | 32,291 | 29,514 | 36,379 | 32,104 | 19,737 | 18,230 | 204,193 |
| | 1990 | 35,849 | 31.875 | 30,353 | 33,173 | 25,547 | 30,862 | 18,907 | 206,566 |
| | 1991 | 34,576 | 34,699 | 33,076 | 32,656 | 29,252 | 26,058 | 31.597 | 221,914 |
| | 1995 | 43,125 | 38.518 | 35,676 | 33,530 | 31,015 | 26,811 | 27.867 | 236,542 |

Chanzo: Mkoa wa Iringa - Takwimu za Elimu, 1979 - 1995.

**Kielelezo Na. 19: Idadi ya Wanafunzi Katika Shule za Msingi za Serikali Kiwilaya na Kijinsia Mkoa wa Iringa, 1995**




Kulingana na Jedwali Na. LVIII(e) idadi ya wanafunzi wavulana (darasa I-VII) iliongezeka kwa asilimia 16 kutoka 99,567 mwaka 1988 hadi 115,818 mwaka 1995. Wakati huo huo idadi ya wanafunzi wasichana ilizidi kidogo tu ile ya wavulana kwa asilimia moja kutoka 103,549 mwaka 1988 hadi 120,724 mwaka 1995. Yapo mambo mawili ya msingi kwanza idadi ya wanawake kawaida ni kubwa kuliko ile ya wanaume, vile vile vifo vya watoto wasichana ni vichache kulingana na vile vya watoto wavulana. Kwa mantiki hii uwezekano wa wasichana kuishi hadi kufikia umri wa kwenda shule ni mkubwa kuliko ule wa watoto wavulana. Kutokana na sababu hii na mambo mengine yakawa sawa kwa watoto wote ingetazamiwa idadi ya wasichana wanaosoma kuwa kubwa. Jedwali Na. LVIII(f) pia linaonyesha idadi ya watoto wanaosoma (darasala I - VII) katika shule za msingi za Serikali kiwilaya mwaka 1995.

Mwaka 1995 wilaya ya Iringa vijijini ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wa kike (Darasa I - VII) 35,052, kuliko wilaya nyingine mkoani Iringa. Wilaya ya Njombe ilifuatia kwa wasichana 32,797. Wilaya ya Makete ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya wanafunzi wa kiume walikuwa 9,918 tu.

**JEDWALI Na. LVIII(f): IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI KIWILAYA NA KIJINSIA MKOA WA IRINGA, 1995.**

| Mkoa | Jinsia | DARAJA | | | | | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | V | VI | VII | |
| Iringa Mjini | Wavulana | 1,475 | 1,333 | 1,311 | 1,200 | 1,085 | 985 | 920 | 8,309 |
| | Wasichana | 1,457 | 1,385 | 1,301 | 1,298 | 1,165 | 1,161 | 1,054 | 8,819 |
| | Jumla | 2,930 | 2,718 | 2,612 | 2,498 | 2,250 | 2146 | 1974 | 17,128 |
| Iringa Vijijini | Wavulana | 6,154 | 5,462 | 5,048 | 4,832 | 4,466 | 4,119 | 3,729 | 33,810 |
| | Wasichana | 6,218 | 5,635 | 5,198 | 4,964 | 4,516 | 4,138 | 4,185 | 35,052 |
| | Jumla | 12,372 | 11,097 | 10,246 | 9,796 | 8,982 | 8,257 | 8,112 | 68,862 |
| Mufindi | Wavulana | 4,475 | 3,849 | 3,510 | 3,312 | 2,778 | 2,407 | 2,411 | 22,742 |
| | Wasichana | 4,523 | 3,841 | 3,720 | 3,407 | 2,936 | 2,546 | 2,622 | 23,595 |
| | Jumla | 8,998 | 7,690 | 7,230 | 6,719 | 5,714 | 4,953 | 5,033 | 46,337 |
| Njombe | Wavulana | 5,824 | 5,075 | 4,601 | 4,398 | 4,258 | 3,404 | 3,743 | 31,303 |
| | Wasichana | 5,841 | 5,104 | 4,794 | 4,682 | 4,604 | 3,686 | 4,186 | 32.797 |
| | Jumla | 11,665 | 10,179 | 9,395 | 8,980 | 8,862 | 7,090 | 7,929 | 64,100 |
| Ludewa | Wavulana | 1,963 | 1,778 | 1,650 | 1,367 | 1,187 | 1,050 | 1,131 | 10,126 |
| | Wasichana | 2,031 | 1,910 | 1,681 | 1,410 | 1,263 | 1,112 | 1,134 | 10,541 |
| | Jumla | 3,994 | 3,688 | 3,331 | 2,777 | 2,450 | 2,162 | 2,265 | 20,667 |
| Makete | Wavulana | 1,546 | 1,552 | 1,431 | 1,374 | 1,361 | 985 | 1,279 | 9,528 |
| | Wasichana | 1,618 | 1,594 | 1,481 | 1,386 | 1,396 | 1,218 | 1.275 | 9,918 |
| | Jumla | 3,164 | 3,146 | 2,862 | 2,760 | 2,757 | 2,203 | 2,554 | 19,446 |
| Total | Wavulana | 21,437 | 19,049 | 17,551 | 16,483 | 15,135 | 12,950 | 13,213 | 115,818 |
| | Wasichana | 21,688 | 19,469 | 18,175 | 17,147 | 15,880 | 13,861 | 14,456 | 120,774 |
| | Jumla | 43,125 | 38,518 | 35,726 | 33,530 | 31.015 | 26,811 | 27,867 | 236,592 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu - Takiwmu za Elimu 1970 - 1995.

**JEDWALI na. LVIII(g) KUONGEZEKA KWA IDADI YA SHULE ZA MSINGI 1980 - 1995 MKOANI IRINGA.**

| Wilaya | Idadi ya Shule | | | | | | Ongezeko 1985 Hadi 1995 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1980 | 1982 | 1985 | 1992 | 1994 | 1995 | |
| Iringa (V) | 184 | 184 | 184 | 186 | 187 | 187 | 2 |
| Iringa (M) | 27 | 27 | 26 | 26 | 29 | 29 | 11.5 |
| Mufindi | 133 | 134 | 134 | 135 | 136 | 138 | 3 |
| Njombe | 173 | 175 | 175 | 195 | 195 | 205 | 17 |
| Ludewa | 66 | 66 | 65 | 74 | 76 | 77 | 18.5 |
| Makete | 84 | 84 | 83 | 87 | 87 | 87 | 5 |
| Jumla | 667 | 670 | 667 | 703 | 711 | 723 | 8.4 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, Takwimu za Elimu, 1980 - 1995.

**JEDWALI Na. LVIII(h) ONGEZEKO LA IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI MKOANI IRINGA KIPINDI CHA 1980 - 1995.**

| **Wilaya** | **Idadi ya Wanafunzi** | | | | | | **Ongezeko 1985 - 1995** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1980 | 1982 | 1985 | 1990 | 1994 | 1995 | **Asilimia** |
| Iringa (V) | 67,200 | 73,542 | 63,418 | 56,926 | 67,173 | 68,862 | 8.6 |
| Iringa (M) | 8,893 | 13,830 | 12,247 | 14,501 | 37,433 | 7,128 | 40 |
| Mufindi | 43,138 | 45,723 | 41,306 | 40,153 | 43,379 | 46,337 | 12.2 |
| Njombe | 54,153 | 58,837 | 55,002 | 57,610 | 62,349 | 64,100 | 16.5 |
| Ludewa | 18,630 | 20,754 | 18,907 | 17,611 | 20,400 | 19,446 | 3 |
| Makete | 22,202 | 24,443 | 21,645 | 19,866 | 19,532 | 20,667 | 4.5 |
| Jumla | 214,216 | 237,187 | 212,525 | 206,667 | 230,266 | 236,540 | 11.3 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, Iringa - Takwimu za Elimu 1980 - 1995.

Jedwali Na. LVII(g) na LVIII(h) yanalinganisha ongezeko la shule za msingi za Serikali na idadi ya wanafunzi kutoka 1980 - 1995. Wilaya ya Ludewa ilikuwa na ongezeko la asilimia 18.5, kiwango kikubwa zaidi ya wilaya nyingine kwa kipindi kati ya 1985 hadi 1995 na kufuatiwa na wilaya ya Njombe. Katika kipindi cha miaka 10 (1985 - 1995) wilaya ya Iringa vijijini iliongeza shule za msingi kwa asilimia 2 tu ikifuatiwa na wilaya ya Mufindi asilimia 3. Lakini cha kushangaza ni kwamba

wilaya ya Ludewa ambayo iliongeza idadi ya shule za msingi kwa asilimia 18.5 kati ya 1985 na 1995, ongezeko la idadi ya wanafunzi katika kipindi hicho cha 1985 - 1995 (darasa I - VII) ilikuwa ya chini kulingana na wilaya zote mkoani Iringa; lilikuwa asilimia 3 tu. Wilaya ya Njombe iliongeza idadi ya wanafunzi kwa asilimia 16.5. Wilaya ya Njombe ilikuwa ya pili baada ya Ludewa katika ongezeko la shule za msingi kati ya 1985 - 1995. Kwa sababu zisizoeleweka idadi ya wanafunzi wilayani Makete ilishuka kutoka 21,645 mwaka 1985 hadi 20,667 mwaka 1995.

**JEDWALI Na. LVIII(i): IDADI YA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUINGIA KITADO CHA I KIJINSIA, MKOA WA IRINGA, KWAKA 1970 - 1995.**

| Mwaka | Watahiniwa | | | Waliochaguliwa kuingia Kidato cha I | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasuchana | Jumla | Wavulana | % | Wasichana | % | Jumla | % |
| 1970 | 1,725 | 796 | 2,521 | 208 | 12 | 62 | 8 | 270 | 11 |
| 1975 | 4,097 | 2,243 | 6,340 | 279 | 7 | 105 | 5 | 384 | 6 |
| 1980 | 7,092 | 4,644 | 11,736 | 253 | 3.6 | 118 | 2.5 | 371 | 3.2 |
| 1985 | 14,049 | 14,296 | 28,345 | 445 | 3.2 | 239 | 1.7 | 684 | 2.4 |
| 1990 | 9,040 | 9,655 | 18,695 | 617 | 7 | 486 | 5 | 1,103 | 5.9 |
| 1995 | 12,574 | 13,787 | 26,361 | 750 | 6 | 703 | 5 | 1,453 | 5.5 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, Iringa - Takwimu za Elimu 1970 - 1995

**JEDWALI LVIII(j): WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA I KIJINSIA NA KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1985 NA 1995.**

| Wilaya | Watahiniwa | | | | Idadi Waliochaguliwa Kidato cha I | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | | Wasichana | | Wavulama | | Wasichana | | Jumla | |
| | 1985 | 1995 | 1985 | 1995 | 1985 | 1995 | 1985 | 1995 | 1985 | 1995 |
| Iringa (V) | 4,149 | 3,719 | 4,094 | 4,098 | 110 | 150 | 51 | 125 | 161 | 275 |
| Iringa (M) | 682 | 918 | 802 | 999 | 57 | 143 | 55 | 138 | 112 | 281 |
| Mufindi | 2,451 | 2,258 | 2,551 | 2,475 | 94 | 100 | 51 | 100 | 145 | 200 |
| Njombe | 3,866 | 3,440 | 4,070 | 3,960 | 112 | 196 | 44 | 195 | 156 | 391 |
| Ludewa | 1,339 | 1,070 | 1,234 | 1,096 | 36 | 95 | 17 | 86 | 53 | 181 |
| Makete | 1,562 | 1,169 | 1.543 | 1,159 | 46 | 64 | 21 | 59 | 67 | 123 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | 14,049 | 12,574 | 14,294 | 13,787 | 455 | 748 | 239 | 703 | 694 | 1,451 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, Iringa - Takwimu za Elimu 1970 - 1995.

**JEDWALI Na. LVIII(k): IDADI YA WANAFUNZI MKOANI IRINGA WALIOJIUNGA NA KIDATO CHA I KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI ZA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Jina la Shule za Sekondari | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| 1. Gagliero | | 190 | 190 |
| 2. Highlands | 72 | 52 | 124 |
| 3. Mwembetogwa | 99 | 83 | 182 |
| 4. Ruaha | 35 | 18 | 53 |
| 5. Kalenga | 25 | 19 | 44 |
| 6. Pomerini | 60 | 47 | 107 |
| 7. Udzungwa | 23 | 19 | 42 |
| 8. Ukumbi | 54 | 14 | 68 |
| 9. Consolata Seminary | - | - | - |
| 10. Den Bosco | 40 | - | 40 |
| 11. Igowole | 33 | 29 | 62 |
| 12. Itengule | 24 | 10 | 34 |
| 13. Kibengu | 44 | 39 | 83 |
| 14. Mafinga | 53 | 44 | 97 |
| 15. Mafinga Seminary | 46 | - | 46 |
| 16. Mdabuzo | 14 | 24 | 38 |
| 17. Mgololo | 41 | 28 | 69 |
| 18. Sadani | 41 | 17 | 58 |
| 19. Kigugala Seminary | 28 | 16 | 44 |
| 20. Kifanya | 17 | 20 | 37 |
| 21. Lupembe | 34 | 26 | 60 |
| 22. Makambako | 38 | 35 | 73 |
| 23. Makoga | 24 | 12 | 36 |
| 24. Mpechi | 56 | 52 | 108 |
| 25. Mtwango | 69 | 51 | 120 |
| 26. Uwemba | 15 | 28 | 43 |
| 27. Wanging'ombe | 75 | 73 | 148 |
| 28. Madunda | 27 | 19 | 46 |
| 29. Bulongwa | 19 | 25 | 44 |
| 30. Itamba | 41 | 33 | 74 |
| 31. Lupalilo | 15 | 13 | 28 |
| 32. Lupila | 14 | 11 | 25 |
| Jumla | 1,176 | 1,047 | 2,223 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu - Takwimu za Elimu 1970 - 1995.

Majedwali Na. LVIII(i) - LVIII (k) yanaonyesha idadi ya wanafunzi wa Mkoa wa Iringa waliojiunga na shule za Sekondari mbalimbali. Idadi ya wanafunzi ambao wamejiunga na shule za sekondari za Serikali imekuwa ikiongezeka kutoka wanafunzi 270 mwaka 1970 hadi 1,453 mwaka 1995. Mwaka 1970 wasichana 62 tu walichaguliwa kuingia shule za Sekondari za Serikali ikilinganishwa na wavulana 208 mwaka huo. Hadi mwaka 1995 hali imebadilika, idadi ya wasichana walioingia Kidato cha I iliongezeka kwa asilimia 1, 034 kutoka wasichana 62 mwaka 1970 hadi 703 mwaka 1995.

Jedwali Na. LVIII(j) linaonyesha wilaya ya Njombe iliandikisha wanafunzi wengi zaidi kujiunga na Kidato cha I katika shule za Serikali mwaka 1995 kuliko wilaya nyingine Mkoani Iringa. Wilaya iliandikisha wasichana 196 na wilaya ya Iringa Vijijini wasichana 125, Mufindi 100 Ludewa 86 na Makete wasichana 59. Lakini mwaka 1985 wilaya ya Njombe ilipeleka wasichana 44 katika shule za sekondari za Serikali, ambapo wilaya za Mufindi na Iringa Vijijini kila moja ilipeleka wasichana 51 katika shuke hizo. Katika hali yeyote ile asilimia kubwa zaidi ya wanafunzi wavulana wamekuwa wakijiunga na shule za sekondari za Serikali kuliko ile ya wasichana. Jedwali Na. LVIII(i) na Jedwali Na. LVIII (j) yanaonyesha wanafunzi 26,361 darasa la VII waliotahiniwa mwaka 1995, lakini wanafunzi 1,453 tu walichaguliwa kuingia kidato cha I katika shule za Sekondari za Serikali mbalimbali; sawa na asilimoa 5.5 tu. Hii ina maana kwamba wanafunzi ambao hawakuchaguliwa sio lazima walishindwa, walijiunga na Sekondari za binafsi au walijihusisha na shughuli zao nyingine. Njia pekee ya kuwasaidia vijana hawa ambao hawachaguliwi ni kufanya jitihada ya kujenga na kuendesha shule za sekondari za binafsi nyingi mkoani humo. Uwezo wa Serikali kuendesha shule za Sekondari ni mdogo sana. Njia pekee ya kuwasaidia

vijana wa Mkoa huu kukamilisha kiu yao ya elimu na ambao hawabahatiki kuchaguliwa siyo kwamba walishindwa mitihani bali kutokana na ufinyu wa uwezo wa serikali kuwasomesha.

i) **Wanafunzi kuacha/kukatiza Masomo**:

Tatizo la wanafunzi kukatiza masomo mkoani Iringa ni tatizo ambalo limeenea mkoani kote. Zipo sababu zilizowazi na zisizowazi zinazosababisha baadhi ya wanfunzi wa shule za msingi kuacha masomo. Sababu kubwa ni utoro. Sababu nyingine ni vifo na mimba kwa upande wa wasichana. Mwaka 1992 asilimia 92 ya kukatisha masomo ilikuwa utoro. Jedwali Na. LVIII(i) linaeleza kinaganaga ukubwa wa tatizo la wanfunzi kukatisha masomo mkoani Iringa.


**JEDWALI Na. LVIII(l): IDADI YA WANAFUNZI KIJINSIA NA KIWILAYA WALIOKATISHA MASOMO YA SHULE ZA MSINGI MKOANI IRINGA, 1990 - 1995.**

| Wilaya | 1990 | | 1991 | | 1993 | | 1995 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana |
| Iringa Vijijini | 15 | 13 | 285 | 244 | 6 | 14 | 284 | 280 |
| Iringa Mjini | 10 | 16 | 30 | 21 | 5 | 2 | 56 | 53 |
| Mufindi | 29 | 46 | 32 | 34 | 34 | 36 | 34 | 37 |
| Njombe | 100 | 102 | 67 | 83 | 93 | 73 | 290 | 273 |
| Ludewa | 45 | 37 | 28 | 32 | 29 | 34 | 47 | 42 |
| Makete | 182 | 61 | 59 | 61 | 62 | 44 | 20 | 13 |
| Jumla | 281 | 275 | 501 | 475 | 229 | 203 | 731 | 698 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu Iringa, 1996.

Jedwali Na. LVIII(l) linaonyesha kwamba wilaya za Njombe na Makete zilikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliokatisha masomo mwaka 1990, ambapo wilaya ya Iringa Vijijini ilikuwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya wanafunzi walioacha masomo mwaka 1991 na mwaka 1995. Wilaya ya Njombe ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wavulana kuacha masomo mwaka 1995. Wilaya za Iringa mjini, Mufindi na Ludewa zilikuwa na idadi ndogo za wavulana kwa wasichana waliokatisha masomo. Je, kuwepo kwa idadi kubwa ya vijana walioacha shule wilayani Njombe kunatokana na ajira za watoto hasa katika mashamba ya chai?

**Kielelezo Na. 20: Wanafunzi wa Shule za Msingi Waliokatisha Masomo Kiwilaya, Kijinisa na Sababu zake, Mkoa wa Iringa, Mwaka 1985 Na 1995**



**JEDWALI Na. LVIII(m): UKUBWA WA TATIZO LA WANAFUNZI WANAOKATISHA MASOMO KIJINSIA NA KIWILAYA - MKOA WA IRINGA 1993**

| Wilaya | Darasa la I Walioingia 1987 | | Jumla ya waliomaliza Darasa la VII, 1993 | | Asilimia ya wale waliokatisha masomo, 1993 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana |
| Iringa Vijijini | 4,714 | 4,820 | 3,447 | 3,557 | 73.1 | 26.2 |
| Iringa Mjini | 1,099 | 1,130 | 871 | 967 | 20.7 | 14.4 |
| Mufindi | 2,978 | 3,036 | 2,185 | 2,279 | 26.6 | 24.9 |
| Njombe | 4,485 | 4,462 | 3,202 | 3,560 | 28.6 | 20.2 |
| Ludewa | 1,277 | 1,287 | 1,036 | 1,073 | 18.9 | 16.6 |
| Makete | 1,602 | 1,451 | 1,162 | 1,176 | 27.5 | 18.9 |
| Jumla | 16,155 | 16,186 | 11,903 | 12,612 | 26.3 | 22.1 |

Chanzo: Ofisii ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu Iringa, 1996.

**JEDWALI Na. LVIII(n): UKUBWA WA TATIZO LA WANAFUNZI WANAOKATISHA MASOMO KIJINSIA NA KIWILAYA - MKOA WA IRINGA 1994**

| Wilaya | Darasa la I Walioingia 1988 | | Jumla ya waliomaliza Darasa la VII, 1994 | | Asilimia ya wale waliokatisha masomo, 1994 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana |
| Iringa Vijijini | 5,291 | 5,278 | 3,776 | 3,836 | 28.6 | 27.3 |
| Iringa Mjini | 1,206 | 1,171 | 907 | 963 | 24.7 | 17.8 |
| Mufindi | 3,554 | 3,298 | 2,264 | 2,345 | 36.3 | 28.9 |
| Njombe | 4,970 | 4,787 | 3,273 | 3,424 | 34.1 | 28.5 |
| Ludewa | 1,462 | 1,530 | 1,120 | 1,111 | 23.4 | 27.4 |
| Makete | 1,465 | 1,688 | 1,208 | 1,344 | 17.5 | 20.4 |
| Jumla | 17,948 | 17,754 | 12,548 | 13,023 | 30.1 | 26.3 |

Chanzo: Ofisii ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu Iringa, 1996.

**JEDWALI LVIII(P): WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI WALIOKATISHA MASOMO KIWILAYA, KIJINISA NA SABABU ZAKE, MKOA WA IRINGA, MWAKA 1985 NA 1995.**

**DARASA LA 1 - 7**

| Wilaya | Sababu | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1985 | 1995 | 1995 | 1995 | 1985 | 1995 |
| Iringa Vijijini | Utoro | | 280 | - | 241 | - | 521 |
| | Mimba | - | - | - | 39 | - | 39 |
| | Vifo | - | 4 | - | - | - | 4 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | - | - |
| Iringa Mjini | Utoro | - | 50 | - | 48 | - | 98 |
| | Mimba | - | - | - | 5 | - | 5 |
| | Vifo | - | 3 | - | - | - | 3 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | - | - |
| Mufindi | Utoro | - | 29 | - | 13 | - | 42 |
| | Mimba | - | - | - | 24 | - | 24 |
| | Vifo | - | 5 | - | - | - | 5 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | - | |
| Njombe | Utoro | - | 285 | - | 249 | - | 534 |
| | Mimba | - | - | - | 12 | - | - |
| | Vifo | - | 5 | - | - | - | 5 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | - | - |
| Ludewa | Utoro | - | 45 | - | 29 | | 74 |
| | Mimba | - | - | - | 14 | | 14 |
| | Vifo | - | 2 | - | - | | 2 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | | - |
| Makete | Utoro | | 19 | - | 11 | | 30 |
| | Mimba | - | - | - | 2 | | 2 |
| | Vifo | - | 1 | - | - | | 1 |
| | Sababu nyingine | - | - | - | - | | - |
| Jumla | | - | 728 | - | 687 | | 1,403 |

Chanzo: Ofisii ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu Iringa, 1996.

**JEDWALI LVIII (q) MATUKIO YA MIMBA YA WANAFUNZI SHULE ZA MSINGI KIWILAYA, MKOA WA IRINGA 1995.**

| | D A R A S A | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wilaya | I | II | III | IV | V | VI | VII | Jumla | % |
| Iringa Mjini | - | - | - | - | 3 | 1 | 1 | 5 | 0.06 |
| Iringa Vijijini | - | - | 1 | 1 | 4 | 18 | 15 | 39 | 0.11 |
| Mufindi | - | - | - | 1 | 2 | 4 | 17 | 24 | 0.10 |
| Njombe | - | - | 1 | - | 1 | 3 | 7 | 12 | 0.04 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ludewa | - | - | 1 | 2 | 2 | 5 | 4 | 14 | 0.13 |
| Makete | - | - | - | - | 1 | - | 1 | 2 | 0.02 |
| Jumla | - | - | 3 | 4 | 13 | 31 | 45 | 96 | 0.08 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, Takwimu za Elimu, 1970 -1995.

Inaonekana katika Jedwali Na. LVIII(q) kwamba wilaya ya Iringa Vijijini ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wasichana waliopata mimba katika shule za msingi mwaka 1995 ikifuatiwa na wilaya ya Mufindi. Mimba kwa wanafunzi wasichana ni tatizo kubwa linalosababisha wasichana wengi kukatisha masomo yao Mkoani Iringa.

**JEDWALI LVIII (r) WANAFUNZI WALIOACHA MASOMO KATIKA SHULE TISA ZA MSINGI KUTOKA BAADHI YA MIKOA, 1994.**

| Mkoa | MADARASA | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | I | II | III | IV | V | VI | VII | Jumla | Nafasi |
| IIringa | 76 | 89 | 126 | 231 | 119 | 209 | 295 | 1145 | 8 |
| Kilimanjaro | 242 | 436 | 710 | 976 | 645 | 848 | 895 | 4752 | 3 |
| Arusha | 392 | 486 | 486 | 773 | 543 | 641 | 695 | 4016 | 4 |
| Dar es Salaam | 225 | 298 | 451 | 641 | 426 | 432 | 326 | 2799 | 6 |
| Kagera | 210 | 420 | 653 | 1131 | 1052 | 1134 | 1145 | 5745 | 2 |
| Mara | 211 | 224 | 295 | 437 | 418 | 355 | 567 | 2107 | 7 |
| Mbeya | 334 | 403 | 368 | 552 | 584 | 584 | 638 | 6406 | 1 |
| Ruvuma | 88 | 60 | 91 | 138 | 108 | 241 | 243 | 969 | 9 |
| Tanga | 293 | 408 | 444 | 760 | 517 | 397 | 418 | 3237 | 5 |

Chanzo: Tume ya Mipango: Basic Education Statistics in Tanzania (BEST), 1994.

Jedwali Na. LVIII (r) linaonyesha kwamba tatizo la vijana kukatisha masomo ya msingi siyo tatizo kubwa sana mkoani Iringa ikilinganishwa na viwango vya tatizo hilo mikoa mingine. Palikuwepo wanafunzi 1,145 tu walioacha masomo Mkoani Iringa dhidi ya wanafunzi 6,406 walioacha masomo ya shule ya msingi Mkoani Mbeya, 5,745 Kagera na wanafunzi 4,752 mkoani Kilimanjaro.


**JEDWALI LVIII (s): UWIANO KATI YA VYUMBA VYA MADARASA NA IDADI YA WANAFUNZI KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Idadi ya Wanafunzi | Idadi ya Vyumba vya Madarasa | Uwiano wanafunzi kwa chumba cha Darasa |
|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 68,862 | 1,335 | 52 |
| Iringa Mjini | 17,128 | 335 | 51 |
| Mufindi | 46,337 | 911 | 51 |
| Njombe | 64,100 | 1,395 | 46 |
| Ludewa | 19,446 | 474 | 41 |
| Makete | 20,667 | 537 | 38 |
| Jumla | 236,540 | 4,987 | 47 |


Chanzo: Tume ya Mipango - Education Statistics of Iringa Region, 1970 - 1995.

Idadi ya wanafunzi inayokubalika ni 45 kwa chumba cha darasa. Wilaya za Ludewa na Makete pekee zina wanafunzi chini ya 45 kwa darasa kwa wastani. Wilaya zilizobakia zina zaidi ya wanafunzi 45 kwa kila chumba cha darasa. Kwa ufanisi zaidi wa mwalimu katika kufundisha idadi ya wanafunzi inayotakiwa ni 45 kwa chumba cha darasa. Kwa hiyo wilaya za Iringa Vijijini na Mjini, Mufindi na Njombe zinahitaji madarasa zaidi.


**Kielelezo Na. 20(a): Hali ya Majengo (Madarasa) Katika Shule za Msingi Kiwilaya Mkoa wa Iringa 1995**


2000
1800
1600
1400
1200
1000
800
600
400
200
0
Iringa(V)
Mufindi
Iringa(M)
Njombe
Ludewa
Makete
Mahitaji
Yaliyopo

**Kielelezo Na. 20(b): Hali ya Majengo (Vyoo) Katika Shule za Msingi Kiwilaya Mkoa wa Iringa 1995**




**Kielelezo Na. 20(c): Hali ya Majengo (Nyumba za Walimu) Katika Shule za Msingi Kiwilaya Mkoa wa Iringa 1995**




**JEDWALI Na. LVIII(t): HALI YA MAJENGO KATIKA SHULE ZA MSINGI KIWILAYA IRINGA 1995**

| Wilaya | Aina ya Jengo | Idadi inayohitajika | Idadi iliyopo | Upungufu uliopo | % ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Iiringa Vijijini | Madarasa | 1,800 | 1,250 | 550 | 30 |
| | Nyumba za Walimu | 1,494 | 841 | 653 | 44 |
| | Vyoo | 2,588 | 335 | 1508 | 58 |
| Iringa Mjini | Madarasa | 392 | 335 | 57 | 14.5 |
| | Nyumba za Walimu | 572 | 43 | 529 | 92 |
| | Vyoo | 631 | 346 | 317 | 45 |
| Mufindi | Madarasa | 1218 | 901 | 317 | 26 |
| | Nyumba za Walimu | 1128 | 513 | 615 | 54 |
| | Vyoo | 1744 | 332 | 1,412 | 81 |
| Njombe | Madarasa | 1732 | 1395 | 337 | 19 |
| | Nyumba za Walimu | 1704 | 1,111 | 593 | 35 |
| | Vyoo | 2564 | 2,172 | 392 | 15 |
| Ludewa | Madarasa | 564 | 443 | 121 | 21 |
| | Nyumba za Walimu | 732 | 233 | 499 | 68 |
| | Vyoo | 794 | 137 | 656 | 83 |
| Makete | Madarasa | 537 | 474 | 63 | 12 |
| | Nyumba za Walimu | 737 | 203 | 534 | 72 |
| | Vyoo | 781 | 176 | 605 | 77 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu - Takwimu za Elimu 1970 - 1995.

**Kielelezo Na. 21: Hali ya Samani (Madawati) ya Shule za Msingi Kiwilaya, Mkoani Iringa 1995.**



**JEDWALI Na. LVIII(u): HALI YA SAMANI YA SHULE ZA MSINGI KIWILAYA, MKOANI IRINGA 1995.**


| IRINGA VIJIJINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Samani** | **Mahitaji** | **Iliyopo** | **Upungufu** | **yaupungufu** |
| Samani | 22,118 | 15,056 | 7.062 | 32 |
| Meza | 3,140 | 1,368 | 1,772 | 56 |
| Viti | 3,228 | 1,319 | 1,909 | 59 |
| Kabati | 1,590 | 288 | 1,302 | 82 |
| **IRINGA MJINI** | | | | |
| Madawati | 5,943 | 4,046 | 1,897 | 32 |
| Meza | 962 | 474 | 488 | 51 |
| Viti | 991 | 528 | 463 | 47 |
| Kabati | 561 | 273 | 288 | 51 |
| **MUFINDI** | | | | |
| Madawati | 15,446 | 11,830 | 3,616 | 23 |
| Meza | 1,978 | 1.064 | 914 | 46 |
| Viti | 3,192 | 1,257 | 1,935 | 61 |
| Kabati | 1,852 | 264 | 1,588 | 86 |
| **NJOMBE** | | | | |
| Madawati | 17,974 | 15,384 | 2,590 | 14 |
| Meza | 3,437 | 1,554 | 1,883 | 55 |
| Viti | 3,829 | 1,786 | 2,043 | 53 |
| Kabati | 2,124 | 389 | 1,735 | 82 |
| LUDEWA | | | | |
| Madawati | 6.946 | 4,733 | 2,213 | 32 |
| Meza | 1,010 | 514 | 496 | 49 |
| Viti | 1,010 | 609 | 401 | 40 |
| Kabati | 475 | 122 | 353 | 74 |
| MAKETE | | | | |
| Madawati | 7,484 | 5,528 | 1,956 | 26 |
| Meza | 1,379 | 692 | 687 | 50 |
| Viti | 1,424 | 124 | 1,300 | 91 |
| Kabati | 827 | 127 | 700 | 85 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu - Takwimu za Elimu 1970 - 1995.

Jedwali Na. LVIII(t) na Jedwali Na. LVIII(u) yanaonyesha idadi ya majengo ya madarasa, nyumba za walimu, vyoo na samani za shule (madawati, meza, viti na kabati). Upo uhaba mkubwa sana wa nyumba za walimu, hali hii inaathiri sana

utendaji wao wa kazi. Tatizo lipo kwa wilaya zote. Ukosefu wa nyumba za walimu ni mkubwa zaidi wilaya ya Iringa Mjini, Makete, Ludewa, Mufindi na Iringa Vijijini. Hali kadhalika kuna hali mbaya ya upatikanaji wa samani mashuleni katika wilaya zote mkoani. Wilaya zenye uhaba mkubwa wa madawati ni Iringa Mjini, Iringa Vijijini na Ludewa. Kitu kinachowaathiri sana wanafunzi ni madawati, na ili mwanafunzi aweze kuwa na ufanisi kimasomo hana budi kuwa na dawati. Hivyo basi suala la madawati kwa shule mkoani Iringa ni la muhimu sana na lazima lipewe kipaumbele.

**Kielelezo Na. 22: Idadi ya Walimu Kiwilaya Kijinsia na Uwiano wa Walimu kwa Wanafunzi Mkoa wa Iringa, 1995.**



**JEDWALI Na. LVIII9V): IDADI YA WALIMU KIWILAYA KIJINSIA NA UWIANO WA WALIMU KWA WANAFUNZI MKOA WA IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Idadi ya Walimu wa Shule za Msingi | | | Uwiano Mwalimu kwa wanafunzi |
|---|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 815 | 889 | 1,704 | 1:40 |
| Iringa Mjini | 153 | 427 | 580 | 1:29 |
| Mufindi | 646 | 469 | 1,115 | 1:41 |
| Njombe | 980 | 775 | 1,755 | 1:36 |
| Ludewa | 458 | 175 | 633 | 1:32 |
| Makete | 446 | 197 | 643 | 1:30 |
| Jumla | 3,498 | 2,932 | 6,430 | 1:37 |

Chanzo: Tume ya Mipango, Takwimu za Elimu Mkoa wa Iringa, 1970 -1995.

Jedwali Na. LVIII(v) linaonyesha mgawanyo wa walimu wa shule za msingi kiwilaya, kijinsia na uwiano uliopo wa walimu kwa wanafunzi. Wilaya ya Mufindi ina idadi kubwa zaidi ya wanafunzi kwa walimu wakati wilaya ya Iringa Mjini ina idadi ndogo sana.

**JEDWALI Na. LVIII(w): MGAWANYO WA WALIMU KIWILAYA NA KIMADARAJA MKOA WA IRINGA, 1995.**

| | Walimu wanaohitajika | | Walimu Waliopo | | Upungufu wa Walimu | | Asilimia ya upungufu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Daraja IIIA** | **Daraja IIIB** | **Daraja IIIA** | **Daraja IIIB** | **Daraja IIIA** | **Daraja IIIB** | **Daraja IIIA** | **Daraja IIIB** |
| Iringa Vijijini | 357 | 270 | 310 | 223 | 47 | 47 | 13.2 | 17.4 |
| Iringa Mjini | 981 | 1,106 | 678 | 1,026 | 303 | 80 | 31 | 7.2 |
| Mufindi | 706 | 865 | 459 | 656 | 247 | 209 | 35 | 24.2 |
| Njombe | 1,074 | 1,178 | 819 | 944 | 255 | 234 | 23.7 | 20 |
| Ludewa | 334 | 398 | 260 | 373 | 74 | 25 | 22.1 | 6.3 |
| Makete | 358 | 369 | 202 | 441 | 156 | +72 | 43.6 | +20.1 |
| Jumla | 3,810 | 4,186 | 2,728 | 3,663 | 1,082 | 595 | 28.4 | 14.2 |

Chanzo: Tume ya Mipango, Takwimu za Elimu, Mkoa wa Iringa, 1970 - 1995.

Jedwali Na. LVIII(w) linaonyesha kwamba Mkoa wa Iringa unaupungufu wa walimu 1,082 wa Daraja IIIA na 595 wa Daraja IIIB. Wilaya ya Makete imeathirika sana na upungufu

wa walimu wa Daraja IIIA ikifuatiwa na wilaya za Mufindi na Iringa Mjini.

**JEDWALI Na. LVIII(x) HALI YA MAENDELEO YA SHULE ZA MSINGI MKOA WA IRINGA 1987 - 1995.**

| Hali halisi | 1987 | 1988 | 1989 | 1990 | 1993 | 1993 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi Ya Shule | 677 | 682 | 683 | 688 | 709 | 723 |
| Idadi ya Wanafunzi | 205,95 | 203,116 | 204,19 | 206,66 | 266,56 1 | 222,79 |
| Walimu wenye Shahada | 5,569 | 5,577 | 5,618 | 5,847 | 6,014 | 6,391 |
| Idadi ya Mikondo | 5,859 | 6,373 | 6,525 | 6,715 | 6,829 | 7,298 |
| Wastani Wanafunzi/Shule | 304 | 298 | 299 | 300 | 319 | 308 |
| Wastani Wanafunzi/Mkondo | 35 | 32 | 31 | 31 | 33 | 30 |
| Wastani Wanafunzi/Mwalimu | 34 | 36 | 36 | 35 | 38 | 35 |

Chanzo: Tume ya Mipango, Takwimu za Elimu Mkoa wa Iringa, 1970 - 1995.

### 4.1.3 Elimu ya Sekondari:

Mwaka 1967 Mkoa wa Iringa ulikuwa na shule moja tu ya Sekondari ya Serikali na tatu za binafsi. Idadi ya shule za sekondari hadi mwaka 1995 imeongezeka hadi kufikia 14 za serikali na 31 za binafsi. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 1025. Jedwali Na. LIX linaonyesha idadi ya shule za sekondari Mkoa Iringa ikilinganishwa na ya mikoa kadhaa Tanzania Bara 1995. Mkoa umepiga hatua kubwa sana lakini hailingani na wa Kilimanjaro (Jedwali Na. LIX) kwa idadi kubwa ya shule za Sekondari. Mkoa wa Iringa unazo shule za sekondari za Serikali 14 wakati Mkoa wa Kilimanjaro unazo 13, pia mkoa wa Iringa ni wa pili kwa idadi ya shule za sekondari za binafsi. Hata hivyo bado Mkoa wa Kilimanjaro unazo shule chache za sekondari za serikali.

**JEDWALI Na. LIX: SHULE ZA SEKONDARI MKOANI IRINGA BAADHI YA MIKOA YA TANZANIA BARA, 1995.**

| Mkoa | Shule za Sekondari | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Za Serikali | Za Binafsi | |
| Iringa | 14 | 31 | 45 |
| Mbeya | 7 | 17 | 24 |
| Kilimanjaro | 13 | 76 | 89 |
| Arusha | 8 | 20 | 28 |
| Kagera | 9 | 23 | 32 |
| Mwanza | 10 | 14 | 24 |
| Dodoma | 9 | 6 | 15 |
| Kigoma | 4 | 3 | 7 |
| Morogoro | 12 | 8 | 20 |
| Mtwara | 9 | 3 | 12 |
| Rukwa | 11 | 9 | 20 |
| Singida | 4 | 4 | 8 |
| Tabora | 5 | 10 | 15 |
| Mara | 8 | 10 | 18 |


Chanzo: Tume ya Mipango, Takwimu za Elimu, 1996.

**JEDWALI Na. LIX(a): MGAWANYO WA SHULE ZA SEKONDARI KIWILAYA MKOA WA IRINGA 1967, 1985 NA 1995.**

| Wilaya | 1967 | | | 1985 | | | 1995 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikal | Binafsi | Jumla |
| Iringa Vijijini | - | 1 | 1 | 2 | - | 2 | 3 | 4 | 7 |
| Iringa Mjini | - | 2 | 2 | 3 | 3 | 6 | 3 | 4 | 7 |
| Mufindi | 1 | - | - | 1 | 5 | 6 | 2 | 12 | 14 |
| Njombe | - | - | - | 1 | 7 | 8 | 3 | 8 | 11 |
| Ludewa | - | - | - | - | 1 | 1 | 2 | - | 2 |
| Makete | - | - | - | - | 1 | 1 | 1 | 3 | 4 |
| Jumla | 1 | 3 | 4 | 4 | 17 | 24 | 14 | 31 | 45 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu (Takwimu za Elimu 1970 - 1995) Iringa.

**Kielelezo Na. 23: Idadi ya Wanafunzi Katika Shule za Sekondari za Serikali na Binafsi Kijinsia 1990 - 1995 Mkoa wa Iringa**




**JEDWALI Na. LIX(b): IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI NA BINAFSI KIJINSIA 1990 - 1995 MKOA WA IRINGA.**

| | Shule za Serikali | | | Shule Binafsi | | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Jumla** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Jumla** | **Wavulana** | **Wasichana** |
| 1990 | 3.156 | 1,502 | 4,658 | 4,072 | 3,244 | 7,316 | 7,228 | 4,746 |
| 1991 | 3,597 | 1,669 | 5,266 | 4,763 | 3,720 | 8,483 | 8,360 | 5,389 |
| 1992 | 3,156 | 1,502 | 4,658 | 4,072 | 3,244 | 7,316 | 7,228 | 4,746 |
| 1993 | 4,422 | 2,212 | 6,634 | 4,575 | 3,940 | 8,515 | 8,997 | 6,152 |
| 1994 | 4,052 | 2,734 | 6,786 | 4,429 | 3,491 | 7,920 | 8,481 | 6,225 |
| 1995 | 4,459 | 2,578 | 7,037 | 3,367 | 3,822 | 7,189 | 7,826 | 6,400 |
| Jumla | 29,595 | 12,197 | 35,039 | 29,350 | 21,461 | 47=6,739 | 63,708 | 33,658 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu (Takwimu za Elimu) 1970 - 1995, Iringa.

Idadi kubwa ya wanafunzi katika shule za Sekondari Mkoani Iringa ni katika shule za binafsi, vile vile idadi kubwa zaidi ya wavulana wanasoma shule za sekondari kuliko wasichana (Jedwali LIX(b).

### 4.1.4 Elimu ya Watu Wazima:

Maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi yeyote hutegemea maendeleo ya elimu ya taifa hilo. Inavyoeleweka hapa nchini Tanzania elimu maana yake ni kujua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili. Tangu nchi hii ipate Uhuru (1961) juhudi kubwa imefanywa kutokomeza ujinga kwa kupanua elimu ya msingi na Sekondari, vile vile mkazo uliwekwa wa kuendesha kisomo cha watu wazima. Miaka ya 1970 shule za msingi zilitumika kama vituo vya elimu hii ya watu wazima na walimu wakuu wa shule hizo waliwajibika na uendeshaji wa kampeni ya elimu hiyo kwa maeneo karibu na shule.

**JEDWALI Na. LX: VIWANGO VYA ELIMU YA WATU WAZIMA WENYE UMRI KATI YA MIAKA 19 NA KUENDELEA KULINGANA NA TAARIFA ZA SENSA YA WATU ZA 1967, 1978 NA 1988.**

| Mkoa | Sensa ya 1967 | Sensa ya 1978 | Sensa ya 1988 % |
|---|---|---|---|
| **Iringa** | **31** | **54.0** | **68.3** |
| Kilimanjaro | 56 | 74.1 | 80.8 |
| Dar es Salaam | 60 | 73.3 | 80.7 |
| Ruvuma | 41 | 66.3 | 70.5 |
| Tanga | 40 | 60.6 | 66.0 |
| Morogoro | 37 | 58.6 | 62.8 |
| Mara | 35 | 56/4 | 63.9 |
| Kagera | 40 | 52.9 | 59.5 |
| Mtwara | 28 | 51.4 | 57.1 |
| Dodoma | 24 | 49.5 | 55.5 |
| Mbeya | 29 | 49.2 | 61.9 |
| Rukwa | - | 48.5 | 58.6 |
| Lindi | - | 48.4 | 53.8 |
| Singida | 24 | 46.7 | 57.4 |
| Mwanza | 25 | 44.3 | 57.3 |
| Pwani | 26 | 44.0 | 51.1 |
| Kigoma | 19 | 43.7 | 55.1 |
| Arusha | 26 | 41.9 | 58.1 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tabora | 27 | 40.5 | 50.5 |
| Shinyanga | 16 | 33.2 | 48.4 |

Chanzo: Tume ya Mipango: Sensa za 1967, 1978 na 1988.

**JEDWALI LX(a): VIWANGO VYA ELIMU YA WATU WAZIMA VIJIJINI NA MJINI WENYE UMRI WA MIAKA 10 NA ZAIDI, SENSA YA 1988, TANZANIA BARA (%).**

| | Wanaume | | | Wanawake | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mikoa** | **Vijijini** | **Mjini** | **Jumla** | **Vijijini** | **Mjini** | **Jumla** |
| **Iringa** | **80.1** | **87.4** | **84.9** | **57.2** | **70.4** | **58.5** |
| Mara | 73.7 | 88.0 | 75.3 | 53.7 | 71.5 | 55.6 |
| Dodoma | 61.5 | 85.4 | 64.3 | 45.1 | 73.7 | 48.2 |
| Arusha | 61.5 | 91.8 | 65.6 | 46.4 | 82.8 | 50.9 |
| Kilimajaro | 84.5 | 90.3 | 85.5 | 75.7 | 83.6 | 76.9 |
| Tanga | 72.8 | 88.6 | 75.9 | 53.2 | 75.6 | 57.3 |
| Morogoro | 68.8 | 86.4 | 72.9 | 49.5 | 72.0 | 54.6 |
| Pwani | 60.1 | 72.2 | 64.0 | 40.1 | 51.8 | 44.9 |
| Dar es Salaam | 68.4 | 90.0 | 87.9 | 48.0 | 77.7 | 74.6 |
| Lindi | 62.4 | 75.9 | 64.6 | 42.0 | 60.2 | 44.8 |
| Mtwara | 65.5 | 77.9 | 67.3 | 46.3 | 61.6 | 48.5 |
| Ruvuma | 77.7 | 87.6 | 78.7 | 61.4 | 75.7 | 63.3 |
| Mbeya | 69.9 | 87.5 | 73.3 | 48.4 | 70.0 | 52.4 |
| Singida | 65.0 | 85.5 | 66.8 | 47.2 | 70.8 | 49.3 |
| Tabora | 50.1 | 85.2 | 60.5 | 36.7 | 67.8 | 41.6 |
| Rukwa | 69.1 | 84.3 | 71.3 | 43.9 | 66 | 47.3 |
| Kigoma | 65.1 | 83.1 | 67.4 | 43.1 | 62.7 | 45.5 |
| Shinyanga | 57.9 | 85.9 | 59.9 | 36.2 | 67.7 | 39.3 |
| Kagera | 63.7 | 83.7 | 67.6 | 43.4 | 66.9 | 47.8 |
| Mwanza | 63.7 | 83.7 | 67.6 | 43.4 | 66.9 | 47.8 |

Chanzo: Tume ya Mipango; Sensa za 1967, 1978 na 1988.

Jedwali Na. LX linalinganisha kiwango cha elimu ya watu wazima kilichofikiwa na Mkoa wa Iringa ambacho ni asilimia 68.3 mwaka 1988. Kiwango hiki kinalinganishwa na vile viwango vya mikoa mingine. Jedwali Na. LX(a) linaonyesha jinsi Viwango vya elimu ya watu wazima wanawake vilivyo chini nchini kote, mijini na vijijini. Viwango hivyo vimeonyeshwa kimkoa.

**JEDWALI Na. LX(b): IDADI YA WATU WAZIMA WANAOJUA KUSOMA NA KUANDIKA KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| | Idadi ya Watu Wazima | | | Idadi wanaojua kusoma na kuandika | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
| Iringa Vijijini | 69,451 | 88,826 | 158,277 | 53,800 | 60,489 | 114,289 |
| Iringa Mjini | 36,839 | 37,867 | 74,706 | 35,091 | 34,538 | 69,629 |
| Mufindi | 63,348 | 67,544 | 130,892 | 55,031 | 51,289 | 106,320 |
| Njombe | 64,536 | 82,849 | 147,38 | 57,944 | 67,520 | 125,464 |
| Ludewa | 34,738 | 40,872 | 75,610 | 29,559 | 32,539 | 62,148 |
| Makete | 22,561 | 32,211 | 55,772 | 18,676 | 22,141 | 40,817 |
| Jumla | 291,473 | 351,169 | 642,642 | 250,101 | 268,516 | 518,617 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, (Takwimu za Elimu, 1970 - 1995) Iringa.

**JEDWALI Na.a LX(c): IDADI YA WATU WAZIMA WASIOJUA KUSOMA NA KUANDIKA KIWILAYA MWAKA 1985 NA 1995 MKOA WA IRINGA.**

| | Idadi ya Watu Wazima - 1985 | | | Idadi ya Watu Wazima - 1995 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
| Iringa Vijijini | 12,868 | 30,337 | 43,205 | 10,590 | 18,547 | 29,131 |
| Iringa Mjini | 519 | 2,036 | 2,555 | 1,558 | 2,811 | 4,369 |
| Mufindi | 8,993 | 17,881 | 24,874 | 8,317 | 16,255 | 24,572 |
| Njombe | 5,790 | 17,925 | 23,715 | 5,025 | 10,996 | 16,025 |
| Ludewa | 2,014 | 6,045 | 8,059 | 4,373 | 6,424 | 10,797 |
| Makete | 2,859 | 10,977 | 13,836 | 3,786 | 7,381 | 11,069 |
| Jumla | 31,043 | 85,201 | 116,244 | 33,653 | 62,408 | 96,061 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu (Takwimu za Eliimu 1970 - 1995), Iringa.

**JEDWALI LX(d) WATU WASIOJUA KUSOMA NA KUANDIKA WA MIAKA 10 HADI 65 NA ZAIDI MWAKA 1995, MKOANI IRINGA.**

| Kundi la Umri | Jinsia | Iringa Mjini | Iringa Vijijini | Ludewa | Makete | Mufindi | Njombe |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10-14 | Wanaume | 68 | 281 | 307 | 5 | 48 | 154 |
| | Wanawake | 111 | 352 | 529 | 17 | 164 | 420 |
| 15-29 | Wanaume | 120 | 1,854 | 390 | 269 | 1411 | 192 |
| | Wanawake | 436 | 3,665 | 1,047 | 872 | 2,860 | 3,422 |
| 30 - 44 | Wanaume | 210 | 286 | 347 | 1141 | 2263 | 3432 |
| | Wanawake | 538 | 6484 | 1117 | 2875 | 4265 | 3422 |
| 45 - 54 | Wanaume | 225 | 1604 | 371 | 427 | 1179 | 2341 |
| | Wanawake | 326 | 3208 | 896 | 1212 | 2122 | 4657 |
| 55-65+ | Wanaume | 38 | 1837 | 824 | 646 | 984 | 1354 |
| | Wanawake | 61 | 2917 | 1309 | 1545 | 1696 | 2773 |
| Jumla | Wanaume | 661 | 8422 | 2239 | 2488 | 5,905 | 5,973 |
| | Wanawake | 2019 | 10,626 | 4,898 | 6521 | 11,107 | 14,694 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | | 2,680 | 19,048 | 7,137 | 9,009 | 17,012 | 20,667 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Elimu, (Takwimu za Elimu 1970 - 1995), Iringa.

Jedwali Na. LX linaonyesha wilaya ya Ludewa ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wasiojua kusoma na kuandika wenye umri wa miaka 10-14; ambapo Wilaya ya Iringa Vijijini ilikuwa na watu wengi zaidi wasiojua kusoma na kuandika wenye miaka 15-29 na miaka 30-44. Wilaya ya Njombe ilikuwa na watu wengi zaidi wa kundi la umri wa miaka 45-54 wasiojua kusoma na kuandika wilaya za Iringa Vijijini na Njombe vile vile zilikuwa zinaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu wa umri kati ya miaka 55-65 na zaidi wasiojua kusoma ka kuandika. Kwa ujumla wilaya ya Njombe iliongoza kwa idadi kubwa ya watu wasiojua kusoma na kuandika mwaka 1995 na kufuatiwa na wilaya ya Iringa vijijini. Wilaya ya Iringa Mjini ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya wilaya zote Mkoani Iringa.

### 4.1.5 Elimu ya Ufundi:

Vipo vyuo vitatu tu vya ufundi mkoani Iringa, viwili vipo Iringa Mjini: Iringa Vacational Training Centre na Don Bosco Vocational Training Centre. Kilichobakia kiko wilaya ya Mufindi ina chuo kimoja ambacho kinajulikana kwa jila la Mufindi Lutheran Vocational Training Centre.

## 4.2 Sekta ya Afya:

Kama ilivyo katika mikoa mingine nchini huduma za afya zilizopo vijijini Mkoa wa Iringa zina hali ya kuchakaa na hazina dawa. Magonjwa makuu ambayo mara kwa mara husababisha vifo mkoani ni malaria, kuharisha, homa ya tumbo,

kifua kikuu, surua, upungufu wa damu, ukimwi na kichomi. Jedwali lifuatalo linaonyesha kukua kwa huduma za afya mkoani Iringa.

**JEDWALI LXI: KUKUA NA MGAWANYO WA HUDUMA ZA AFYA 1961 - 1995.**

| Wilaya | Hospitali | | | Zahanati | | | Vituo vya Afya | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1961 | 1981 | 1995 | 1961 | 1981 | 1995 | 1961 | 1981 | 1995 |
| Iringa Vijijini | - | 1 | 1 | - | 29 | 53 | - | 4 | 4 |
| Iringa Mjini | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 3 | - | - | 1 |
| Mufindi | 1 | 1 | 3 | 3 | 21 | 45 | 1 | 3 | 5 |
| Njombe | 1 | 3 | 3 | 3 | 25 | 33 | 1 | 1 | 3 |
| Ludewa | - | 3 | 3 | - | 11 | 31 | - | 3 | 3 |
| Makete | - | 2 | 3 | 1 | 11 | 21 | - | 2 | 3 |
| Jumla | 3 | 11 | 15 | 8 | 99 | 185 | 2 | 13 | 19 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Afya, Iringa 1994.

**JEDWALI LXII: IDADI YA HOSPITALI, VITUO VYA AFYA, NA ZAHANATI ZA SERIKALI NA BINAFSI MKOA WA IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Hospitali | | Zahanati | | Vituo vya Afya | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Serikali | Binafsi | Serikali | Binafsi |
| Iringa Vijijini | - | 1 | 37 | 16 | 4 | - |
| Iringa Mjini | 1 | 1 | 3 | - | 1 | - |
| Mufindi | 1 | 2 | 40 | 5 | 5 | - |
| Njombe | 1 | 2 | 26 | 7 | 3 | - |
| Ludewa | 1 | 2 | 25 | 6 | 3 | - |
| Makete | - | 2 | 21 | - | 3 | - |
| Jumla | 5 | 10 | 152 | 34 | 19 | |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Afya, Iringa, 1995

**JEDWALI Na. LXIII: MAGONJWA KUMI YANAYOONGOZA KATIKA KUATHIRI AFYA YA JAMII MKOANI IRINGA, 1995**

| Jina la Ugonjwa | Idadi ya Wati walioadhiriwa |
|---|---|
| Malaria | 40,750 |
| Kuharisha | 15,953 |
| Dondakoo (URTI) | 13,956 |
| Magonjwa ya Mdomoni | 9.861 |
| Magonjwa, yennye hali ya kupasuliwa | 7,523 |
| Magonjwa mengine | 9,795 |
| Magonjwa yasiyofahamika | 134,750 |
| Magonjwa ya macho | 7,411 |
| Kichomi | 6,717 |
| Magonjwa ya ngozi | 5,374 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Afya, Iringa, 1995.

Jedwali Na. LXIII linaonyesha kwamba watu wengi mkoani Iringa walipatwa na malaria mwaka 1995. Ugonjwa wa kuhara pia uliathiri afya ya jamii kwa kiwango kikubwa kwa jumla ya watu 15,953.

### 4.2.1 Zahanati:

Ngazi ya kitaifa zahanati inatarajiwa kuhudumia watu wasiozidi 10,000. Zipo zahanati 205 mkoani Iringa kila moja kwa wastani inahudumia watu 8,187 (matarajio ya idadi ya watu 1995). Kutokana na Jedwali Na. LXIV zahanati mkoani Iringa zinahudumia watu wachache kuliko kiwango cha kitaifa. Mgawanyo wa zahanati kiwilaya mkoani umeonyeshwa kwenye Jedwali Na. LXIV.

**JEDWALI Na. LXIV: MGAWANYO WA ZAHANATI KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995**

| Wilaya | Zahanati | | Jumla ya Zahanati | Idadi ya Watu 1995 | Watu kwa Zahanati |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | | | |
| Iringa Vijijini | 37 | 16 | 53 | 500,577 | 9,445 |
| Iringa Mjini | 21 | 2 | 23 | 143,911 | 6,257 |
| Mufindi | 28 | 5 | 33 | 319,481 | 9,681 |
| Njombe | 26 | 19 | 45 | 440,121 | 8,780 |
| Ludewa | 25 | 5 | 30 | 138,853 | 4,628 |
| Makete | 21 | - | 21 | 135,357 | 6,445 |
| Jumla | 158 | 47 | 205 | 1,678,302 | 8,187 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Afya, 1995.

### 4.2.2 Vituo vya Afya:

Kulingana na kituo cha Afya kinatarajiwa kuhudumia wagonjwa 50,000 kiwango kilichowekwa kitaifa. Hadi mwaka 1995 kulikuwepo na Vituo vya Afya 19 Mkoani Iringa.

Jedwali LXV Na. linaonyesha mgawanyo wa vituo vya afya mkoani kiwilaya.

**JEDWALI Na. LXV: IDADI YA VITUO VYA AFYA NA MGAWANYO WAKE KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Vituo vya Afya | | | Idadi ya Watu kwa Kituo 1995 | Idadi ya Vitanda | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Juml | | Serikali | Bina | Juml |
| Iringa Vijijini | 4 | 2 | 6 | 83,430 | - | - | - |
| Iringa Mjini | 1 | - | 1 | 143,911 | - | - | - |
| Mufindi | 3 | - | 3 | 106,494 | - | - | - |
| Njombe | 3 | - | 3 | 146,707 | - | - | - |
| Ludewa | 3 | - | 3 | 46,284 | 49 | - | 49 |
| Makete | 3 | - | 3 | 45,119 | 45 | - | 45 |
| Jumla | 17 | 2 | 19 | 88,332 | 94 | - | 94 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Afya Iringa, 1995.

Idadi ya watu kwa kila kituo cha Afya ikilinganishwa na kiwango cha kitaifa cha watu 50,000 kwa kituo, Mkoa wa Iringa una wastani wa watu 88,332 kwa kituo. Kiwango hiki ni cha juu kwa asilimia 77. Kwa hiyo Mkoa wa Iringa unahitaji kuongeza huduma hii. Wilaya ya Njombe imeathirika zaidi kwa kuwa na idadi kubwa zaidi kwa kila kituo kuliko wilaya zote mkoani. Wilayani Ludewa na Makete kila kituo cha Afya kinahudumia watu chini ya kiwango cha kitaifa cha watu 50,000. Wakati huo huo kitaifa kwa maendeleo ya Wizara ya Afya kituo kimoja cha Afya kinatakiwa kusimamia zahanati za serikali zisizozidi 5. Lakini vituo hivi mkoani Iringa vinasimamia zahanati 9, hali hii inaendelea kuthibitisha umuhimu wa kuongezwa kwa idadi ya vituo vya Afya Mkoani Iringa.

### 4.2.3 Huduma za Hospitali:

Hadi mwisho wa mwaka 1995 mkoa wa Iringa ulikuwa na hospitali 17 zenye vitanda 1746. Hospitali 5 kati ya hizi ni za

serikali na 12 ni za binafsi. Jedwali Na. LXVI linaonyesha mgawanyo wa hospitali kiwilaya mkoani Iringa.

**JEDWALI Na. LXVI: MGAWANYO WA HOSPITALI NA MADAKTARI KIWILAYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Idadi ya Hospitali | | | Vitanda | Watu kwa Kitanda | Idadi ya Madaktari | Watu kwa Daktari | Wakwa kila Hospitali |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | - | 1 | 1 | 163 | 3071 | 2 | 250,289 | 500,579 |
| Iringa Mjini | 1 | 1 | 2 | 366 | 393 | 16 | 8,994 | 71,955 |
| Mufindi | 1 | 3 | 4 | 238 | 1,342 | 3 | 106,494 | 79,870 |
| Njombe | 1 | 3 | 4 | 314 | 1402 | 3 | 146,707 | 110,030 |
| Ludewa | 1 | 2 | 3 | 361 | 385 | 1 | 138,853 | 46,284 |
| Makete | 1 | 2 | 3 | 304 | 445 | 1 | 135,357 | 45,119 |
| Jumla | 5 | 12 | 17 | 1746 | 961 | 26 | 64,550 | 98,724 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ta Afya, Iringa 1995.

Tatizo kubwa linajitokeza katika Jedwali LXVI ni uwiano uliopo kati ya idadi ya madaktari na idadi ya watu wanaohudumiwa. Wastani wa kiwango cha kitaifa kilichopo sasa ni cha daktari 1 kwa watu 24,930. Wilaya zote mkoani Iringa, isipokuwa wilaya ya Iringa Mjini, daktari mmoja anahudumia watu wasiopungua 100,000 kwa mwaka. Kiwango hiki ni kikubwa sana kwa ufanisi wa daktari. Kwa hiyo mkoa unahitaji madaktari zaidi. Tofauti na kiwango cha daktari kwa watu anaohudumia idadi ya watu kwa kila hospitali kiko chini ya lengo la kitaifa la watu 100,000 kwa kila hospitali. Wilayani Iringa Vijijini na Njombe kila hospitali unahudumia zaidi ya wastani ya watu 100,000 kwa mfano hospitali Iringa Vijijini inahudumia watu 500,579 na zile za wilayani Njombe watu 110,030. Wilaya zilizobaki zinahudumia chini ya kiwango cha kitaifa. Kwa mantiki hii, wilaya za Iringa Vijijini na Njombe zinahitaji hospitali zaidi, tena haraka sana na hasa kwa Iringa Vijijini. Jedwali lifuatalo linaonyesha mahitaji na idadi ya watalaam wa afya waliopo Mkoani Iringa mwaka 1995.

**JEDWALI LXVII: MAHITAJI YA WATAALAM WA AFYA MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wataalam | Mahitaji | Waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Waganga | 14 | 10 | 4 |
| Waganga Wafawidhi | 15 | 12 | 3 |
| Waganga Wasaidizi (Tabibu) | | 51 | |
| Maafisa Wauguzi | 70 | 63 | 7 |
| Wauguzi Wakunga | 171 | 166 | 5 |
| Waganga Wasaidizi Vijijini | | 11 | |
| Wahudumu wa Kinamama na Watoto | | 22 | |
| Wahudumu Wasaidizi wa Maabara | 43 | 40 | 3 |
| Wafamasia | | 1 | |
| Wataalam wa Maabara | | 6 | |
| Wataalam wa Mionzi | | 5 | |
| Waganga wa Meno | | 1 | |
| Wataalam wa Meno | | 9 | |
| Maafisa Afya | | 9 | |

Chanzo: Mganga Mkuu wa Mkoa, Iringa 1996.

## 4.2.4 Matarajio ya Umri wa Kuishi:

Sensa za Idadi ya Watu za 1978 na 1988 zinaonyesha matarajio ya umri wa kuishi kwa wakazi wa Mkoa wa Iringa ni miaka 50. Jedwali Na. LXVIII linaonyesha matarajio ya umri wa kuishi kimkoa, Tanzania Bara.

**JEDWALI LXVIII: MATARAJIO YA UMRI WA KUISHI, KIJINSIA NA KIMKOA TANZANIA BARA MWAKA 1978 NA 1988.**

| Mkoa | Sensa ya 1978 | | Sensa ya 1988 | |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Wanaune | Wanawake |
| Iringa | 41 | 45 | 44 | 47 |
| Arusha | 50 | 57 | 57 | 58 |
| Pwani | 47 | 48 | 46 | 51 |
| Dar es Salaam | 50 | 50 | 50 | 50 |
| Dodoma | 45 | 46 | 45 | 47 |
| Kagera | 45 | 45 | 44 | 45 |
| Kigoma | 40 | 48 | 47 | 49 |
| Kilimanjaro | 58 | 59 | 57 | 62 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Lindi | 42 | 47 | 46 | 48 |
| Mara | 44 | 47 | 46 | 48 |
| Mbeya | 41 | 47 | 45 | 48 |
| Morogoro | 44 | 46 | 45 | 48 |
| Mtwara | 40 | 46 | 45 | 48 |
| Mwanza | 44 | 48 | 46 | 50 |
| Rukwa | 40 | 45 | 44 | 48 |
| Ruvuma | 43 | 49 | 48 | 51 |
| Shinyanga | 42 | 50 | 48 | 51 |
| Singida | 44 | 55 | 54 | 55 |
| Tabora | 44 | 53 | 53 | 54 |
| Tanga | 49 | 49 | 48 | 51 |
| Jumla | 44 | 50 | 49 | 51 |

Chanzo: Takwimu za Afya, 1994.

JedwaliLXVIII linalinganisha matarajio ya umri wa kuishi katika Mikoa ya Tanzania Bara. Wakazi wa mkoa wa Iringa wanaishi miaka karibu 48 tu na wale wa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Singida na Tabora wanaishi zaidi ya miaka 48 (Sensa ya Idadi ya Watu 1978 na 1988). Takwimu za matarajio ya kuishi ya wakazi wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora na Singida zinakubaliana na za vifo vichache vya watoto wachanga na wa chini ya miaka 5 katika mikoa hiyo (Jedwali Na. LXIX).

### 4.2.5 Vifo vya Watoto wachanga na Watoto chini ya Umri wa miaka Mitano:

Ingawa Mkoa wa Iringa ni maarufu kwa kilimo cha mahindi, vifo vingi mkoani humo husababishwa na umaskini, magonjwa na lishe duni (utapiamlo). Viwango vya vifo na utapiamlo hupatikana kwa wingi kati ya wakinamama na watoto. Kabla ya utekelezaji wa mpango wa Uhai wa Mama na Mtoto mwaka 1992 kiwango cha utapia mlo mkali kilikuwa zaidi ya asilimia 1.3 na hatimaye kiwango hicho kilishuka hadi kufikia

asilimia 1.1 mwaka 1994. Mwaka 1988 kiwango cha vifo vya watoto wadogo kilikuwa 130/1000 ambapo kitaifa kilikuwa 115/1000.

Jedwali Na. LXIX linaonyesha kuwepo kwa viwango vya juu vya vifo kati ya watoto wachanga na wale wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Iringa mwaka 1975, 1985 na 1995. Hata hivyo vifo vya watoto wachanga vimekuwa vikipungua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano vifo vilipungua kutoka 152/1000 mwaka 1975 hadi vifo 111/1000 mwaka 1995. Vile vile vifo vya watoto chini ya miaka 5 navyo vilishuka kutoka 257/1000 mwaka 1975 hadi vifo 187/1000 mwaka 1995. Majedwali Na. LXX na Na. LXXI yanaonyesha hali ya utapiamlo mkali na ule wa kawaida katika mikao iliyokuwa chini ya mpango wa Uhai wa Mama na Mtoto mwaka 1990 - 1994.

**JEDWALI LXIX: VIWANGO VYA VIFO VYA WATOTO WACHANGA NA WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO MIKOANI, TANZANIA BARA, 1995.**

| Mkoa | IMR | | | U5MR | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1975 | 1985 | 1995 | 1975 | 1985 | 1995 |
| Iringa | 152 | 130 | 111 | 257 | 220 | 187 |
| Pwani | 121 | 113 | 105 | 204 | 189 | 174 |
| Dar es Salaam | 108 | 105 | 102 | 179 | 173 | 168 |
| Dodoma | 133 | 132 | 130 | 25 | 222 | 220 |
| Arusha | 108 | 75 | 52 | 179 | 119 | 78 |
| Kagera | 133 | 130 | 127 | 225 | 219 | 212 |
| Kigoma | 163 | 115 | 81 | 269 | 192 | 137 |
| Kilimanjaro | 76 | 67 | 59 | 119 | 104 | 90 |
| Lindi | 151 | 140 | 129 | 255 | 236 | 218 |
| Mara | 140 | 125 | 112 | 236 | 211 | 189 |
| Mbeya | 161 | 124 | 96 | 267 | 209 | 163 |
| Morogoro | 140 | 125 | 112 | 236 | 211 | 189 |
| Mtwara | 161 | 138 | 119 | 267 | 233 | 202 |
| Mwanza | 139 | 115 | 95 | 233 | 192 | 157 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Rukwa | 170 | 131 | 101 | 283 | 221 | 172 |
| Ruvuma | 145 | 113 | 88 | 245 | 168 | 143 |
| Shinyanga | 150 | 110 | 81 | 252 | 283 | 131 |
| Singida | 137 | 96 | 67 | 231 | 157 | 106 |
| Tabora | 140 | 101 | 73 | 236 | 166 | 116 |
| Tanga | 112 | 106 | 100 | 187 | 176 | 166 |

Chanzo: Takwimu za Wizara ya Afya, 1996.

**JEDWALI LXX: HALI YA UTAPIAMLO MKALI (5) KATIKA MIKOA ILIYOKUWA CHINI YA MAPNGO WA UHAI WA MAMA NA MTOTO MWAKA 1990 - 1994.**

| Mkoa | Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **1990** | **1991** | **1992** | **1993** | **1994** |
| Pwani | - | - | - | 7.1 | 4.4 |
| Iringa | 1.7 | 1.4 | 1.3 | 1.1 | 1.1 |
| Kagera | 2.0 | 2.1 | 1.6 | 1.2 | 2.1 |
| Kilimanjaro | 0.6 | 0.4 | 0.3 | 0.2 | 0.2 |
| Mara | 6.9 | 3.0 | 2.8 | 1.6 | 1.4 |
| Morogoro | 3.2 | 3.3 | 2.2 | 1.6 | 1.4 |
| Mtwara | 6.3 | 5.5 | 1.8 | 1.9 | 2.0 |
| Mwanza | - | - | - | 3.2 | 2.3 |
| Ruvuma | 3.9 | 3.7 | 2.3 | 1.6 | 1.5 |
| Shinyanga | 2.0 | 1.4 | 1.5 | 1.1 | 1.1 |
| Singida | 3.5 | 1.8 | 1.5 | 1.5 | 1.6 |
| Jumla | 2.8 | 2.5 | 1.6 | 1.6 | 1.4 |

Chanzo: Takwimu za Wizara ya Afya, 1996.

**JEDWALI LXXI: HALI YA UTAPIAMLO WA KAWAIDA (%) KATIKA MIKOA ILIYOKUWA CHINI YA MPANGO WA UHAI WA MAMA NA MTOTO MWAKA 1990 - 1994.**

| Mkoa | Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1990 | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 |
| Pwani | - | - | - | 46.5 | 42.5 |
| Iringa | 38.8 | 34.0 | 32.8 | 33.0 | 34.8 |
| Kagera | 29.5 | 33.6 | 29.3 | 27.1 | 25.0 |
| Kilimanjaro | 15.4 | 13.2 | 12.5 | 12.1 | 12.8 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mara | 32.2 | 27.0 | 23.1 | 20.0 | 18.2 |
| Morogoro | 38.6 | 36.5 | 35.8 | 31.8 | 30.4 |
| Mtwara | 43.4 | 41.4 | 35.5 | 35.8 | 37.1 |
| Mwanza | - | - | - | 30.4 | 32.0 |
| Ruvuma | 39.5 | 34.4 | 29.3 | 30.4 | 32.0 |
| Shinyanga | 27.2 | 26.8 | 29.4 | 31.0 | 30.1 |
| Singida | 34.6 | 31.5 | 33.6 | 30.0 | 29.6 |
| Jumla | 34.0 | 33.3 | 30.6 | 28.9 | 28.3 |

Chanzo: Takwimu za Wizara ya Afya, 1996.

Jedwali Na. LXXI linaonyesha kuwepo kwa viwango vya juu sana vya utapiamlo wa kawaida mkoani Iringa kushinda mikoa iliyolinganishwa nayo isipokuwa Mikoa ya Mtwara na Pwani. Hata hivyo mikoa ya Iringa na Shinyanga iliweza kupunguza kwa asilimia 35 na 45 kwa kufuatana na utapiamlo wa kawaida. Mkoa wa Iringa ulipunguza kutoka asilimia 1.7 hadi 1.1 na mkoa wa Shinyanga kutoka asilimoa 2.0 hadi 1.1 mwaka 1997. Mikoa ya Mara na Mtwara ilikuwa na viwango vya juu sana vya utapiamlo mkali mwaka 1990. Mkoa wa Pwani uliongoza kwa kuwa na asilimia 4.4 ya utapiamlo mkali mwaka 1994.

### 4.2.6 Viwango vya Vifo vya Akina mama Wajawazito:

Tafasiri ya vifo vya akina Mama wajawazito ni vifo vya wanawake wakiwa na mimba au kifo cha wanawake hao kinachotokea kabla ya siku 42 baada ya kujifungua. Hili ni tatizo kubwa lililoenea mikoa yote Tanzania Bara. Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa mitatu inayoongoza kwa idadi kubwa ya vifo hivyo vya akinamama (Mbeya 436, Iringa 276 na Mwanza 266). Jedwali Na. LXXII linalinganisha viwango vya vifo vya akinamama nchini miaka 1992, 1993 na 1994. Kimkoa kulingana na Jedwali Na. LXXII mkoa wa Iringa ulikuwa na kiwango cha juu sana mwaka 1992 kupita mikoa

yote Bara, wakati mwaka 1993 mkoa huo ulikuwa wa tatu baada ya Dar es Salaam, Mbeya na Kagera. Mwaka 1994 Mkoa wa Iringa ulikuwa wa pili baada ya Mkoa wa Mbeya ambao ulikuwa na kiwango cha vifo kwa kila watoto 100,000 wazima waliozaliwa.

**JEDWALI Na. LXXII: VIWANGO VYA VIFO VYA AKINA MAMA WAJAWAZITO TANZANIA BARA KWA MIKOA 1992, 1993 NA 1994.**

| **Mkoa** | **Viwango vya Vifo vya Akinamama** | | |
|---|---|---|---|
| | 1992 | 1993 | 1994 |
| **Iringa** | **311** | **321** | **276** |
| Arusha | 102 | 158 | 114 |
| Pwani | 209 | 111 | 70 |
| Dar es Salaam | 220 | 398 | 237 |
| Dodoma | 197 | 214 | 208 |
| Kagera | 304 | 343 | 190 |
| Kigoma | 144 | 155 | 105 |
| Kilimanjaro | 126 | 46 | 107 |
| Lindi | 262 | 289 | 193 |
| Mara | 67 | 59 | 106 |
| Mbeya | 67 | 361 | 436 |
| Morogoro | 289 | 172 | 190 |
| Mtwara | 264 | 212 | 161 |
| Mwanza | 221 | 186 | 266 |
| Rukwa | 172 | 294 | 243 |
| Ruvuma | 225 | 189 | 186 |
| Shinyanga | 143 | 188 | 199 |
| Singida | 242 | 171 | 239 |
| Tabora | 151 | 185 | 130 |
| Tanga | 255 | 172 | 220 |

Chanzo: Takwimu za Wizara ya Afya, 1996.

### 4.2.7 Utapiamlo:

Sababu kubwa ya utapiamlo mkoani Iringa ni kutomlisha mtoto chakula chakutosha, hali hii inatokana na elimu ndogo juu ya lishe na matunzo ya mtoto kwa upande wa mama. Aidha kazi nyingi zinazomkabili mama zinampunguzia muda wa kumhudumia mtoto. Hatua mbalimbali zimekwisha chukuliwa na mkoa za kufuta utapiamlo na vile vile kuhakikisha lishe bora kwa mama na mtoto. Hatua hizi ni kama zifuatazo:-

i) Wataalam washauri 546 wamekwishapata mafunzo katika ngazi za Kata na vijiji juu ya kutambua kaya zenye kuelekea kwenye kupungukiwa na chakula kwa lengo la kuzisaidia.

ii) Kutolewa misaada kwa kaya zenye matatizo mbalimbali kama vile zile zinazoongozwa na mwanamke peke yake, familia zenye wake zaidi ya mmoja au familia zenye mapacha n.k. Mafanikio ya kupunguza utapiamlo mkali kati ya watoto walio chini ya miaka mitano mkoani Iringa kutoka kwenye idadi ya 6948 mwaka 1992 hadi 6376 mwaka 1995 yanatokana na kazi nzuri iliyofanywa na mpango wa uhai wa Mama na Mtoto mkoani Iringa (Jedwali Na. LXXIII).

## JEDWALI Na. LXXIII: HALI YA LISHE YA WATOTO UMRI WA MIAKA 0-5 (1992 - 1994).

| Wilaya | 1992 | | 1993 | | 1994 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Utapiamlo Mkali | Utapiamlo wa kiasi | Utapiamlo Mkali | Utapiamlo wa kiasi | Utapiamlo mkali | Utapiamlo wa kiasi |
| Iringa Vijijinii | 2175 | 56170 | 1919 | 59446 | 1860 | 61326 |
| Iringa Mjini | 73 | 2160 | 49 | 2192 | 120 | 6,070 |
| Mufindi | 1,642 | 33,694 | 1,660 | 42,242 | 1,490 | 43,504 |
| Njombe | 1,496 | 53.395 | 1,540 | 54,434 | 1,471 | 56,411 |
| Ludewa | 739 | 14854 | 830 | 18119 | 950 | 22,148 |
| Makete | 822 | 16,040 | 701 | 20,134 | 485 | 20,611 |
| Jumla | 6,948 | 178,313 | 6,699 | 196,567 | 6,376 | 210,070 |

Chanzo: Uhai wa Mama na Mtoto Mkoa wa Iringa, Taarifa ya 1994.

## JEDWALI Na. LXXIV: HUDUMA CHA CHANJO/KINGA KWA WATOTO WA UMRI WA MWAKA 0 - 1; 1992 NA 1993 MKOA WA IRINGA

| | Aina ya Kinga | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wilaya | 1992 | | | | 1993 | | | |
| | (BCG) Kifua Kikuu | (DPT-3) Donda Koo | (Polio - 3) Kupooza | (Measles) Surua | (BCG) Kifua Kikuu | (DPT - 3) Donda Koo | (Polio -3) Kupooza | (Measles) Surua |
| Iringa Vijijini | | | | | | | | |
| Lengo | 20,096 | 20,096 | 20,096 | 20,096 | 20,818 | 20,818 | 20.818 | 20,818 |
| Utekelezaji | 13,393 | 16,377 | 15,694 | 16,032 | 20,609 | 8,112 | 18,994 | 16,862 |
| | (67) | (82) | (78) | (80) | (99) | (87) | (91) | (81) |
| Iringa Mjini | | | | | | | | |
| Lengo | 3,908 | 3,908 | 3,908 | 3,908 | 3,908 | 3,908 | 3,908 | 3,908 |
| Utekelezaji | 2,707 | 2,662 | 2,513 | 3,449 | 3,449 | 2,173 | 2,844 | 3,949 |
| | (69) | (68) | (64) | (86) | (86) | (73) | (72) | (99) |
| Mufindi | | | | | | | | |
| Lengo | 10,221 | 10,221 | 10,221 | 10,221 | 10,221 | 10,221 | 10,221 | 10,221 |
| Utekelezaji | 4,904 | 9,373 | 9,523 | 10,217 | 6,129 | 10,002 | 10,067 | 9,045 |
| | (48) | (92) | (93) | (99) | (58) | (95) | (96) | (86) |
| Njombe | | | | | | | | |
| Lengo | 14,060 | 14,060 | 14,060 | 14,060 | 14,440 | 14,440 | 14,440 | 14,440 |
| Utekelezaji | 13,656 | 12,969 | 11,747 | 12,220 | 14,151 | 12,969 | 13,285 | 14,440 |
| | (97) | (80) | (84) | (87) | (98) | (90) | (92) | (90) |
| Ludewa | | | | | | | | |
| Lengo | 4,884 | 4,884 | 4,848 | 4,884 | 5,138 | 5,138 | 5,138 | 5,138 |
| Utekelezaji | 4,414 | 3,959 | 3,994 | 3,975 | 4,888 | 4,939 | 5,097 | 5,000 |
| | (90) | (81) | (82) | (81) | (95) | 96) | (99) | (97) |
| Makete | | | | | | | | |
| Lengo | 4,309 | 4,309 | 4,309 | 4,309 | 4,309 | 4,309 | 4,309 | 4,309 |
| Utekelezaji | 3,793 | 3,701 | 3,681 | 3,373 | 3,531 | 3,621 | 3,621 | 3,573 |
| | (88) | (86) | (85) | (78) | (81) | (84) | (83) | (83) |

Chanzo: Mpango wa Uhai wa Mama na Mtoto Mkoa wa Iringa Taarifa ya mwaka Jan. 1992 - June 1994.

Takwimu katika mabano = Asilimia ya utekelezaji wa lengo.

**JEDWALI Na. LXXV: CHANJO YA PEPO PUNDA (TETANUS) KWA WAKINAMAMA, KIWILAYA MKOA WA IRINGA MWAKA 1992 NA 1993.**

| Mwaka | Ugonjwa | Iringa Vijijini | Iringa Mjini | Mufindi | Njombe | Ludewa | Makete |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Wanawake | Wanawake | Wanawake | Wanawake | Wanawake |
| 1992 | TT1 | 15795 | 3941 | 11865 | 13431 | 5664 | 4089 |
| | TT2 | 110111 | 1723 | 10594 | 9748 | 4529 | 3953 |
| | TT3 | 4883 | 414 | 3564 | 6213 | 2640 | 3936 |
| | TT4 | 1530 | 38 | 699 | 584 | 923 | 1463 |
| | TT5 | 42 | 0 | 38 | 6 | 32 | 7 |
| Jumla | | 32361 | 6116 | 26760 | 29982 | 13788 | 13448 |
| 1993 | TT1 | 33692 | 4549 | 13203 | 57036 | 5461 | 2445 |
| | TT2 | 23910 | 3193 | 10693 | 44764 | 4663 | 2428 |
| | TT3 | 11955 | 1899 | 7419 | 29612 | 3048 | 2949 |
| | TT4 | 4046 | 424 | 2270 | 5198 | 2203 | 2873 |
| | TT5 | 996 | 95 | 368 | 722 | 732 | 849 |
| Total | | 74,599 | 10,160 | 33.953 | 268728 | 16107 | 11544 |

Chanzo: Taarifa ya Mpango wa Uhai wa Mama na Mtoto June 1994, Mkoa wa Iringa.

Jedwali Na. LXXV linaonyesha wanawake wengi wilayani Iringa Vijijini walipata chanjo ya pepo punda kuliko wilaya nyingine Mkoani Iringa isipokuwa wilaya ya Njombe ambayo iliongoza kwa idadi ya chanjo 1993. Kwa mfano mwaka 1992 wanwake 32,361 Iringa Vijijini walipata chanjo kuunganisha na idadi ya wanawake 29,982 waliopata wilayani Njombe na 13,448 waliopata wilayani Makete. Mwaka 1993 wanawake 74,599 walipata chanjo ya pepo punda Iringa Vijijini ikilinganishwa na wanawake 33,953 waliopata wilayani Mufindi, wanawake 11,544 Makete na wanawake 137,324 walipata chanjo hiyo wilayani Njombe.

### 4.2.8 Usafi wa Mazingira:

Uchafuzi wa vyanzo vya maji umekuwa chanzo cha magonjwa mengi yakiwemo magonjwa ya kuharisha, homa ya matumbo n.k. Hivyo njia pekee ya kuhifadhi usafi wa mazingira ni kwa kujenga vyoo bora katika maeneo muhimu ya Umma kama vile katika shule za msingi na kwenye taasisi za afya. Vyoo ni

vyombo muhimu sana katika kufanikisha usafi wa mazingira; hivyo basi uongozi wa Mkoa unawajibika katika kutafuta njia za kutunga sheria ndogo ndogo ambazo zingewabana wananchi ili wote waweze kuwa na vyoo na wanavitumia.

**JEDWALI Na. LXXVI: KAYA ZILIZO NA ZISIZO NA VYOO MKOANI IRINGA, 1995.**

| Wilaya | Kaya zenye Vyoo vya Kudumu | Kaya zenye Vyoo vya muda | Jumla ya Vyoo | Kaya ambazo hazina Vyoo | Asilimia ya Kaya hazina Vyoo |
|---|---|---|---|---|---|
| Iringa Mjini | 12,320 | - | 12,320 | 315 | 2.5 |
| Iringa Vijijini | 14,036 | 10,696 | 24,732 | 737 | 3.0 |
| Mufindi | 36,033 | 10,985 | 47,018 | 984 | 2.1 |
| Njombe | 117,682 | 17,372 | 135,054 | 70 | 0.1 |
| Kudewa | | | | | |
| Makete | 21,942 | 3,314 | 25,256 | 220 | 0.9 |
| Jumla | 202,013 | 53,063 | 244,380 | 2,326 | 0.9 |

Chanzo: Taarifa ya Idara ya Afya ya mwaka 1994, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Iringa.

Kwa wastani idadi kubwa ya Kaya Mkoani Iringa wana vyoo, ni asilimia 0.9 tu ya Kaya hazina vyoo.

**JEDWALI Na.LXXVII: HALI YA MGAWANYO WA AINA TA VYOO MIJINI NA VIJIJINI KIMKOA TANZANIA BARA; SENSA YA 1988.**

| | Vijijini (Asilimia) | | | Mjini (Asilimia) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mikoa | Vyoo vya kuvuta kwa maji | Vyoo vya shimo | Hakuna Vyoo | Vyoo vya Kuvuta kwa maji | Vyoo vya shimo | Hakuna Vyoo |
| Iringa | 0.9 | 97.1 | 2.0 | 4.0 | 94.9 | 1.1 |
| Dodoma | 0.6 | 81.0 | 18.2 | 16.5 | 78.6 | 4.2 |
| Arusha | 1.2 | 65.9 | 32.8 | 18.4 | 79.5 | 2.0 |
| Kilimanjaro | 2.7 | 92.5 | 4.5 | 24.4 | 71.3 | 4.3 |
| Tanga | 0.8 | 80.8 | 18.3 | 16.2 | 79.2 | 4.5 |
| Morogoro | 1.3 | 88.6 | 9.5 | 12.7 | 84.8 | 2.5 |
| Pwani | 0.9 | 76.1 | 23.0 | 4.8 | 88.3 | 6.7 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 3.8 | 80.9 | 15.2 | 15.9 | 83.1 | 1.0 |
| Lindi | 0.6 | 77.2 | 22.2 | 4.7 | 85.0 | 10.3 |
| Mtwara | 1.0 | 84.2 | 14.8 | 7.4 | 86.1 | 6.6 |
| Ruvuma | 1.3 | 95.4 | 3.2 | 4.0 | 94.7 | 1.3 |
| Mbeya | 1.4 | 94.3 | 4.4 | 6.1 | 91.8 | 2.1 |
| Tabora | 0.7 | 91.9 | 7.4 | 9.1 | 89.5 | 1.5 |
| Rukwa | 0.5 | 73.2 | 26.3 | 4.2 | 92.4 | 3.4 |
| Kagera | 0.5 | 86.6 | 12.9 | 13.0 | 81.4 | 5.7 |
| Singida | 0.9 | 78.6 | 20.5 | 7.0 | 87.6 | 5.5 |
| Kigoma | 0.7 | 94,1 | 5.2 | 5.3 | 91.9 | 2.8 |
| Shinyanga | 1.0 | 84.3 | 14.7 | 16.1 | 79.4 | 4.6 |
| Mwanza | 0.6 | 86.9 | 12.4 | 11.9 | 80.7 | 7.3 |
| Mara | 0.8 | 76.0 | 23.2 | 9.0 | 85.0 | 6.0 |

Chanzo: Sensa ya Idadi ya Watu 1988, Ripoti ya Kitaifa.

Jedwali Na. LXXVII linaonyesha kwamba Mkoa wa Iringa ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya vyoo vya shimo vijijini na mjini kuliko mikoa mingine nchini. Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na vyoo vya kuvuta kwa maji, vingi zaidi vijijini na mjini kuliko mikoa mingine nchini.

## 4.3 Sekta ya Maji:

Maji ni kitu muhimu sana kwa maisha bora ya binadamu na ni muhimu kwa shughuli za uzalishaji kama vile kilimo na viwanda. Lengo la Taifa kuhusu huduma ya maji ni kuwapatia wananchi huduma hii karibu nao kwa umbali usiozidi meta 400 hadi ifikapo mwaka 2000. Pamoja na Sera hii kufikia hadi mwaka 1996 jumla ya watu 733,996 tu sawa na asilimia 52 Mkoani Iringa walikuwa wanahuduma ya maji safi (Jedwali Na. LXXVIII(a)).

**JEDWALI Na. LXXVIII(a) IDADI YA WATU WANAOPATA MAJI SAFI KIWILAYA MKOANI IRINGA 1996.**

| Wilaya | Watu wanaopata Maji safi | Vijiji vinavyopata Maji safi | Vijiji haivna Maji safi |
|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 193,835 | 91 | 75 |
| Iringa Mjini | 106,400 | - | 3 |
| Mufindi | 154,500 | 45 | 82 |
| Njombe | 185,311 | 74 | 96 |
| Ludewa | 53,664 | 23 | 24 |
| Makete | 40,287 | 37 | 59 |
| Jumla | 733,996 | 270 | 339 |

Chanzo: Mhandisi wa Maji Mkoa, Iringa.

Asilimia 48 ya watu mkoani wanapata mahitaji yao ya maji kutoka visimani na mito maji ambayo hayana usafi na usalama. Ni muhimu kuwahamasisha wananchii katika ujenzi wa huduma bora zaidi za maji na usafi wa mazingira. Hii ni pamoja na kuvilinda vyanzo vya maji, kuwafunza namna ya kuyahifadhi maji ya mvua na ujenzi wa vyoo bora. Vyanzo muhimu vya maji Mkoani Iringa ni pamoja na mito (mfano mto Ruaha), vijito, chemchem na mabwawa.

### 4.3.1 Huduma ya Maji Mjini:

Matarajio ya idadi ya watu waishio mjini mwaka 1995 ni 194,701 mkoani Iringa. Jedwali Na. LXXVIII(b) linaweka bayana hali ya usambazaji maji mjini mkoani Iringa mwaka 1995.

**JEDWALI Na. LXXVIII(b) HUDUMA YA MAJI SAFI MJINI, MKOA IRINGA, 1995**

| **Mji** | **Idadi ya Watu** | | | **Watu wanaopata Maji safi** | **Asilimia wanaopata maji** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Sensa ya 1988** | **Makisio ya Watu 1995** | **Asilimia Ongezeko la Watu** | | |
| Iringa Mjini | 84,501 | 114,994 | 4.5 | 68,996 | 60 |
| Mafinga | 25,010 | 30,138 | 2.7 | 12,055 | 40 |
| Njombe | 25,339 | 30,534 | 2.7 | 18,320 | 60 |
| Ludewa | 6,417 | 7,733 | 2.7 | 3,093 | 40 |
| Iwawa | 9,379 | 11,302 | 2.7 | 5,650 | 50 |
| Jumla | 150,646 | 194,701 | 2.8 | 108,114 | 55.5 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Maji, Hali ya Usambazaji Maji Mkoani Iringa.

Miji ya Iringa na Njombe pekee ilipata maji kwa wakazi wake kwa asilimia 60 mwaka 1995. Miji ya Mafinga na Ludewa kwa kiwango cha asilimia 40 ya wakazi wake walikuwa wanapata huduma ya maji safi. Mji mdogo wa Iwawa ulipata kwa asilimia 50. Viwango hivi vya chinii vinaleta wasiwasi iwapo kweli Sera ya kuwafikishia huduma ya maji wananchi karibu nao umbali usiozidi meta 400 ifikapo mwaka 2000 utafanikiwa kwa hiyo iwapo lengo halijabadilika, basi kuna ulazima wa kufanya juhudi kubwa zaidi kufikia utekelezaji wa lengo lenyewe ikizingatiwa hali halisi ilivyo kwa mwaka 1995, ambapo asilimia 55.5 ya wakazi wa mijini Mkoani Iringa walikuwa wanapata huduma ya maji safi na yaliyosalama karibu nao umbali usiozidi meta 400.

a) **Usambazaji Maji Iringa Mjini:**

Mpango wa usambazaji maji mjini Iringa ulianza mwaka 1953. Tangu hapo huduma ya maji mjini imeendelea kutegemea kutoka vyanzo vya mito na visima virefu. Kutokana na kupanuka kwa mji wenyewe na kuchakaa mitambo ya kusukuma maji, mji wa Iringa haupati maji ya kutosheleza mahitaji ya

wakazi wake. Upungufu huu wa maji utaendelea kukua iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa kurekebisha hali hii. Idadi ya wakazi mjini Iringa inatarajiwa kufikia 137,714 ifikapo mwaka 1999. Mahitaji ya maji kwa wakazi wa mji huu ni meta za ujazo 15,000 kwa siku na kiwango kinachopatikana ni meta za ujazi 10,000 kwa siku. Kwa hiyo upo upungufu wa meta za ujazo 5,000 kwa siku.

b) **Usambazaji Maji Mjini Mafinga**:

Mji wa Mafinga uko km 80 kusini mwa mji wa Iringa unapata maji kwa njia ya mteremko kutoka vyanzo vya chemchemi na kiasi yanasukumwa na mitambo kutoka vijito. Mji unaokuwa kwa asilimia 2.7 kwa mwaka vyanzo vya maji vilivyopo sasa havitatosheleza mahitaji ya maji mjini Mafinga. Mahitaji ya maji kwa siku mjini Mafinga ni meta za ujazo 3,200 lakini kiwango kinachopatikana kwa siku ni meta za ujazo 1,280. Hivyo upo upungufu wa meta za ujazo 1920 kwa siku. Hali ya upatikanaji maji mjini Mafinga utaendelea kuwa duni zaidi na zaidi iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa haraka iwezekanavyo.

c) **Usambazaji Maji Mjini Njombe**:

Mji wa Njombe uko km 240 kusini mwa mji wa Iringa na unapata mahitaji yake ya maji kutoka kwenye mito. Uwezo wa mto huu ni 2,760 $M^3$ 4,600$M^3$ kwa siku. Hali hii inaeleza kuwepo kwa upungufu wa 1840 $M^3$ kwa siku. Idadi ya watu Mjini Njombe inaongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.7 kwa mwaka mpaka ifikapo mwaka 2010 mji huu utakuwa na wakazi

wapatao 45,500 wakihitaji maji 6,830 $M^3$ kwa siku. Budi Njia zitafutwe za kupata vyanzo vingine vya maji au kuimarisha chanzo cha maji kilichopo sasa.

d) **Usambazaji Maji Mjini Iwawa**:

Mji wa Iwawa unapata maji kutoka vyanzo viwili vya mito midogo kwa njia ya kutiririka (gravity). Kama ilivyo kwa miji mingine, kiwango cha maji yanayopatikana hayatoshelezi mahitaji ya mji. Kutokana na ongezeko la watu kwa asilimia 2.7 kwa mwaka, mji huu utakuwa na idadi ya watu 16,860 ifikapo mwaka 2010. Hali hii itasababisha mahitaji ya maji hadi kufikia 2,520 $M^3$ kwa siku dhidi ya mahitaji ya sasa ya 1150 $M^3$ kwa siku, Kiwango kinachopatikana sasa ni 580 $M^3$. Wahusika wanakumbushwa kuanza kupanga na kutekeleza mipango itakayowezesha mji kuwa na huduma ya maji ya kutosha sasa na hapo baadaye.

e) **Usambazaji Maji Mjini Ludewa**:

Mji wa Ludewa hupata maji kutoka vyanzo vya maji ya mito miwili umbali wa km. 11. Vyanzo hivi havitoshelezi mahitaji ya mji ambayo ni 780$M^3$ kwa siku, lakini uwezo uliopo sasa ni 310 $M^3$ kwa siku, sawa na asilimia 40. Iwapo tatizo hili halitashughulikiwa sasa au hivi karibuni basi ongezeko la watu linalosababishwa na ukuaji wa idadi ya watu kwa asilimia 2.7 litaongeza tatizo la maji mjini Ludewa kuwa kubwa sana. Inakisiwa idadi ya watu mjini Ludewa itakuwa 11,530 ifikapo mwaka 2010.

### 4.3.2 Usambazaji Maji Vijijini:

Usambazaji maji vijijini mkoani Iringa unagharamiwa na wafadhili kutoka nje, hali kama ilivyo kwa mikoa mingine nchini. DANIDA (Danish International Development Agency) limefadhili mipango ya maji vijijini tangu 1979. Hadi mwishoni mwa mwaka 1995 Shirika hili lilikuwa limekamilisha na kukabidhi miradi 111 ya maji vijini. Kukamilika kwa miradi hii kumelifanya Shirika hili kuwa lenye shughuli nyingi zaidi za kimaendeleo Mkoani Iringa. Mashirika mengine ni pamoja na UNICEF, Benki ya Dunia, Umoja wa Uchumi wa Ulaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, CONCERN, CDTF na Taasisi za Kidini. Shirika la Umoja wa Mataifa la UNICEF limejihusisha na miradi mingi ya maji vijijini mkoani Iringa. Mfano wa mradi iliyotekelezwa na shirika hili ni:- Mradi mkubwa wa Maji wa Wanging'ombe Njombe (Maji yanasambazwa kwa mteremko).

Mradi wa maji wa Fukulwa/Makambako unahudumia vijiji 10 na maji yake husambaa kwa mteremko. Mradi wa Maji wa Lifua Manda nao pia unahudumia vijiji 10 wilayani Ludewa kwa njia ya miteremko. Shirika la UNICEF ni la pili kwa umuhimu katika kuvipatia maji vijiji mkoani Iringa. Benki ya Dunia na Umoja wa Uchumi wa nchi za Ulaya yamejihusisha zaidi na kugharamia miradi ya maji mjini Iringa tangu 1982. Shirika la Ireland "CONCERN" limejihusisha na mradi wa maji wa Malangali unaosambaza maji kwa vijiji 10 wilayani Mufindi. Kanisa Katoliki limegharamia miradi kadhaa ya maji wilayani Njombe, Ludewa na Iringa Vijijini; ambapo kanisa la Kiinjili la Kilutheri nalo limekamilisha miradi kadhaa wilayani Njombe, Makete na Iringa Vijijini. Jedwali Na. LXXIX linaonyesha hali ya usambazaji maji vijijini Mkoani Iringa 1995.

**JEDWALI Na. LXXIX: HALI YA USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI, MKOA WA IRINGA, 1995**

| Wilaya | Idadi ya Watu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sensa ya 1988 | Makisio 1995 | Watu wapatao Maji | % ya wale wapatao Maji | Idadi ya Vijiji | Vijiji vyenye Maji | % ya Vijiji vyenye Maji |
| Iringa Vijijini | 362,493 | 436,810 | 240,320 | 55 | 183 | 87 | 47.5 |
| Mufindi | 204,260 | 246,137 | 111,576 | 45.3 | 127 | 52 | 40.9 |
| Njombe | 288,648 | 347,826 | 190,973 | 54.9 | 166 | 82 | 49.4 |
| Ludewa | 93,789 | 113,017 | 56,284 | 49.8 | 48 | 23 | 27.9 |
| Makete | 93,283 | 112,408 | 38,021 | 33.8 | 96 | 29 | 30.2 |
| Jumla | 1,042,473 | 256,198 | 637,174 | 50.7 | 619 | 273 | 44.0 |

Chanzo: Iringa Region: Situation Analysis for Water Supplies in Iringa Region 1995.

Jedwali Na. LXXIX linaonyesha kwamba asilimia 50.7 tu ya wakazi wa vijijini mkoani Iringa walikuwa wanapata maji safi mwaka 1995. Vile vile linaonyesha kuwa chini ya asilimia 50 ya wakazi wa vijijini wilayani Makete, Ludewa na Mufindi walikuwa wanapata maji safi. Kwa upande wa vijiji Jedwali Na. LXXIX linadhihirisha kwamba chini ya asilimia ya vijiji wilayani Makete na Ludewa vilikuwa vimepata maji safi (1995). Wilaya za Iringa na Njombe zilikuwa zinahudumiwa vema, kwani asilimia 87 ya vijiji Iringa Vijijini vilikuwa vinapata maji safi, na kwa asilimia 82 vijiji vya wilaya ya Njombe.

## 4.3.3 Mifereji ya Maji Machafu:

Hakuna hata mji mmoja katika mkoa wa Iringa ambao unamifereji ya maji machafu, badala yake yanatumika matanki kwa madhumuni ya kufanikisha usafi mjini. Inakadiriwa vile vile kuwa asilimia 95 ya wananchi mijini wanayo hayo matanki ya maji machafu. Kwa upande wa vijijini asilimia 80 ya wananchi hutumia vyoo vya mashimo kama njia kuu ya kufanikisha usafi.

## 5.0 MASUALA MENGINE KUHUSIANA NA MAENDELEO

### 5.1 Wanawake na Maendeleo:

Kuwapa uwezo wanawake na kuinua hali yao ya maisha ni mwelekeo muhimu sana katika kuleta maendeleo makubwa. Lengo ni kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake; kuwawezesha wanawake kutambua umuhimu wao katika shughuli za uzalishaji; kuwahusisha wanawake katika kufikia maamuzi mbali mbali ya kiuchumi, siasa na kijamii kama washiriki na wenye kufaidika na maamuzi hayo. Lakini kwa bahati mbaya haya yote hawayapati pamoja kwamba wao ndio waliowengi zaidi katika jamii. Kwa mfano mkoa wa Iringa ulikuwa na jumla ya watu 1,208,914 na kati ya hawa wanawake walikuwa asilimia 53 (Sensa ya Idadi ya Watu 1988). Kiwango hiki kinadhihirisha jinsi walivyowengi Mkoani Iringa. Wanawake ndio wajibidishao mashambani licha ya jukumu au wajibu wao wa asili wa kuzaa na kulea watoto. Licha ya wanawake kuchangia kwa kiwango kikubwa kwa pato la mwaka la Mkoa (Regional GDP) wanawake wanaunda kundi kubwa la watu wasiojua kusoma na kuandika, karibu asilimia 65 na kujikuta wao ndio wanaopata lishe duni na kutoshirikishwa katika maamuzi katika jamii. Wanawake pia wanaunda kundi kubwa la watu maskini huko vijijini na kunyimwa haki zao za msingi za kugawana na kumiliki mali kutokana na jasho lao au kushiriki katika uzalishaji huo.

Wilayani Mufindi vifo vya akinamama wajawazito vinafikia karibu 397 kati ya wajawazito 100,000 kila mwaka. Taarifa ya 1994 ya Mpango wa Uhai wa Mama na Mtoto Mkoani Iringa inasema kwamba watoto 2,131 walio chini ya miaka mitano walikufa kutokana na utapiamlo mwaka 1993. Vifo hivi

vya watoto na wakinamama vingeweza kuepukika au kupunguzwa iwapo wanawake wangepewa uwezo wakujipatia pato la kutosha na kupewa uwezo wa kutumia uchumi huo jinsi wanavyoona inafaa. Umaskini na pato duni ndiyo sababu kubwa zinazosababisha utapiamlo na vifo vya wakinamama na watoto. Hii ni kwa sababu familia maskini hazina uwezo wa kuwalisha vyema wanaowategemea. Katika jitihada za kuwakwamua wanawake kutoka katika tatizo la umaskini Mkoani Iringa, wanawake wenyewe wamejiunga pamoja katika makundi mbalimbali ya kiuchumi. Hadi mwaka 1996 kulikuwa na makundi ya wakinamama 263 yenye jumla ya wanachama 747 wakijishughulisha na mambo mbalimbali.

**JEDWALI Na. LXXX: IDADI YA VIKUNDI VYA UCHUMI VYA WANAWAKE NA IDADI YA WANACHAMA, MKOANI IRINGA 1996**

| Wilaya | Idadi ya Vikundi vya Wanawake | Jumla ya Wanachama |
|---|---|---|
| Iringa Vijijini | 127 | 150 |
| Mufindi | 39 | 155 |
| Njombe | 39 | 344 |
| Ludewa | 22 | 53 |
| Makete | 36 | 45 |
| Jumla | 263 | 747 |

Chanzo: Taarifa ya Uhai wa Mama na Mtoto, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, 1996.

Tofauti na mikoa mingine shughuli zinazofanywa na vikundi vya wanawake mkoani Iringa Vijijini ni za kiuchumi kimsingi. Shughuli muhimu zinazopendwa na vikundi hivyo kiwilaya ni kama zifuatazo:-

a) **Iringa Vijijini**:

- Kilimo
- Ukamuaji mafuta
- Usagaji wa nafaka.

b) **Njombe:**

- Ukamuaji mafuta
- Usagaji wa nafaka
- Ng’ombe wa kukokota jembe
- Kilimo cha mahindi
- Kilimo cha nafaka
- Ufugaji ng’ombe wa maziwa.

c) **Mufindi:**

- Usagaji wa nafaka
- Kilimo cha ujumla

d) **Makete:**

- Kilimo cha ujumla
- Ushonaji
- Kilimo cha mahindi

e) **Ludewa**:

- Kilimo cha mazao
- Ufugaji wa nguruwe.

## 5.2 Elimu ya Wanawake:

Elimu ni msingi wa maendeleo. Elimu ndiyo ufunguo wa maarifa, inasaidia wanawake kupunguza viwango vya uzazi, magonjwa na vifo; elimu inampa uwezo mwanamke. Mwanamke anapokuwa ameelimika vizuri viwango vya kuishi watoto vinakuwa juu, wanaolewa wanapokuwa wamefikia umri mkubwa, kupunguza ukubwa wa familia na kwa kufanya hivyo hupata muda wakutosha katika shughuli za kiuchumi na kulea watoto wake walio na afya nzuri na wenye furaha.

## 5.3 Matatizo yanayojitokeza katika vikundi vya Kinamama:

Wanawake ndiyo waliowengi zaidi ya nusu ya idadi ya watu mkoani, wanawake ndiyo wazalishaji wakuu wa chakula na ndio wenye jukumu la kulea watoto, hivyo basi kuna sababu za kutosha kwa uongozi wa mkoa kufuatilia kwa karibu matatizo yanayojitokeza katika vikundi vya wanawake na kuvipatia ufumbuzi yafuatayo ni matatizo ambayo yamejitokeza katika vikundi vya wanawake mkoani Iringa.

i) Ukosefu wa huduma ya mikopo ya kuwawezesha wanawake kujipatia zana, pembejeo n.k.
ii) Ukosefu wa mafunzo kwa washiriki wa vikundi.
iii) Tatizo la usafiri na usafirishaji.
iv) Kutopatikana ushauri wa kitaalam ili kuwawezesha kuongeza idadi na ubora wa matunda ya kazi zao.
v) Kutumia teknolojia ya zamazi katika uzalishaji.

## 5.4 Ushirika:

Shughuli za ushirika Tanzania kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita zimekuwa na mabadiliko mengi. Mabadiliko makubwa ya mwelekeo wa ushirika yamo katika sheria ya Ushirika ya 1991. Sheria hii inaipunguzia Serikali nguvu ya kuingilia masuala ya ushirika na inampa uhuru mtu kujiunga au kutojiunga na ushirika, kuwepo na gharama za uanachama na ulazima wa kununua angalau hisa moja, hii ni kwa wanachama wote. Kwa kuongezea, sheria hii inazipa vyama vya msingi vya ushirika kuunda chombo chao cha juu cha ushirika (Ushirika na Muungano). Kabla ya sheria ya 1991 vyama vikuu vya ushirika vilikuwa vimechukua ukiritimba wa ununuzi wa mazao yote makuu ya biashara yaliyozalishwa na vyama vya msingi. Sheria ya zamani ya Vyma vya Ushirika ilikuwa inavipa Vyama Vikuu vya Ushirika mamlaka ya kuvinyonya vyama vya msingi na uendeshaji mbovu wa vyama vya ushirika hizo. Kwa sheria hii mpya tatizo hili limetoweka kabisa na vyama vya msingi sasa vinajiendesha kibiashara na kwa msingi ulio imara. Vipo vyama vya msingi 219 vilivyojiandikisha Mkoani Iringa. Kati ya hivi 219 ni vyama vya Ushirika vya msingi na vyama 2 vikuu vya ushirika (Iringa Famers Cooperative Union (1993) Ltd. na Njombe, Ludewa, Makete Farmers Cooperative Union Ltd.

## 5.5 Shughuli za NGO's Mkoani Iringa:

Idadi ya NGO's Mkoani Iringa ni kubwa na shughuli zake ni nyingi na inawezekana kabisa kwa uongozi wa Mkoa kutofahamu barabara madhumuni ya kila moja wapo na kiwango gani cha rasilimali NGO fulani inaweza ikasaidia. Kuelewa vyema shughuli na malengo ya NGO mbalimbali mkoani kunaweza kukasaidia katika kuratibu shughuli za mashirika haya yasiyo ya kiserikali na hivyo kutumia kwa

kikamilifu zaidi rasilimali zilizopo kwa manufaa ya wakazi wa Mkoa. Shirika la CONCERN linafanya shughuli zake katika Tarafa za lsimani na Malangali katika wilaya ya Iringa Vijijini na wilayani Mfindi. CONCERN imekuwemo mkoani kuanzia 1978 ikijishughulisha na shughuli za kilimo katika utoaji ushauri wa kitaalam na utoaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa njia ya mikopo. Aidha shirika linajihusisha na masuala ya kifadhi ya mazingira kwa kuotesha miche ya miti. Shirika la CDTF linatoa misaada ya kifedha kwa miradi ya maji hasa katika wilaya ya Ludewa. Mashirika ya kidini yanayojihusisha mkoani Iringa ni Kanisa Latoliki, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri na Kanisa la Kianglikana.

**Miradi ya Wafadhili:**

Miradi inayoendeshwa au kufadhiliwa na nchi au mashirika ya nje ni:-

| | | |
|---|---|---|
| Mradi wa Maji Vijijini | - | DANIDA |
| Hifadhi Mazingira (HIMA) | - | DANIDA |
| CSPD | - | UNICEF/WHO |

i) **Hifadhi Mazingira (HIMA):**

Mradi huu ulianza mwaka 1982 katika Tarafa za Kilolo na Mazombe wilayani Iringa vijijini. Mwaka 1992 mradi ulipanuka na kushirikisha Tarafa 2 zaidi za Imalinyi na Lupembe wilayani Njombe. Mwaka 1995 mradi wa HIMA ulipanuliwa zaidi na kushirikisha wilaya nyingine mbili: Mufindi na Ludewa.

ii) Mradi wa Uhai wa Mama na Mtoto (CSPD) ulianza mwaka 1983 ukifadhiliwa na UNICEF, WHO na Serikali za Italia na Tanzania. Madhumuni ya mradi ni kupambana na utapiamlo na kupunguza viwango vya vifo vya watoto na akinamama. Mradi ulianza na tarafa chache tu lakini sasa unahusisha Mkoa mzima.

iii) **CONCERN:**

Ni shirika la kujitolea la nchi ya Ireland, shirika linajihusisha na miradi midogo midogo ikiwemo hifadhi ya ardhi, kilimo, mboga na matunda, upatikanaji miti, lishe na maendeleo ya wanawake. Shirika linafanya shughuli zake wilayani Iringa, Mufindi na Njombe.

iv) **<u>DANIDA:</u>**

Huendesha miradi midogo midogo na maendeleo ya mifugo wilayani Njombe.

v) **IRISH FOUNDATION FOR COOPERATION AND DEVELOPMENT:**

Hushughulika na kilimo cha mboga, masoko, upatikanaji miti wilayani Iringa.

vi) **ILO:**

Hujihusisha na mradi wa uwiano wa uchukuzi vijijini wilayani Makete; mafunzo na matengenezo ya biashara kwa kutuma nguvu za wananchi walengwa.

vii) **WHO/UNCEF**:

Mradi wa ushirikiano wenye malengo mengi yakiwemo afya ya msingi, usalama wa chakula ngazi ya Kaya, Malezi na maendeleo ya mtoto; Wanawake kumiliki na kusimamia rasilimali.

viii) **Korea ya Kaskazini**:

Hutoa msaada kwa kilimo cha umwagiliaji kitelewasi wilayani Mufindi.

**Hifadhi ya Mazingira**:

Tunapozungumzia juu ya hifadhi ya mazingira tunainisha kuhifadhi uwezo wa eneo kiasili katika kuzalisha na kuendea kuwa hivyo. Maeneo yaliyo na mvua nyingi huwa na uwezo mkubwa wa kujirudia kuzalisha vyema zaidi kuliko yake katika maeneo yenye ukame. Tarafa ya Isimani ni mfano ulio hai, katika Tarafa hii maeneo ya kilimo sasa hivi yameshindwa kabisa kuzalisha mazao kwa kuwa mimea ya asili ya eneo hilo ambayo ni majani na misitu imeshindwa kuendelea kuwepo kwa sababu ya shughuli nyingi za binadamu zikiwemo za ukataji ovyo, uchomaji moto na uchomaji majani na misitu na mifugo kupita uwezo wa eneo kimalisho. Hivyo juhudi zinazofanywa sasa na DANIDA katika hifadhi ya mazingira haina budi kuungwa mkono na wote wapendao maendeleo.

DANIDA inafadhili mradi wa HIFADHI MAZINGIRA (HIMA) Mkoani Iringa. Chini ya mradi huu msaada wa Danida uko katika hifadhi ya maji, hifadhi ya udongo ili usiendelee kumomonyoka, pia maendeleo ya upandaji miti. Lazima tukumbuke daima kulisha mifugo katika malisho kupita

kiasi, uchomaji misitu, ukataji wa kuni na uvunaji samaki bila mpangilio. Vyote hivi hupunguza uzalishaji kwa kiwango kikubwa sana na kuingilia utaratibu mzima wa hali bora ya mazingira. Kwa hiyo ni suala la lazima kuandaa Sera mpya ya kudhibiti uharibifu huu. Yanapendelezwa yafuatayo yazingatiwe katika utayarishaji wa sera hiyo:-

i) Rasilimali ya misitu mkoani Iringa itaweza kutunzwa, kuheshimiwa na kuweza kukua ipasavyo kama ilivyokuwa hapo awali kabla haijaingiliwa na shughuli za binadamu.

ii) Mifugo haitaruhusiwa kulishwa katika malisho mara iwapo malisho yamekwishatumika zaidi ya nusu ili kuyawezesha malisho hayo kukua tena kabla hayajaweza kutumika tena.

iii) Kutoruhusu uvuvi unaohatarisha idadi ya samaki katika eneo.

iv) Uharibifu wa ardhi hautasababisha kukua kwa jangwa, kushuka kwa mavuno kutoka kwenye mashamba na hivyo kupunguza uzalishaji.

**Utalii:**

Utalii ni sekta inayokua haraka sana mkoani Iringa na kuendeleza uchumi wa Mkoa. Hata hivyo utalii huu unategemea sana Mbuga za Taifa za wanyama za Ruaha na Udzungwa. Mbuga hizi mbili ni tofauti na mbuga nyingine kwani zimeendelea katika hali zake za kiasili kwa maisha ya viumbe vyote waishio katika mbuga hizo. Hali hii imetokana na kutoingiliwa na shughuli za binadamu. Mbuga ya Ruaha ni ya

pili kwa ukubwa baada ya mbuga za Serengeti. Mbuga ya Ruaha inautajiri mkubwa wa aina mbalimbali ya wanyamapori isipokuwa wanyama kama swala aina ya Thomson's gazelle, nyumbu na topi. Zipo aina mbalimbali ya ndege zipatazo zaidi ya 370 ndani ya mbuga hii na baadhi yake hawajawahi kuonekana katika mbuga za ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania. Zipo Hoteli nzuri kwa wageni.

## SEHEMU YA VI

## 6.0 MAENEO YENYE UTAJIRI KWA UWEKEZAJI

### i) <u>Kilimo:</u>

Kilimo ni sekta muhimu sana katika kujenga uchumi wa Mkoa. Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 85 ya pato la mwaka la Mkoa na kutoa ajira karibu kwa asilimia 90 ya watu. Maendeleo ya kilimo hapo baadaye yatategemea kwa kiwango fulani maeneo yafaayo kwa kilimo nayo yatakuwa yanatumika kwa shughuli hiyo. Mkoa wa Iringa unazo hekta 4,194,780 ambazo zinafaa kwa kilimo lakini ni hekta 464,413 ndizo zinatumika kwa kilimo. Ina maana kwamba hekta 3,730,367 hazitumiki. Iringa vijijini zipo hekta 1,540,173 zinazofaa kwa kilimo na zinahitaji kuendelezwa. Wilayani Mufindi zipo hekta 543,445 ambazo hazijatumika; wilayani Njombe helta 828,696, hekta 430,586 wilayani Ludewa na hekta 387,463 wilayani Makete pia nazo hazijatumika kikamilifu.

Jedwali Na. LXXXI linaorodhesha mazao yanayofaa kiwilaya na kiuwekezaji:

**JEDWALI Na. LXXXI: MAZAO YANAYOFAA KIUWEKEZAJI KIWILAYA MKOA WA IRINGA.**

| Iringa Mjinii | Iringa Vijijini | Mufindi | Njombe | Ludewa | Makete |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mazao yanayofaa** | **Mazao Yanayofaa** | **Mazao Yanayofaa** | **Mazao Yanayofaa** | **Mazao Yanayofaa** | **Mazao Yanayofaa** |
| Mboga | 1. Kahawa<br>2. Tumbaku<br>3. Alizati<br>4. Pamba<br>5. Nyanya<br>6. Vitunguu<br>7. Viasi Mviringo<br>8. Mpunga<br>9. Pareto<br>10. Mahindi | 1. Kahawa<br>2. Tumbaku<br>3. Alizati<br>4. Viazi Mviringo<br>5. Pareto<br>6. Mahindi | 1. Kahawa<br>2. Tumbaku<br>3. Alizati<br>4. Nyanya<br>5. Viazi Mviringo<br>6. Pareto<br>7. Mahindi | 1. Kahawa<br>2. Tumbaku<br>3. Alizeti<br>4. Viazi Mviringo<br>5. Mpunga<br>6. Pareto<br>7. Mahindi | 1. Kahawa<br>2. Alizeti<br>3. Vitunguu<br>4. Viazi Mviringo<br>5. Mpunga<br>6. Mahindi |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mipango, 1996

## ii) Kilimo cha Umwagiliaji:

Uwezekano wa kilimo cha umwagiliaji upo katika wilaya zote Mkoani Iringa. Zipo hekta zipatazo 13,080 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa sasa Mkoa unatekeleza kilimo hiki kwa kiwango cha hekta 4,715.5 tu; hivyo hekta 8,364.5 hazijaendelezwa bado. Kiwilaya maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni kama yafuatayo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| Iringa Vijijini | - | Hekta | 3,525 |
| Mufindi | - | “ | 1,695 |
| Njombe | - | “ | 1,699.5 |
| Ludewa | - | “ | 1,480 |
| Makete | - | “ | 65 |

iii) **Ufugaji**:

Mkoa wa Iringa una idadi ya mifugo ifuatayo: Ng'ombe 534,792; mbuzi 178,874 na kondoo 19,136 (Sensa ya mifugo 1984) upo uwezekano kuendeleza ufugaji bora wananchi wataelimishwa juu ya umuhimu wa kupunguza idadi ya mifugo waliyonayo. Kuwa na idadi ndogo ya mifugo inamwezasha mfugaji kutunza vizuri mifugo yake na pale pale kuongeza ubora wa mazao yatokanayo na mifugo hiyo na hivyo kumwongezea pato.

**JEDWALI LIFUATALO LINAONYESHA VIWANGO VYA UZALISHAJI NA UWEZEKANO WA KUFIKIA VIWANGO VYA JUU VYA UZALISHAJI.**

| Kuku wa Kienyeji | | |
|---|---|---|
| Mayai<br>Nyama (kgs) | 30 kwa mwaka<br>0.75 Kgs | 75 kwa mwaka<br>1.5 kgs |
| Ng'ombe wa kienyeji | | |
| Uzito (Nyama)<br>Maziwa | 250 Kgs<br>0.6 lita kwa siku | 400<br>1.5 lita kwa siku |
| Ng'ombe Chotara | | |
| Uzito (Nyama)<br>Maziwa | 350<br>6 lita kwa siku | 450 Kgs.<br>15 lita kwa siku |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Idara ya Kilimo na Mifugo.

iv) **Misitu:**

Mkoa wa Iringa ni miongozi mwa mikoa nchini yenye rasilimali kubwa ya misitu. Rasilimali hii inahitajika kutumika lakini kwa kiwango kisichoweza kuadhiri mazingira. Kutokana na mahitaji makubwa ya kuni, mbao, karatasi na mazao mengine ya misitu kuna hatari ya misitu hiyo kupotea polepole na hivyo hatimaye kujikuta iko mbali na watu kutokana na mahitaji hayo makubwa na mwishoni misitu hiyo kupotea kabisa. Uharibifu wa misitu unapunguza rutuba na uimara wa udongo. Ili kuzuia

uharibifu wa ukataji wa misitu ovyo bila mpangilio, wawekezaji wakaribishwe katika upandaji wa miti. Yapo maeneo mengi na makubwa kwa ajili hii.

v) **Ufugaji Nyuki**:

Zaidi ya asilimia 60 ya eneo lote la mkoa wa Iringa linafaa kwa ufugaji nyuki. Taarifa zipo zunazoeleza kwamba makundi ya nyuki yaliyopo mkoani Iringa yanauwezo wa kuzalisha tani 116 za asali na tani 7 za nta kwa mwaka kwa bei za sasa ya asali na nta (1994/95) mkoa ungeweza kujipatia pato kubwa la T.Shs. 63.6 millioni kwa mwaka.

Mfano:

i) Kilo 1 ya asali = 500/=

500/= x 116 tani x 1000= 58,000,000/=.

ii) Kilo 1 ya nta = 800/=

800/= x 7 tani x 1000 = <u>5,600,000/=</u>

Jumla Tshs. <u>63,600,000/=</u>

Kwa mfano huu inaonyesha jinsi gani mkoa ungeweza kufaidika kiuchumi na ufugaji nyuki iwapo tu wananchi wangeelimishwa ya kutosha juu ya faida ya ufugaji huu.

vi) **Madini:**

Mkoa wa Iringa umebahatika kuwa na madini mengi ya thamani, yakiwemo madini ya aina ya:-

Makaa ya mawe, manganese oxide, kaolin, kimbelite, dhahabu, rubby, green tomalite, soap stone, chrome n.k. Madini sharti yachimbwe ili kuuletea mkoa pato na nchi yote kwa ujumla. Madini ya chuma na makaa ya mawe yaliyoko wilayani Ludewa yanahitaji uwekezaji mkubwa wa rasilimali.

Kwa sasa Serikali ya Tanzania imejenga barabara inayoelekea kwenye maeneo ya madini hayo. Madini haya yote mkoani Iringa yako katika wilaya kama ifuatavyo:-

**Wilaya ya Iringa:**

Kaolin, Ifunda na Image

Chokaa - Ifunda na Image

**Wilaya ya Mufindi:**

Magnetite na dhahabu - Madawa na Ikimilizo.

Chokaa - Nyanyembe na Ikweha.

**Wilaya ya Njombe**:

Dhahabu - Makanjaula, Kidugala na Mjimwema

Gemstone - Wanging'ombe.

**Wilaya ya Ludewa:**

| | | |
|---|---|---|
| Dhahabu | - | Mchuchuma |
| Chuma | - | Liganga |
| Kimbrlite | - | Nkomang'ombe |
| Almasi | - | Amani na Ibumi |
| Yellowscope | - | Lupingu, Nkomang'ombe, Lwilo na Iwela. |
| Rubby | - | Lwilo na Lupingu |
| Green Tomaline | - | Lupingu, Nkomang'ombe, Lwilo na Iwela. |

**Wilaya ya Makete**:

| | | |
|---|---|---|
| Chuma | - | Lupila na Kata ya Ukwama |
| Dhahabu | - | Usalimwani Kata ya Ikuwo. |
| Kaolin | - | Matamba na Kata ya Mlondwe. |

viii) **<u>Wanyamapori:</u>**

Zipo mbuga za Taifa mbili: Mbuga ya Taifa ya Ruaha yenye ukubwa wa kilometa za mraba 10,300 na mbuga ya Taifa ya Udzungwa yenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,990. Mbuga nyingi zilizopendekezwa kuwa mbuga za kitaifa za wanyama ni Kihongosa, Mpanga na Lunda zote mbili zikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 7,117. Mbuga za wanyama za Ruaha na Udzungwa zina utajiri wa wanyama wengi kama vile, viboko, mamba, simba, tembo n.k. na mimea ya aina mbalimbali. Mto Ruaha umekatisha sehemu ya mashariki mwa mbuga ya Ruaha na kuwa kivutio kikubwa kwa watalii.

**MAENEO YANAYOFAA KWA UWEKEZAJI KIWILAYA MKOANI RINGA, 1997**

| Maeneo ya Uwekezaji | Shughuli za kiuchumi zinazofaa kwa kila Wilaya | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Iringa Mjini | Iringa Vijijini | Mufindi | Njombe | Ludewa | Makete |
| Kilimo | Mboga | Kahawa<br>Tumbaku<br>Alizeti<br>Pamba, Nyanya<br>Vitunguu<br>Viazi Mviringo<br>Mpunga<br>Pareto<br>Mahindi | Kahawa<br>Tumbaku<br>Alizeti<br>Viazi<br>Mviringo<br>Pareto<br>Mahindi | Kahawa<br>Tumbaku<br>Alizeti<br>Nyanya<br>Viazi<br>Mviringo<br>Pareto<br>Mahindi | Kahawa<br>Tumbaku<br>Alizeti<br>Viazi<br>Mviringo<br>Mpunga<br>Pareto<br>Mahindi | Kahawa<br>Alizeti<br>Vitunguu<br>Viazi<br>Mviringo<br>Mpunga<br>Pareto<br>Mahindi |
| Mifugo | Ng'ombe wa Maziwa | Ng'ombe wa maziwa na Nyama | Ng'ombe wa Maziwa na nyama | Ng'ombe wa Maziwa na nyama | Ng'ombe wa Maziwa na nyama | Ng'ombe ya maziwa na nyama |
| Upandaji Miti | Upandaji miti kwa ajili ya Kuni | 1. Upandaji miti kwa ajili ya mbao na kuni.<br>2. Kupanda miti ya matunda ya nchi za baridi na joto. | 1. Upandaji miti kwa ajili ya mbao na kuni.<br>2. Kupanda miti ya matunda ya nchi za baridi na joto. | 1. Upandaji miti kwa ajili ya mbao na kuni.<br>2. Kupanda miti ya matunda ya nchi za baridi na joto. | 1. Upandaji miti kwa ajili ya mbao na kuni.<br>2. Kupanda miti ya matunda ya nchi za badiri na joto. | 1. Upandaji miti kwa ajili ya mbao na kuni.<br>2. Kupanda miti ya matunda ya nchi za baridi na joto. |
| Uvuvi | - | Uvuvi mabwawa ya samaki , Mtera na Mto Ruaha | Uvuaji na mabwawa ya samaki Ngirazil | Uvuvi na mabwawa ya samaki | Uvuvi Ziwa nyasa. | - |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ufugaji Nyuki | - | Ufugaji nyuki | Ufugaji nyuki | Ufugaji nyuki | Ufugaji nyuki | - |
| Wanyamapori | Kujenga hoteli za kitalii | Kujenga kambi na hoteli za kitalii na kujenga barabra katika mbuga za wanyama za Ruaha na Udzungwa. | - | - | - | - |
| Madini | - | Kaolin, Chokaa, Chuma na magnitite | dhahabu na magnitite | Makaa ya mawe, kaolin, soap stone, dhahabu, kimberlite, titano magnitite, manganese oxide, carbonitites | Makaa ya mawe, chuma, dhahabu, kimberlite, almasi, rubby, yellowscope green tomalite. | Shaba, chuma soapstone, kaolin, manganese chrome, ochre. |
| Viwanda | Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo | Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo mfano matunda na chai, ukamuaji, mbegu mafuta. | Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, kukamua mbegu mafuta na pareto | Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kwa kupanua viwanda vya chaii na viwanda vya kukamua mbegu za mafuta. | Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo mdano ukamuaji mbegu mafuta na viwanda vya kusaga nafaka. | Usindikaji matunfa katika makopo. |
| Barabara, njia za majini na mawasiliano | - | Kujenga nyumba za kupangisha. | Kujenga nyumba za kupangisha. | Kujenga nyumba za kupangisha | | |

## KIAMBATISHO "A"

## MKOA WA IRINGA KWA KIFUPI

1.0 **MAHALI ULIPO:**

Mkoa wa Iringa uko katika Nyanda za Juu za Kusini mwa Tanzania, Mkoa umetanda kati ya latitudo 7.. 05.. na 12.. 32.. Kusini na Longitudo 33.. 47.. hadi 36.. 32.. Mashariki mwa Meridiani.

1.1 **MIPAKA YA MKOA:**

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | - | Mkoa wa Dodoma |
| Mashariki | - | Mkoa wa Morogoro |
| Kusini | - | Mkoa wa Ruvuma |
| Kusini Magharibi | - | Ziwa Nyasa |
| Magharibi | - | Mkoa wa Mbeya |

1.2 **ENEO LA ARDHI:**

| | | |
|---|---|---|
| Ardhi | - | Kilometa za mraba 56,864 |
| Maji | - | Kilometa za mraba 2,072 |
| Jumla | - | Kilometa za mraba 58,936 |

1.3 **UTAWALA:**

Wilaya 6, tarafa 31, kata 113 na vijiji 627.

1.4 **IDADI YA WATU:**

- Sensa ya Watu 1988 - Jumla ya 1,208,914 au asilimia 5.3 ya watanzania ambao walikadiriwa kuwa 23,126,952 .
- Makadirio ya mwaka 2000 ni watu 1,678,302
- Kiwango cha ongezeko la watu 2.7 (1988)
- Idadi ya watu kwa kilometa ya mraba 21.2

- Wastani wa watu kwa kaya 4.8

1.5 **MAKABILA:**

- Wahehe 43%
- Wabena 37%
- Wakinga 11%
- Wapangwa 3%
- Mengine (Manda, Kisi) 6%

1.6 **HALI YA HEWA:**

i) **Mvua**

- Uwanda wa juu 1,000-1, 600mm kwa siku 200-280 kwa mwaka
- Uwanda wa kati 600 - 1,000 mm
- Uwanda wa chini 500 - 600mm

ii) **Hali ya Joto:**

Kiwango cha juu cha joto 25%C
Kiwango cha chini cha joto 10%C
Wastani 18C

1.7 **UTALII:**

Utalii uko katika Mbuga za Taifa za Wanyama za Ruaha na Udzungwa.

# KIAMBATISHO "B"

## WILAYA YA IRINGA VIJIJINI

**1.1 MAHALI ILIPO:**

Mipaka:

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | - | Mkoa wa Dodoma |
| Kusini | - | Mkoa wa Morogoro |
| Kusini Magharibi | - | Mkoa wa Mbeya |
| Magharibi | - | Mkoa wa Mbeya |
| Mashariki | - | Mkoa wa Morogoro |

**1.2 ENEO NA IDADI YA WATU:**

- Ardhi - 28,620 km2
- Sensa ya 1998 - Watu 363,605 na ongezeko la watu la 2.7%
- Idadi ya watu kwa Kilometa ya mraba - watu 12.7/km2 (1988)
- Makadirio ya mwaka 2000 watu 500,579
- Wastani wa watu kwa Kaya (1988) - watu 5

**1.3 UTAWALA:**

Tarafa 10, Kata 39 na Vijiji 185

**1.4 MAENEO YA KIUCHUMI:**

- Zaidi ya asilimia 90 ya watu wanaishi vijijini na wanategemea kilimo na ufugaji kama shughuli kuu za kiuchumi.
- Mazao ya chakula: Mahindi, maharage, viazi mviringo na viazi vitamu
- Mazao ya biashara: Chai, Kahawa, Tumbaku, Alizeti na Pamba.

- Ardhi ya Kilimo: 16,607.85 km, 2
  Maeneo ya 1,206.12 km2 (7.2%) zimelimwa.
- Kilimo cha umwagiliaji - Tarafa za Mahenge na Pawaga

1.5 **MIFUGO:**

- Sensa ya Mifugo ya 1984:
  Ngómbe 256,264
  Mbuzi 94,221
  Kondoo 31,462
  Punda 3,448

- Huduma za mifugo: Majosho 64,
  Machinjio 2, vituo vya afya vya mifugo 5, mabanda ya ngozi 6.

1.6 **MISITU NA WANYAMAPORI:**

- Mbuga za Taifa za Wanyama: Ruaha na Udzungwa
- Imependekezwa kuwa hifadhi ya wanyama Lundwa na Kihongosa
- Hifadhi ya misitu eneo: 159,100 Hekta
- Vyanzo vya maji (misitu) Hekta 155,302

1.7 **MADINI:**

Kaolin, Chokaa, Magnitite na Chuma

1.8 **VIWANDA:**

Usagaji wa nafaka, useremala, utengenezaji matofali; cotex, usindikaji matunda; Dabaga, Gereji na Vacum-lug rubber.

1.9 **UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Barabara:

Barabara Kuu - 2.78 kilometa

Barabara za Mkoa - 415.92 kilometa
Barabara za Wilaya - 532 kilometa
Barabara za Vijijini - 834 kilometa

2.1 **ELIMU:**

- Shule za msingi - 187
- Shule za ufundi - -
- Shule za sekondari - 7
- Chuo cha Ualimu - 1

2.2 **AFYA:**

- Hospitali - 1
- Vituo vya Afya- 4
- Zahanati - 53

2.3 **MAJI:**

- Vijiji vyenye maji safi 91
- Watu wanaopata maji safi - 193,835

## KIAMBATISHO "C"

## WILAYA YA NJOMBE

### 1.1 MAHALI ILIPO:

Mipaka

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | - | Wilaya ya Mufindi |
| Mashariki | - | Mkoa wa Morogoro |
| Kusini | - | Wilaya ya Ludewa |
| Magharibi | - | Wilaya ya Makete |

### 1.2 ENEO NA IDADI YA WATU:

- Ardhi - 10,668 km2
- Sensa ya Watu 1988 - watu 315,976
- Ongezeko la kila mwaka - 2.8%
- Idadi ya watu kwa kilometa ya mraba 29.6
- Makadirio ya mwaka 2000 - watu 440,121

### 1.3 UTAWALA:

Tarafa 7, Kata 25 na Vijiji 172

### 1.4 SHUGHULI ZA KIUCHUMI:

- Karibu asilimia 90 ya watu wanaishi vijijini na wanategemea kilimo na ufugaji kwa uchumi.
- Mazao ya chakula: Mahindi, Maharage, Viazi vitamu, viazi mviringo, mtama na ngano.
- Mazao ya biashara: chai, Alizeti, Pareto na Kahawa.
- Eneo la Kilimo: 9,728.75 km2
- Eneo linalolimwa: 1,441.79 km2 (14.8%)

## 1.5 MIFUGO:

- Sensa ya mifugo ya 1984:

| | |
|---|---|
| Ngómbe | 135,275 |
| Mbuzi | 36,596 |
| Kondoo | 25,870 |

- Huduma za mifugo: Majosho 34, machinjio 7, Vibanio 2, Mabanda ya Ngozi 7.

## 1.6 MISITU NA WANYAMAPORI:

- Hifadhi ya misitu - 20 yenye ukubwa wa hekta 17,146
- Mapori kwenye vyanzo vya maji - 6 yenye ukubwa wa Hekta 23,026

## 1.7 MADINI:

Manganese oxide, titano magnetite, carbonates, makaa ya mawe, kaolin, soap stone, dhahabu, kimbelite.

## 1.8 VIWANDA:

Usindikizaji wa chai na mafuta, usindikaji wa miwati, useremala, utengenezaji matofali, usagaji wa nafaka.

## 1.9 BARABARA NA MAWASILIANO:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Barabara Kuu | - | 140.0 km |
| - | Barabara za Mkoa | - | 276.21 km |
| - | Barabara za Wilaya | - | 430.0 km |
| - | Barabara za Vijijini | - | 656 km |

## 2.0 ELIMU:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Shule za msingi | - | 205 |
| - | Shule za Ufundi- | - | |
| - | Shule za Sekondari | - | 11 |

## 2.1 AFYA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Hospitali | - | 3 |
| - | Vituo vya Afya- | | 3 |
| - | Zahanati | - | 33 |

## 2.2 MAJI:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Vijiji vyenye maji safi | - | 74 |
| - | Watu wenye maji safi | - | 185,311 |

## KIAMBATISHO "D"

## WILAYA YA MAKETE

1.1 **Mipaka**

| | | |
|---|---|---|
| Kusini | - | Wilaya ya Ludewa |
| Magharibi | - | Mkoa wa Mbeya na Ziwa Nyasa |
| Kaskazini na Mashariki | - | Wilaya ya Njombe |

1.2 **ENEO NA IDADI YA WATU:**

- Ardhi - 4128 km2
- Sensa ya 1988 - watu 115,480
- Idadi ya watu kwa Kilometa ya mraba - 28
- Makadirio ya mwaka 2000 - watu 135,357
- Ongezeko la watu kila mwaka - 1.2 (Sensa ya Idadi 1988)

1.3 **UTAWALA:**

Tarafa 5, Kata 15, na vijiji 95

1.4 **SHUGHULI ZA KIUCHUMI:**

- Asilimia 95 ya watu wanaishi vijijini na wanashughulika na kilimo
- Mazao ya Chakula: Viazi mviringo, mahindi, ngano, maharage, viazi vitamu, mpunga na mtama.
- Mazao ya biashara - Pareto na Kahawa
- Eneo la Kilimo: 4,195 km2 na eneo linalolimwa 320.37 km2 (7.6%)

1.5 **MIFUGO:** - Sensa ya Mifugo ya 1984:

Ngómbe - 23,730
Mbuzi - 19,609
Kondoo - 9,795

Punda - 144

1.6 **MISITU:**

- Misitu ya Hifadhi - 6 ya eneo la 23,026 hekta
- Misitu kwenye Vyanzo vya maji Hekta 44,495.

1.7 **MADINI:**

Shaba, chuma, soap stone, Kaolin, Manganese, chrome, dhahabu na ochre.

1.8 **VIWANDA:**

- Viwanda vya mbao, usagaji nafaka na ufinyanzi wa vyungu.

1.9 **BARABARA:**

- Barabara Kuu - 12.0 km
- Barabara za Mkoa - 230.38 km
- Barabara za Wilaya - 188.0 km
- Barabara za Vijijini - 314.0 km

2.0 **ELIMU:**

- Shule za Msingi - 87
- Shule za Ufundi - -
- Shule za Sekondari - 4
- Vyuo vya Ualimu - 1

2.1 **AFYA:**

- Hospitali - 3
- Vituo vya Afya - 3
- Zahanati - 21

2.2 **MAJI:**

- Vijiji vyenye maji safi - 37

- Watu wenye maji safi - 40,287

## KIAMBATISHO "E"

## WILAYA YA LUDEWA

### 1.1 MAHALI ILIPO:

**MIPAKA**

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | - | Wilaya ya Njombe |
| Kusini na Mashariki | - | Mkoa wa Ruvuma |
| Magharibi | - | Ziwa Nyasa |

### 1.2 ENEO NA IDADI YA WATU:

- Ardhi - 6,325 km2
- Sensa ya Idadi ya 1988 - watu 99,689
- Idadi ya watu kwa kilometa ya mraba 15.8
- Wastani wa ukubwa wa kaya sensa ya 1988 - watu 4.9
- Makadirio ya watu mwaka 2000 - 138,858
- Ongezeko la watu kwa kila mwaka

### 1.3 UTAWALA:

Tarafa 4, Kata 20, Vijiji 50

### 1.4 SHUGHULI ZA KIUCHUMI:

- Asilimia 95 ya watu wanaishi vijijini na wanategemea kilimo na ufugaji kiuchumi
- Mazao ya chakula: mahindi, mtama, ngano, maharage na muhogo.
- Mazao ya Biashara - Kahawa, Alizeti, Tumbaku na Pareto
- Eneo la Kilimo - 4,195 km2 na eneo linalolimwa 344.44 km2 (7.4%)

## 1.5 MIFUGO:

- Sensa ya Mifugo ya 1984:

| | | |
|---|---|---|
| Ngómbe | - | 30,650 |
| Mbuzi | - | 16,035 |
| Kondoo | - | 4,493 |
| Punda | - | 180 |

- Huduma ya Mifugo: Majosho - 9, machinjio -3, vibanio - 1, mabanda ya ngozi - 3.

## 1.6 MISITU:

- Misitu ya hifadhi - 4 ya eneo la hekta 7,504
- Misitu kwenye vyanzo vya maji - Hekta 7,500

## 1.7 MADINI:

- Makaa ya Mawe, chuma eneo la Liganga na Mchuchuma.
- Dhahabu, Kimberlite, Almasi, Yelloscope rubby, green tomaline.

## 1.8 VIWANDA:

Viwanda vya mbao, ukamuaji mafuta, na usagaji nafaka.

## 1.9 BARABARA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Barabara Kuu | - | 179.59 km |
| - | Barabara za Mkoa | - | 80.34 km |
| - | Barabara za Wilaya | - | 565.0 km |

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Barabara za Vijijini | - | 320.0 km |

2.0 **ELIMU:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Shule za msingi | - | 77 |
| - | Shule za Ufundi- | - | |
| - | Shule za Sekondari | - | 2 |

2.1 **AFYA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Hospitali | - | 3 |
| - | Vituo vya Afya - | 3 | |
| - | Zahanati | - | 31 |

2.2 **MAJI:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Vijiji vyenye maji safi | - | 23 |
| - | Watu wenye maji safi | - | 53,665 |

# KIAMBATISHO F

## WILAYA YA MUFINDI

1.1 **MAHALI ILIPO**:

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | - | Wilaya ya Iringa Vijijini |
| Mashariki | - | Mkoa wa Morogoro |
| Kusini | - | Wilaya ya Njombe |
| Magharibi | - | Mkoa wa Mbeya |

1.2 **ENEO NA IDADI YA WATU:**

- Ardhi - 7,123 km2
- Sensa ya Watu 1988 - Watu 173,824
- Idadi ya Watu kwa kilometa ya mraba - 32.2
- Makadirio ya watu mwaka 2000 - 319,481
- Wastani wa ukubwa wa Kaya (1988) watu 4.8
- Ongezeko la watu kwa mwaka 2.8%

1.3 **UTAWALA:**

Tarafa 5, kata 14 na Vijiji 126

1.4 **SHUGHULI ZA KIUCHUMI:**

- Zaidi ya asilimia 90 ya watu wanaishi vijijini na wanategemea kilimo na ufugaji kiuchumi.
- Mazao ya chakula - mahindi, viazi vitamu, viazi mviringo, maharage na uwele.
- Mazao ya Biashara - Chai, Kahawa, Pareto na Alizeti.
- Eneo la Kilimo - 6,765.9 km2 na eneo linalolimwa - 1,331.5 km2

## 1.5 MIFUGO:

- Sensa ya Watu 1984 ya mifugo:

| | | |
|---|---|---|
| Ngómbe | - | 81,873 |
| Mbuzi | - | 12,413 |
| Kondoo | - | 7,616 |
| Punda | - | 180 |

- Huduma ya mifugo - Majosho 40, machinjio 7, vibanio 8, mabanda ya ngozi 2.

## 1.6 MISITU NA WANYAMAPORI:

- Misitu ya Hifadhi - 23, ya hekta 47,338
- Misitu ya hifadhi kwenye vyanzo vya maji 18 ya ukubwa wa hekta 16,690.

## 1.7 MADINI:

Dhahabu na Magnetite

## 1.8 VIWANDA:

Usindikaji wa chai na pareto, viwanda vya mbao, kiwanda cha karatasi, upasuaji mbao, usagaji nafaka na utengenezaji matofali.

## 1.9 BARABARA NA MAWASILIANO:

| | | |
|---|---|---|
| - Barabara Kuu | - | 178 km |
| - Barabara za Mkoa | - | 210.03 km |
| - Barabara za Wilaya | - | 360.0 km |
| - Barabara za Vijijini | - | 475.0 km |

- Kiwanja cha ndege - 1

2.0 **ELIMU (1995):**

- Shule za msingi - 138
- Shule za Ufundi- -
- Shule za Sekondari - 14

2.1 **AFYA:**

- Hospitali - 3
- Vituo vya Afya- 5
- Zahanati - 45

2.2 **MAJI:**

- Idadi ya Vijiji vyenye maji safi - 45
- Idadi ya Watu wenye maji safi - 154,500

## KIAMBATISHO G

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU TANZANIA

### 1.1 MAHALI ILIPO:

Longitudo $29^0$-$41^0$ Mashariki mwa Griniwichi na Latitudo $1^0$-$12^0$ kusini mwa Ikweta.

### 1.2 MIPAKA YA NCHI:

| | |
|---|---|
| Kaskazini: | Kenya na Uganda |
| Magharibi: | Burundi, Rwanda na Zaire |
| Kusini: | Zambia, Malawi na Mozambique |
| Mashariki: | Bahari ya Hindi |

### 1.3 UKUBWA/ENEO:

| | |
|---|---|
| Nchi kavu: | 881,289 $km^2$ |
| Maji (bara): | 61,495 $km^2$ |
| Jumla: | 942,784 $Km^2$ |

### 1.4 UKUBWA WA ENEO LA KILA MKOA TANZANIA BARA ($Km^2$):

**TANZANIA 942,784**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Arusha | 84,567 | Morogoro | 70,799 |
| Pwani | 32,407 | Tanga | 35,248 |
| Dodoma | 41,311 | Lindi | 66,046 |
| **Iringa** | **58,936** | D'Salaam | 1,393 |
| Kigoma | 45,066 | Rukwa | 75,240 |
| Kagera | 39,627 | Ruvuma | 66,477 |
| Kilimanjaro | 13,309 | Shinyanga | 50,781 |
| Mara | 30,150 | Singida | 49,341 |
| Mbeya | 62,420 | Tabora | 76,151 |
| Mtwara | 16,707 | Tanga | 26,808 |

## 1.5 IDADI YA WATU:

**HESABU YA IDADI YA WATU NA WASTANI WA UMRI WA KUISHI NCHINI TANZANIA KATIKA KILA MKOA 1967, 1978, 1988, 1996**

| MKOA | IDADI YA WATU | | | | UMRI WA KUISHI (WASTANI) 1988 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1967 (No.) | 1978 (No.) | 1988 ('000) | 1996** ('000) | Me Miaka | Ke Miaka |
| Dodoma | 709,380 | 972,005 | 1,234.9 | 1,472.5 | 45 | 47 |
| Arusha | 610,474 | 926,223 | 1,348.4 | 1,784.0 | 57 | 58 |
| Kilimanjaro | 652,722 | 902,437 | 1,106.0 | 1,703.5 | 57 | 62 |
| Tanga | 771,060 | 1,037,767 | 1,307.3 | 1,521.8 | 48 | 51 |
| Morogoro | 682,700 | 939,264 | 1,254.0 | 1,519.4 | 45 | 48 |
| Pwani | 428,041 | 516,586 | 636.5 | 740.9 | 46 | 51 |
| Dar es Salaam | 356,286 | 843,090 | 1,357.6 | 1,945.7 | 50 | 50 |
| Lindi | 419,853 | 527,624 | 645.0 | 744.8 | 46 | 48 |
| Mtwara | 621,293 | 771,818 | 887.4 | 976.7 | 44 | 48 |
| Ruvuma | 395,447 | 561,575 | 781.4 | 1,001.3 | 48 | 50 |
| **Iringa** | **689,905** | **925,044** | **1,206.0** | **1,472.9** | **44** | **47** |
| Mbeya | 753,765 | 1,079,864 | 1,472.7 | 1,857.0 | 45 | 48 |
| Singida | 457,938 | 613,949 | 789.9 | 949.4 | 54 | 55 |
| Tabora | 502,068 | 817,907 | 1,033.8 | 1,232.6 | 53 | 54 |
| Rukwa | 276,091 | 451,897 | 693.3 | 954.7 | 44 | 47 |
| Kigoma | 473,443 | 648,941 | 857.8 | 1,047.6 | 47 | 49 |
| Shinyanga | 899,468 | 1,323,535 | 1,768.6 | 2,194.83 | 48 | 51 |
| Kagera | 658,712 | 1,009,767 | 1,358.8 | 1,659.5 | 44 | 45 |
| Mwanza | 1,055,883 | 1,443,379 | 1,874.4 | 2,270.9 | 48 | 50 |
| Mara | 544,125 | 723,827 | 968.6 | 1,202.0 | 46 | 48 |
| Tanzania Bara | 11,958,654 | 17,036,499 | 22,582.4 | 28,252.2 | 49 | 51 |
| Zanzibar Kaskazini | 56,360 | 77,017 | 97.1 | 119.0 | 46 | 52 |
| Zanzibar Kusini | 39,087 | 51,749 | 70.2 | 91.8 | 46 | 48 |
| Zanzibar Mjini | 95,047 | 142,041 | 208.4 | 290.4 | 45 | 50 |
| Pemba Kaskazini | 72,015 | 106,290 | 137.4 | 172.6 | 46 | 47 |
| Pemba Kusini | 92,306 | 99,014 | 127.7 | 160.4 | 45 | 50 |
| Zanzibar | 354,815 | 476,111 | 640.7 | 834.2 | 45 | 49 |
| Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 12,313,469 | 17,512,610 | 23,223.1 | 29,086.4 | 49 | 51 |

Chanzo: Idara ya Takwimu

**MAELEZO: Idadi ya Watu 1996 ni makadirio kutokana na mwenendo wa ukuaji wa Idadi ya hesabu ya watu tangu sensa ya mwaka 1978 hadi 1988.

## 1.6 MATUMIZI YA ARDHI (HA):

| | | (Hekta milioni) | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Mashamba Madogo | - | 4.1 | - | 5 |
| Mashamba Makubwa | - | 1.1 | - | 1 |
| Malisho | - | 35.0 | - | 39 |
| Misitu na Miti | - | 44.0 | - | 50 |
| Ardhi nyingine | - | 4.4 | - | 5 |
| **Jumla** | **-** | **88.6** | **-** | **100** |

## 1.7 ARDHI KWA AJILI YA KILIMO NA MIFUGO:

Ardhi inayofaa kwa kulimwa na mifugo (Ha.) 3,634,000

## 1.8 MAZIWA:

| | | |
|---|---|---|
| Victoria | - | 34,850 $km^2$ |
| Tanganyika | - | 13,350 $km^2$ |
| Nyasa | - | 5,600 $km^2$ |
| Rukwa | - | 2,850 $km^2$ |
| Eyasi | - | 1,050 $km^2$ |
| Natron | - | 900 $km^2$ |
| Manyara | - | 320 $km^2$ |

## 1.9 MILIMA: (Mita za urefu kutoka usawa wa Bahari)

| | | |
|---|---|---|
| Kilimanjaro: | - | 5,895 |
| Meru: | - | 4,566 |

## 1.10 HALI YA HEWA:

### (a) MVUA:

Kuna misimu miwili ya mvua moja ni Vuli: Mvua hunyesha kati ya miezi ya Oktoba na Desemba na pili ni Masika: Mvua hunyesha kati ya miezi ya Machi na Mei.

Mtawanyiko wa mvua ni mzuri katika mwaka mzima ingawa zipo tofauti kati ya sehemu mbalimbali

Mvua nyingi hunyesha hasa katika miezi ya Machi na Mei

### (b) HALI YA JOTO:

Wastani wa juu wa joto (Nyuzijoto)

| | **Januari**. | **Aprili** | **Julai** | **Oktoba** |
|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 31.6 | 30.1 | 28.6 | 31.3 |
| Arusha | 28.9 | 25.3 | 21.1 | 27.3 |
| Dodoma | 31.4 | 28.4 | 26.0 | 30.2 |

Wastani wa kiwango cha chini wa halijoto (Nyuzijoto)

| | **Januari**. | **Aprili** | **Julai** | **Oktoba** |
|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 23.3 | 22.9 | 18.3 | 31.3 |
| Arusha | 12.2 | 16.9 | 12.6 | 27.3 |
| Dodoma | 19.2 | 13.5 | 16.2 | 30.2 |

1.11 **PATO LA TAIFA (1996)**

| | | |
|---|---|---|
| Kwa bei za mwaka unaohusika (Tsh.milioni) | - | 3,317,634 |
| Kwa bei za mwaka 1992 (Tsh.milioni) | - | 1,354,038 |

1.12 **WASTANI WA PATO LA MTU BINAFSI (1996)**

| | | |
|---|---|---|
| Kwa bei za mwaka unaohusika (Tsh.) | - | 117,230.9 |
| Kwa bei za mwaka 1992 (Tsh.) | - | 47,845.9 |

## 2.0 HUDUMA ZA JAMII

### 2.1 AFYA:

Idadi ya Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati

| MWAKA | HOSPITALI | VITUO VYA AFYA | ZAHANATI |
|---|---|---|---|
| 1960 | 98 22 | 975 | |
| 1980 | 149 239 | 2,600 | |
| 1990 | 173 276 | 3,014 | |

### 2.2 ELIMU:

Ulinganisho wa kiwango cha kuandikisha wanafunzi katika mashule kati ya nchi za Afrika Mashariki 1995.

| NCHI | IDADI | |
|---|---|---|
| | SHULE ZA MSINGI | SHULE ZA SEKONDARI |
| KENYA | 94 | 28 |
| UGANDA | 76 | 20 |
| TANZANIA | 67 | 13 |

## 2.3 MAJI:

Hali ya usambazaji wa huduma ya maji safi mijini na vijijini Tanzania Bara 1994

| JUMLA YA WATU (000) | IDADI YA WATU MJINI (000) | WANAO PATA MAJI (000) | % | IDADI YA WATU VIJIJINI (000) | WANAOPATA MAJI (000) | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 27,061.7 | 5,363.4 | 3,668.6 | 68.5 | 21,698.3 | 10,046.3 | 46.3 |

Chanzo: Wizara ya Maji, Madini na Nishati, 1994

## 3.0 HIFADHI ZA TAIFA:

| JINA LA HIFADHI | MAHALI ILIPO NA MAELEZO MUHIMU |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI** | **MAHALI ILIPO:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ipo karibu na mpaka wa Mkoa wa Arusha na Mara, mwendo wa kilometa 32 kutoka mjini Arusha.<br><br>**UKUBWA:**<br>Hifadhi ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 14,763. Ni hifadhi iliyokubwa zaidi na ya zamani Tanzania iliyoendelezwa baada ya kuanzishwa na wakoloni wa Kiingereza mwaka 1951.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Kongoni kiasi cha 1.7 milioni, Simba 3,000, Spishi 35 za wanyama pori na 500 za ndege , pia wamo Nyati, Duma, Chui n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA LAKE MANYARA** | **MAHALI ILIPO:**<br>Ipo kiasi cha kilometa 125 kusini magharibi mwa mji wa Arusha.<br><br>**UKUBWA:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Lake Manyara ina ukubwa wa kilo meta za mraba 320. Kati ya hizo kilometa 230 za mraba ni eneo la Ziwa Manyara.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Bonde la Ufa kwa upande wa magharibi na Ziwa kubwa (Manyara) kwa upande wa chini. Misitu yenye mito na chemchemi asili. Simba wenye kukwea mitini, aina mbalimbali za hayawani na anuwai 360 za ndege wakiwemo Tembo, Viboko, Chui, Nyani n.k. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA TARANGIRE** | **MAHALI ILIPO:**<br>Kusini mwa mji wa Arusha kando kando ya barabara kuu iendayo Dodoma. Hifadhi imeanzishwa mwaka 1970.<br><br>**UKUBWA:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ina eneo la kilometa za mraba 2,600.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Chatu wenye kukwea mitini, Pundamilia, Kongoni, Tembo, Nyati, Swala, Choroa n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA ARUSHA (MONELLA)** | **MAHALI ILIPO:**<br>Hifadhi ipo katikati ya mlima Meru na mlima Kilimanjaro. Mwanzoni ilijulikana kama hifadhi ya Taifa ya Ngudoto hadi mwaka 1967. Ilipewa hadhi ya kuwa hifadhi ya Taifa Mwaka 1960.<br><br>**UKUBWA:**<br>Ukubwa wa eneo la hifadhi hii ni kilometa za mraba 140.<br><br>**VIVUTIO:**<br>"Ngudoto Crater", Ziwa Momela, mlima Meru, na misitu ya asili ya Momela. Anuwai mbalimbali za wanyama pori na ndege. Wanaofahamika zaidi ni pamoja na Tembo, Viboko, Nyani, Funo/Mindi na aina mbalimbali za ndege. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA KILIMANJARO** | **MAHALI ILIPO:**<br>Hifadhi ya Kilimanjaro ipo katika mlima wa Kilimanjaro ambao ndio chimbuko la jina lake. Hifadhi hii imeanzishwa mwaka 1973.<br><br>**UKUBWA:**<br>Mipaka yake inajumuisha misitu ya asili iliyopo maeneo yote ya chini na pembezoni/karibu na mlima. Ukubwa wa eneo la hifadhi ni kilometa za mraba 760.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Mlima Kilimanjaro na vilele vyake vitatu: Shira (3,962 meta), Mawenzi (5,149 meta) na Kibo (5,895 meta) juu ya usawa wa bahari. Zipo pia anuwai mbalimbali za wanyama pori na ndege. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA MIKUMI** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi hii ipo kiasi cha kilometa 216 kando kando mwa barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Zambia eneo la Mikumi Mkoa wa Morogoro/Iringa. Imeanzishwa mwaka 1964.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Mikumi hupakana na hifadhi kubwa ya wanyama kuliko zote katika Afrika ya Selous. Ni ya tatu kati ya hifadhi za Taifa kubwa ikipitwa tu na hifadhi za Serengeti na Ruaha. Ina eneo la kilometa za mraba 3,230.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Tambarare zinazozunguka mto Mkata. Utajiri mkubwa wa Flora na Fauna aina aina. Namna mbalimbali za wanyama pori wakiwemo Tembo, Pundamilia, Nyati, Twiga, Viboko, Simba, Swalapala n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA UDZUNGWA** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi hii ipo kusini mwa hifadhi ya Taifa ya Mikumi kando kando mwa barabara kuu ya Mikumi-Ifakara. Ilianzishwa mwaka 1992.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa ambayo asili ya jina lake linatokana na milima maarufu ya Udzungwa ina eneo la kilometa za mraba 1990.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Namna mbalimbali na za kipekee za Fauna na Flora zilizopelekea ipewe hadhi ya kuwa hifadhi ya Taifa. Milima ya Udzungwa ambayo ni chanzo asili cha mito na chemchemi za maji, ukiwepo mto maarufu wa kilombero wenye kumwagilia shamba la hekta nyingi za kilimo cha miwa la kilombero. Vivutio vingine ni wanyama pori: Simba, Nyati, Twiga n.k. |
| **HIFADHI YA TAFIA YA RUAHA** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Jina Ruaha hutokana na neno la kihehe **"Luvaha"** likimaanisha mto. Hifadhi hii ipo kilometa 130 magharibi mwa mji wa Iringa.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ina ukubwa wa kilometa za mraba 12,950. Ni ya pili kwa ukubwa nchini na imeanzishwa mwaka 1964.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Mto wa Ruaha ni mojawapo yakivutio kikubwa. Mamia ya namna mbalimbali za Flora. Wanyama aina aina wakiwemo Mamba, Viboko, Tembo n.k. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA KATAVI** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Katavi ipo wilayani Mpanda Mkoa wa Rukwa. Ilianzishwa mwaka 1974.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Katavi iliyopo kiasi cha umbali wa kilometa 40 kusini mashariki mwa mji wa Mpanda ina ukubwa wa kilometa za mraba 2253.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Ziwa Chala na Chada pamoja na Chemchemi na mito ambayo maji yake hutiririka kwenye Ziwa Rukwa ni vivutio vya kipekee kwa watalii katika/ kwenye hifadhi hii. Wanyama mbalimbali wakiwemo Pundamilia, Mbelele, Pofu, Chui, Nyati, Simba, Tembo, Paa/Palakala, Kulungu n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA MAHALE** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Ikiwa umbali wa kiasi cha kilometa 120 kusini mwa mji wa Kigoma na kandokando ya ufukwe wa Ziwa Tanganyika, hifadhi ya Taifa ya Mahale ni kivutio kingine maarufu katika urithi wa maliasili za Tanzania.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Mahale ina ukubwa wa karibu kilometa za mraba 410 na ilichapishwa kwenye gazeti la serikali mwaka 1948.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Idadi kubwa ya Sokwe ni mojawapo ya kivutio cha kusisimua katika hifadhi hii. Ipo pia idadi nzuri ya Nyani wa namna mbalimbali wakiwemo aina ya nyani wekundu wajulikanao kwa lugha ya kiingereza kama "Red Colobus Monkey". |
| **HIFADHI YA TAIFA YA RUBONDO** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi hii ipo kati ya mojawapo ya vifungu visiwa (Archiplelagos) vilivyopo katika Ziwa Victoria.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 460 na imeanzishwa mwaka 1977.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Sokwe na namna mbalimbali za wanyama pori wakiwemo Viboko, Twiga na Tembo. Kutokuwepo kwa Simba wala watu na Chui ni hakikisho tosha kuivinjari hifadhi kwa usalama na pia kufanya shughuli za uvuvi wa boti kwa msaada wa "wadeni" au mlinzi wa hifadhi. |
| **HIFADHI YA TAFIA YA NGORONGORO** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Ngorongoro ipo magharibi mwa mji wa Arusha umbali wa kiasi cha kilometa 230.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi hii ina ukubwa wa kilometa za mraba 8,320.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Kongoni, Simba, Nyati, Chui, Anuwai mbalimbali za ndege, Twiga, Tembo n.k. Inakadiriwa kwamba wapo Sokwe 700 katika hifadhi ya Taifa ya Mahale na anuwai 15 za Nyani ambazo makazi yao ya asili ni sawa na yale ya Sokwe. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA GOMBE** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Gombe ipo kilometa 16 kusini ya mji wa kigoma magharibi mwa Tanzania. Ni mwanya mwembamba wa eneo la milima linalopakana kwa upande wa magharibi na bonde la Ufa na Ziwa Tanganyika kwa upande wa mashariki.<br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Ina ukubwa wa kiasi cha kilometa za mraba 52 na ilianzishwa mwaka 1968.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Misitu ya kijani kibichi cha kudumu na mamalia wa hali ya juu wakiwemo Sokwe na anuwai mbalimbali za Nyani - wakiwemo Mbega (Red Colobus), Nyani (Baboons), Nyani wekundu/Bluu na Ngedere. |